
SUPA JACKPOT
TZS.1,046,433,814
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**RIPOTI MAALUM:** Mtihani wananchi waliosababisha maji kuyavamia makazi




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Novemba 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581120
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# HOFU YATANDA

**WAKAZI** katika nyumba 48 waondolewa kwa amri ya mahakama, wahusika walonga... *Endelea Ukurasa wa 2*



Baadhi ya wakazi wa Majohe Halisi, jijini Dar es Salaam, wakiwa wametoa vitu vyao nje jana, baada ya kutakiwa kuhama kwenye nyumba zao walizokuwa wakiishi kwa amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Ardhi, kwa kile kinachodaiwa kuwa zimejengwa kwenye eneo la mtu. **Picha nyingine:** Askari polisi wakisimamia zoezi hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wanafunzi wadaiwa kuingilia mfumo, waghushi malipo ada

UKURASA 3

## Vigogo Bodi ya mikopo wawekwa kitimoto saa mbili

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA KAZI MOJA TU KWA CLUB AFRICAIN UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Mkurungenzi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Abdul-Razaq Badru (wa pili kulia), akiwa na wajumbe na wafanyakazi wa Bodi hiyo, wakitoka Bungeni, jijini Dodoma jana, baada ya kumaliza kuhojiwa na Kamati ya Bunge Huduma na Maendeleo ya Jamii. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hofu yatanda wakazi nyumba 48 kuondolewa

**Na Waandishi Wetu**

FAMILIA katika nyumba 48 zilizoko Majohe Halisi, Pugu, jijini Dar es Salaam, zimeondolewa ndani kwa amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Ardhi, baada ya mmiliki halali wa eneo hilo kushinda kesi.

Amri hiyo ya mahakama ilitoka Jumatano na siku iliyofuata mamia ya wananchi wa eneo hilo, walipewa taarifa ya kutakiwa kuondoka kwenye nyumba huku zingine 22 wamiliki wake wakitakiwa kubaki kwa sababu walishamalizana na mmiliki huyo baada ya kulipa fedha walizotakiwa.

Nipashe ilishuhudia jana mamia ya wanafamilia wakiondoa vitu kwenye nyumba zao huku wengine wakiwa wamekaa hapo zaidi ya miaka 10 lakini baadhi wakibaki kwa madai wakati kesi hiyo ikiendelea mahakamani, walikubali kufuata sharti la mmiliki huyo la kulipa Sh. 150,000.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya wananchi hao walisema wanalazimika kulala nje na watoto wao pamoja na mali zao baada ya kuondolewa kwenye nyumba.

Lilian Ubisimbali, mwenye eneo la ekari mbili, alisema alilinunua mwaka 1990 kutoka kwa mtu aliyemtaja kwa majina ya Samwel Kwabu kwa Sh. 300,000 na kujenga nyumba ya vyumba vitatu.

"Ilipofika mwaka 2008 alikuja kijana anayefanya kazi ya Baharia aitwaye Emmanuel Kwabu, mjukuu wa mzee Kwabu ambaye sasa ni marehemu, akawa anawataka majirani zangu wampe Sh. 150,000 kwa sababu wanakaa kwenye eneo ambalo si lao.

"Baada ya muda akarudi tena upande wetu, akasema eneo letu ni lake, akasema alikuwa baharia sasa amerejea nchini na eneo lote lina ukubwa wa ekari 10.

Alisema Emmanuel alikwenda mahakamani mara ya kwanza lakini wananchi walishinda kesi na alipokata rufani ndipo akashinda.

"Jana (juzi) nikiwa nyumbani ndipo tangazo likawa linatangazwa likitutaka ifikapo leo (jana) saa 2:00 asubuhi, tutoe vitu vyote vilivyomo ndani ya nyumba na tukae mita 10.

"Binafsi ninauguliwa na mama yangu mzazi amepooza. Baada ya tangazo hilo, nilijaribu kuomba msaada lakini amri ikawa ni ile ile iliyotolewa, hivyo nimelazimika kutoka na sasa ninapeleka vitu Shule ya Sekondari Halisi. Nimeomba darasa moja nihifadhi vitu," alisema huku akibainisha kuwa familia yao ina watu 10 wakiwamo wazazi wao.

Agnes Wangisati, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema eneo lao lina ukubwa wa kujenga nyumba nne na wamejenga fremu tatu mbele ndani ya familia yao kwa sasa wanalala nje na familia ina watu 10 na wapangaji watatu.

Alisema walianza kuishi maeneo hayo tangu mwaka 2005 na wameshangaa kitendo kilichofanywa na Emmanuel.

Mwanaharusi Bintimzee (70) kwa upande wake ni kicheko baada ya mmiliki halali wa eneo hilo kumtaka abaki. Aliliambia gazeti hili kuwa baada ya tangazo hilo kutolewa, alitii amri yake lakini baada ya muda, alifuatwa na watu na kuambiwa kuwa mmiliki amemtaka abaki hapo.

"Lakini baadaye ndipo akajitokeza hUondoaji wa wananchi hao ulisimamiwa na askari wa Jeshi la Polisi ambao wakati wote walihakikisha kuwapo kwa usalama eneo hilo pamoja na walinzi wengine ambao wamebaki hapo kulinda.

**IMEANDALIWA na Jumanne Juma na Romana Mallya.**

# Vigogo bodi ya mikopo wawekwa kitimoto

**Na Richard Makore,** DODOMA

VIGOGO wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB), wamewekwa kitimoto na Kamati ya Kudumu ya Bunge na Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa takribani saa mbili, jijini hapa.

Kuhojiwa kwa vigogo hao kunatokana na madai ya kugomea maagizo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ya kutaka timu iliyoundwa kuchunguza mifumo ya bodi hiyo katika utoaji wa mikopo.

Watumishi hao wa bodi waliingia katika ukumbi ambao kamati hiyo ilikuwa ikifanya kikao chake saa 9:00 alasiri hadi saa 11:00 jioni.

Akizungumza baada ya kuwahoji watumishi hao, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, alisema walipata ushirikiano kutoka bodi hiyo na vitu walivyopanga kuwauliza walijibiwa.

Hata hivyo, Nyongo alikataa kuzungumzia suala hilo kiundani kwa madai kuwa ripoti kamili inatarajiwa kuwasilishwa bungeni kama Spika alivyoelekeza Jumanne wiki hii.

Alisema mwenyekiti wa bodi, mkurugenzi mtendaji na viongozi wengine waandamizi walifika mbele ya kamati hiyo kama alivyoagiza Spika.

Nyongo alisema kabla ya viongozi hao kuanza kuhojiwa, waliwahoji pia viongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakiongozwa na Waziri, Prof. Mkenda.

Akizungumza baada ya kumalizika kikao hicho, Meneja Habari na Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole, alikiri kuitwa mbele ya kamati kwa ajili ya kuhojiwa. Viongozi wa bodi waliofika mbele ya kamati na kuhojiwa ni pamoja na Mwenyekiti wake, Prof. Hamisi Dihenga na Mkurugenzi Mtendaji, Abdul-Razaq Badru.

Jumanne wiki hii, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliagiza viongozi wa bodi kufika mbele ya kamati hiyo na kuhojiwa ni kwa nini wanaonyesha kiburi na kugoma kutekeleza maagizo ya Waziri.

"Mheshimiwa mwenyekiti naagiza bodi hiyo ifike mbele ya kamati Ijumaa wiki hii ili waje wajibu hiki kiburi wanakitoa wapi mpaka kumgomea waziri," alisema Spika.

Kabla ya Spika kutoa agizo hilo, Waziri Mkenda alisimama bungeni wiki hii na kueleza namna anavyopata ugumu anapotoa maagizo kwa bodi hiyo.

"Nashindwa kuelewa Mheshimiwa Spika. Napata upinzani mkali sana tangu nilipoteua timu ya wataalam kwenda kuchunguza mifumo ya utoaji mikopo ya bodi hiyo," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo, Spika akaagiza viongozi wa bodi hiyo wafike mbele ya kamati kwa ajili ya kuhojiwa ili bunge lijue sababu ya kuweka upinzani wakati timu hiyo ya wataalam ilipotaka kufanya kazi.

# Usingizi hafifu chanzo maradhi yasiyoambukiza

**Na Romana Malllya**

MTAALAM wa Afya na Mazoezi kutoka Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza, Dk. Waziri Ndonde, amesema moja ya sababu inayochangia watu kupata magonjwa yasiyoambukiza ni kutopata usingizi wa kutosha.

Akizungumza na Nipashe jana, mtaalam huyo alisema kwa kawaida mtu mzima hutakiwa kulala saa saba hizo mfululizo nyakati za usiku lakini wengi hawafanyi hivyo.

"Magonjwa yasiyoambukiza yanachangiwa na mambo matatu. Kwanza, kukosa usingizi wa kutosha, pili, kutofanya mazoezi na kula vyakula bila mpangilio," alibainisha.

Kutokana na hali hiyo, alisema wanaendelea kuelimisha makundi mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari ili wasaidie kuelimisha jamii isiendelee kupata maradhi hayo.

"Kwa sasa tunawaelimisha waandishi wa habari wa mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita, Kagera, Mara na Mwanza. Tunawapa mafunzo ya uelewa wa kujikinga wao wenyewe lakini, namna ya utoaji wa taarifa za magonjwa yasiyoambukiza ili kujenga uelewa mpana ndani ya jamii," alisema.

Dk. Ndonde alisema ziko sababu nyingi zinazochangia magonjwa hayo, lakini mfumo wa afya ulivyo unahitaji vitu vitatu ili mtu awe na afya bora ambavyo ni kula vizuri, kufanya mazoezi na kupata usingizi wa kutosha ambao si chini ya saa saba kwa mtu mzima.

"Wastani wa mtu kulala usiku ni saa saba. Hivi vitu vitatu mtu akivizingatia, vitamwepusha kupata magonjwa. Mwili utakuwa unajengeka na kinga, kwa nini kulala, mtu anapofanya shughuli zake siku nzima, unapokwenda kulala mwili unajengeka.

" Unapofanya shughuli tishu zilizoko kwenye mwili wako zinaharibika, muda wa kulala ndiyo mwili unajitengeneza, kama ni moyo ulikuwa na hitilafu itajikarabati wenyewe," alisema na kuongeza kuwa kama mtu hapati muda wa kulala, ni rahisi kupata msongo wa mawazo. Kwa mujibu wa Dk. Ndonde, magonjwa ya moja kwa moja ambayo mtu anapata kwa kutolala vizuri, ni magonjwa ya moyo na mishipa ya damu.

Alisema, takwimu za dunia zilizotolewa mwaka jana, magonjwa ya moyo na mishipa ya damu kwa mwaka yanasababisha vifo milioni 18 duniani na moja ya sababu ni watu kutopata usingizi wa kutosha.

Takwimu za mwaka 2012 zilizofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Wizara ya Afya, nchini Tanzania, asilimia 33 ya vifo hutokana na magonjwa ya moyo na mishipa ya damu.

Kwa upande wa watoto, Dk. Ndonde alisema wasipopata usingizi wa kutosha, ukuaji wao unakuwa siyo mzuri. "Mwanamichezo asipopata usingizi wa kutosha hawezi kupona majeraha, watu wote wanaofanya kazi nguvu wanaotembea sana, wanaoendesha baiskeli, wasipopata usingizi wa kutosha, mwili hauponi majeraha, namna unavyotembea sana au kuendesha baiskeli mwili unapata majeraha.

"Ukienda kulala yale majeraha ndiyo yanajikarabati, ushauri wetu kwa ujumla watu watimize vitu vitatu kula mlo kamili,mazoezi siyo chini ya dakika 30 kwa siku na kulala sio chini ya saa saba na ni usiku," alishauri.

HABARI KITAIFA



Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Prof. Edward Hoseah (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa zamani wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (kushoto) na Mbunge wa zamani wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa, katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, kabla ya kuanza kusikilizwa kwa hukumu ya kesi yao waliyoifungua dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mkuu wa Jeshi la Magereza, wakipinga vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanyika magerezani. Hukumu hiyo iliahirishwa hadi Desemba 07 mwaka huu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanafunzi wadaiwa kuingilia mfumo, waghushi malipo ada

**Na Thobias Mwanakatwe, aliyekuwa** IRINGA

ZAIDI ya wanafunzi 260 wa Chuo Kikuu cha Iringa wanadaiwa kuingilia mfumo wa chuo, ujulikanao kama SAMIS na kufanikiwa kujiorodhesha majina, hivyo kuonekana kama wamelipa ada.

Kwa kufanya hivyo, wanafunzi hao wanaonekana hawadaiwi, hivyo kukikosesha chuo mamilioni ya shilingi. Pia wanadaiwa kughushi stakabadhi za malipo na mihuri ya benki ili kujiridhisha kuwa hawadaiwi ada.

Uchunguzi wa kina ambao umefanywa na gazeti hili na kuthibitishwa na uongozi wa chuo, umebaini wanafunzi waliofanya hujuma hiyo ni wanaosomea cheti na shahada (bachelor) hali ambayo imeleta taharuki kubwa chuoni hapo.

Ada wanayopaswa kulipa wanafunzi wanaosomea cheti (certificate) kwa mwaka ni Sh. 840,000 wakati wa shahada mwaka wa kwanza ada yao ni Sh.1,670,400, mwaka wa pili Sh.1,610,400 na mwaka wa tatu ada ni Sh.1,760,400.

Mfumo wa SAMIS unaodaiwa kuingiliwa na wanafunzi hao unatumika na chuo hicho katika masuala ya malipo ya ada, kuweka kumbukumbu za wanafunzi na masomo.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa, Prof. Ndelilio Urio, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili, alikiri tatizo hilo kujitokeza katika chuo hicho na kwamba uongozi ulichukua hatua kuunda tume ya watu wanne ambao wanaendelea kuchunguza.

Alisema uchunguzi wa awali uliofanywa ulibaini wanafunzi 262 ndio walihusika katika kuingilia mfumo huo ambao baada ya kufanikiwa na ukaonyesha wamelipa ada, waliruhusiwa kufanya mitihani kabla chuo hakijashtukia hujuma hiyo. Prof. Urio alipoulizwa inakuwaje wanafunzi waingilie mfumo wakati hawana 'saver', alisema baadhi ya wanafunzi wanasomea masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hivyo kuna uwezekano wa kufanya hujuma hizo.

Alisema mbali na kuingilia mfumo, pia wanafunzi wamebainika walikuwa wakighushi stakabadhi za malipo ya benki na mihuri ambazo nazo zilikuwa zikipelekwa chuo ili kujiridhisha kwamba wamelipa ada wakati si kweli.

Kutokana na hujuma hiyo ambayo alisema ilikuwa ikifanyika hata miaka ya nyuma lakini haikuwahi kubainika, alisema wanafunzi waliobainika wamepewa muda hadi Novemba 11, mwaka huu, wawe wamelipa ada.

"Baada ya kuwabaini wanafunzi waliofanya hujuma hiyo huku wakiwa tayari walishafanya mitihani, tumezuia matokeo yao hadi watakapolipa ada," alisema.

Alisema Novemba 22, mwaka huu Baraza la Chuo litakutana katika kikao kujadili suala hilo na kuona hatua gani zichukuliwe kwa wanafunzi ambao watakuwa hawajalipa ada.

Hata hivyo, alisema baadhi ya wanafunzi wanaodaiwa wameshaanza kulipa ada na hivyo chuo kimewapa matokeo ya mtihani walioufanya.

Kuhusu madai ya kwamba wanafunzi waliobainika kuingilia mfumo huo wananyanyaswa na askari wanaosoma chuoni hapo kwa kupigwa na kupelekwa polisi, alisema madai hayo si ya kweli bali yanaenezwa na watu wasiokitakia mema chuo hicho.

Prof. Urio alisema kuna askari na wanajeshi wanaosoma katika chuo hicho lakini kamwe chuo hakijawashirikisha katika sakata hilo. Katika kukabiliana na tatizo lisijitokeze tena, alisema chuo kimeanza kuchukua hatua kwa kuwasiliana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kwa ajili ya kutengeneza mfumo mpya ambao utaunganisha chuo na benki moja kwa moja.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iringa, Hans Mejooli, alisema hujuma hizo zilibainika Agosti, mwaka huu, na baada ya hapo iliundwa timu ya kuchunguza zaidi suala hilo.

Alisema wanafunzi wanaodaiwa kuhusika na kuingilia mfumo huo wanasomea cheti na shahada ya kwanza na kwamba licha ya kufanya hujuma hizo, bado wako chuoni huku uchunguzi ukiendelea.

Kama wazazi wa wanafunzi hao wamejulishwa suala hilo, alisema baadhi walijulishwa na kwamba wahusika ni wanafunzi wenyewe kwa kuwa walipewa pesa na wazazi wao.

Baadhi ya wazazi wa wanafunzi ambao wamehusika katika hujuma hiyo, wakizungumza na gazeti hili, walilalamika watoto wao kunyanyaswa kwa kuzuilia matokeo kwamba hawajalipa ada.

"Kama kuna hujuma ya kuingilia mfumo wa chuo mbona sisi kama wazazi hatujajulishwa suala hili na inakuwaje wanafunzi waingilie mfumo huu wakati 'saver' wanayo walimu? Hapa kuna jambo linajificha nyuma ya pazia," alisema mzazi mmoja ambaye aliomba jina lake lisitajwe.

Mzazi mwingine alihoji kama kuna hujuma kama hizo ni kwa nini uongozi wa chuo haujalifikisha suala hilo Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili kufanyiwa uchunguzi na kama mfumo huu una upungufu ufanyiwe maboresho ili kuondoa hujuma zaidi zisijitokeze.

# Mbunge acharuka bil. 64/- kutafunwa ndani ya siku 1

**Na Richard Makore,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Judith Kapinga, ameliibua bungeni sakata la kutafunwa Sh. bilioni 64.3 kwenye Bandari ya Tanga baada ya kutolewa kwa zabuni iliyogubikwa na utata, akitaka hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika ili kuongeza uwajibikaji.

Judith aliibua hoja hiyo jana alipochangia taarifa ya utendaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyochambua ripoti ya ukaguzi wa mashirika ya umma uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake ya mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu.

Akichangia taarifa hiyo ya PAC kwa kipindi kinachoishia Februari mwaka huu, Judith alisema ufisadi katika bandari hiyo ulitokana na mkataba wa mwaka mmoja ambao Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) iliingia na Kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) wa Sh. bilioni 172.36.

Alisema mkataba huo uliingiwa Agosti 3, 2019 na ulipaswa kuisha Agosti 2020, ambapo ulilenga kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga, kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kununua vifaa kwa ajili ya shughuli za bandari.

Alisema kwa mujibu wa mkataba huo, gharama ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga ilikuwa ni Sh. bilioni 104.92, sawa na asilimia 60 ya mkataba wote.

Judith alisema kuwa Agosti Mosi, 2019, Kampuni ya CHEC iliuza kazi hiyo kwa mkandarasi mbia, ikiwa ni siku mbili kabla ya kampuni hiyo ya China haijatia saini mkataba na TPA.

Alisema kuwa baada ya kampuni hiyo kutoa kazi siku moja kabla ya kutia saini mkataba na TPA, siku mbili baadaye, yaani Agosti 3, 2019, ilitia saini rasmi mkataba na TPA wa kufanya kazi hiyo kwa Sh. bilioni 104.92, ilhali tayari CHEC ilishatoa kazi hiyo kwa mkandarasi mbia kwa Sh. bilioni 40.

"Kampuni ya CHEC, yaani China Harbour Engineering Company ilipewa kazi hiyo kwa Sh. bilioni 104.92, haikufanya kazi hiyo ila iligawa kwa bei rahisi kwa mkandarasi mbia, kwa mkataba wa dola za marekani milioni 18.15 sawa na Sh. bilioni 40.46 kwa kipindi cha miezi 11 bila kutoa taarifa kwa TPA.

"Pia mkandarasi mkuu, Kampuni ya CHEC, yaani China Harbour Engineering Company iliingia mkataba na 'mkandarasi mbia' hata kabla ya kutia saini mkataba wake na TPA kwa kuwa walitia saini Agosti Mosi, 2019 kabla ya Mkataba wa Mkandarasi Mkuu na TPA Agosti 3, 2019," alisema.

Mbunge huyo alisema kuingia mkataba bila kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Bandari ilikuwa ni kinyume cha kifungu kidogo cha 4.4 cha masharti ya jumla ya mkataba kati ya Mamlaka ya Bandari na mkandarasi mkuu ambacho kinazuia mkandarasi mkuu kutoa sehemu ya kazi kwa mkandarasi mwingine.

Alisema kwa mujibu wa kifungu hicho, ikiwa kuna uhitaji wa kutoa kazi kwa kampuni nyingine kutekeleza kazi zilizoko kwenye mkataba, mkandarasi mkuu anapaswa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Bandari siku 28 kabla ya kutoa kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Judith, CAG alibaini jumla ya malipo yaliyolipwa kwa kazi ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli yalikuwa dola za Marekeni milioni 18.22 sawa na Sh. bilioni 40.62.

Alisema kiasi hicho pia kinajumuisha malipo ya dola za Marekani 73,824 sawa na Sh. milioni 164.55 kwa huduma za wakala wa meli kwa mkandarasi mbia.

Alisema ulinganifu wa kiasi kilichotozwa na mkandarasi mkuu cha Sh. bilioni 104.92 na kiasi alicholipwa na mkandarasi mbia cha Sh. bilioni 40.62 inaonyesha kiasi kilichotozwa na mkandarasi mkuu kimezidi kiasi halisi kilichotumika kufanya malipo ya kazi hiyo kwa Sh. bilioni 64.3. Alisema kutokana na hali hiyo, mkandarasi huyo alijipatia Sh. bilioni 64 bila kufanya kazi yoyote, fedha ambazo zingetosha kujenda vyumba vya madarasa 3,200 nchini kwa gharama ya Sh. milioni 20 kwa chumba cha darasa. "Inawezekanaje mkandarasi kuchota kiasi kikubwa cha fedha na kukiweka mfukoni bila kufanya kazi wakati viongozi wa serikali wapo na hawachukui hatua?

"Mawaziri wapo, makatibu wakuu wa wizara wapo, viongozi wa bandari wapo, lakini wote hawa hawachukui hatua yoyote ili kuokoa fedha zetu ilhali mkandarasi anacheza na akili za Watanzania bila woga," Judith alisema.

RIPOTI MAALUM

# Mtihani wananchi waliosababisha maji ya bahari kuyavamia makazi

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa**
MTWARA

MIKINDANI ni mji wa kihistoria katika pwani ya Bahari ya Hindi kusini mwa Tanzania. Upo karibu na Mji wa Mtwara na umeunganishwa kiutawala katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara.

Mahali ulipo kutoka mjini Mtwara ni umbali wa Km 10.2 kuufikia na kulishuhudia eneo lake ambalo karne ya 16 lilikuwa mwanzo wa biashara ya misafara ya watumwa na pembe za ndovu.

Kwa mujibu wa wenyeji, jina Mikindani lilitokana na neno 'minazi mikinda' likiwa na maana jina la miti michanga aina ya mnazi.

Historia inabainisha kuwa Machi 1866, David Livingston alifika Mikindani. Mwonekano wa eneo hilo kwa miaka mingi ulikuwa kivutio, likipambwa na misitu ya mikoko na minazi katika eneo lote la bahari na nyumba zinazoashiria mji wa kihistoria.

Hata hivyo, kinachoshuhudia sasa ni hali tofauti, eneo hilo limezungukwa na maji ya bahari huku msitu na mikoko iliyoonekana miaka 10 iliyopita sasa haipo.

Kinachoshuhudiwa na Nipashe kwenye Mtaa wa Kisungule A, ni nyumba zikiwa zimepakana na maji ya bahari, uzio wa taka na viroba vya michanga umejengwa ili kukinga maji ya bahari yasibomoe ukuta wa nyumba.

Mosa Ahma, mkazi wa eneo hilo, anasema wamekuwa wakikusanya taka zinazotolewa baharini na maji, yakiwamo magogo, na kuzitumia kama uzio na kinga dhidi ya maji ya bahari kubomoa nyumba zao.

"Maji ya bahari yanapojaa, yanafika hadi ndani. Ili kuyazuia tunaweka hizi taka, tunachukua na viroba tunavijaza mchanga na kutengeneza uzio huu unaouona hapa ili maji yasiendelee kuingia ndani," anafafanua.

Mosa, anasimulia zaidi kwamba aliolewa katika familia iliyojenga nyumba hiyo enzi za ukoloni kwa kutumia mawe ya baharini, maarufu matumbawe.

"Nimeikuta hii nyumba, hatuwezi kuhama, tutakwenda wapi na familia yote ya mume wangu kuanzia babu na baba ilianzia hapa? Inabidi tuendelee kuziba haya maji," anasema Mosa na kubainisha kuwa ukarabati wa uzio huo unafanyika kila baada ya wiki mbili, wakitumia taka na mchanga wa baharini.

Aisha Rajabu, mkazi mwingine wa eneo hilo, anasema wenye uwezo kifedha, hutumia mawe makubwa kuzua maji hayo.

"Wanawake tunafanya kazi hii ya kuweka uzio wa taka na viroba vya mchanga, maeneo mengine tunazungusha na makuti ili kuzuia haya maji yasije huku," anasema Aisha.

Eneo lingine lililoathiriwa na maji ya bahari ni Msikiti wa Rehman ambao ulijengwa enzi za ukoloni kwa kutumia udongo.

Msham Abdallah, mmoja wa waumini katika msikiti huo, anasema ulikuwa mbali na bahari lakini sasa umefikiwa na maji ya bahari.

"Awali jengo hili la ibada lilikuwa limejengwa kwa udongo, sasa jengo limezungushiwa saruji na mawe kuzuia maji yasilete madhara. Maji yamekuwa yakipiga umbali wa futi sita kupanda ukuta wa msikiti. Ili kudhibiti madhara, tunalazimika kuwa na mchango wa kila mara kwa ajili ya ukarabati.

"Hatuwezi kujua ni kiasi gani kinatumika kukarabati maana utaratibu uliopo ni kila muumini anatakiwa kuwasilisha sadaka yake kwa ajili ya kurekebisha pale inapoonekana kuna madhara yanataka kutokea.

"Kama unavyoona hapa tayari kuna ufa umeanza kutokea kutokana na maji ya bahari kupiga eneo hili, inabidi ukarabati ufanyike," Abdallah analalama.

Ali Mwakanjila, anawasilisha ushuhuda wake kwamba alizaliwa miaka 1970 na amekua akishuhudia eneo hilo likiwa na msitu wa mikoko na minazi lakini sasa miti hiyo haipo na kusababisha maji kusogea kwenye makazi yao.

Mwakanjila anabainisha kilichowaponza ni kitendo cha wakazi wa eneo hilo na majirani zao kuitumia mikoko kuchoma mawe ya bahari (matumbawe) ili kupata chokaa ya kujengea nyumba zao.

Anaeleza kuwa kupwa na kujaa kwa bahari kunafanyika siku zote lakini kuanzia mwaka 2018, kasi ya maji kuingia kwenye makazi yao iliongezeka.

"Kwa hali inayoendelea hapa lazima tuhame kwa sababu hatuwezi kushindana na maji, yamekuwa mengi sana," anasema Mwakanjila.

Hussen Namchinga (65), mkazi wa eneo hilo, anasema: "Awali mikoko ilikuwa imezunguka eneo lote hili la bahari, bahari ilikuwa inaonekana ndani ya msitu kwa mbali lakini sasa mikoko inahesabika, minazi ni ya kutafuta, bahari imetawala hadi maeneo ya makazi yetu.

"Kama unavyoona maji yanatufuata kwenye nyumbani zetu, maji yameongezeka, ile miti iliyokuwa inayazuia, kwa sababu ilikatwa na watu ambao hawakuwa wanajua umuhimu wake, kizazi hiki ndicho kinaishi madhara yake. Watu waliona fahari kujenga kwa kutumia chokaa lakini sasa tunayaishi madhara yake."

### UCHIMBAJI MCHANGA

Mbali na ukataji wa mikoko, shughuli za uchimbaji wa mchanga katika eneo hilo la bahari, pia unatajwa kuwa chanzo kingine cha maji kujaa na kuingia kwenye nyumba za wananchi.

Mosa anasema vijana wamekuwa wakichimba mchanga na kuuza kwa wanaojenga na kwamba jitihada zao kuwazuia hazijazaa matunda.

"Ukiwakataza wanasema 'mchanga huu ni mali ya Mungu na ukifika unakuzika, unanikatazaje nisichimbe?' Kwa hiyo mimi ninaona haya kweli, kwanini nimkataze," anasema Mosa.

Mariam Nahimbe, mkazi mwingine wa Mikindani, anasema biashara ya mchanga inawapatia vijana kipato lakini madhara yanawapata wakazi wa eneo hilo ambao maji yamewafuata.

Anataja hatua walizochukua ni pamoja na kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kisungule A, ambaye amefika eneo hilo mara kadhaa na kuwaona vijana hao lakini hawajashuhudia hatua inayochukuliwa dhidi yao.

### UONGOZI MTAANI

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kisungule A, Debwe Cherehani anakiri wakazi wa eneo hilo kuishi hatarini kutokana na kuzingirwa na maji ya bahari.

Anasema, kwa sasa shughuli za ukataji wa mikoko katika eneo hilo hazipo lakini uharibu uliopo hauwezi kudhibitiwa na miti michache iliyobaki.

Debwe pia anaitupia lawama tabia ya ujenzi holela wa nyumba kwenye eneo la bahari na kwenye mitaro, hali inayosababisha kuendelea kupata madhara zaidi.

Anabainiha kuwa mtaa wake una nyumba 250 na kati yake, 90 (sawa na asilimia 30) zimeathiriwa na maji ya bahari, akibainisha kuwa na taarifa za nyumba zinazokumbwa na mmomonyoko kutokana na maji yanayozizunguka.

Anasema kwa kushirikiana na viongozi wenzake wamewafuata na kuwaonya vijana kuchimba mchanga lakini wamekuwa wakiwapa kauli zinazowapa hofu.

"Unawakataza wanakuambia 'mchanga huu unakataza lakini kesho utazikwa nao', ni kauli zinazotupa unyonge na kupunguza kasi ya kuwakataza," anasema.

Kiongozi huyo wa mtaa anasema wanaendelea na jitihada za kuzuia uchimbaji mchanga kwenye eneo hilo kwa kushirikiana na diwani wao, pia kutoa taarifa kwa uongozi wa halmashauri.

Diwani wa Kisungule, Issah Napunda, anasema ukataji mikoko kwa miaka ya karibuni wameukomesha na kilichobaki kuwa mtihani kwao ni madhara yanayotokana na kukosekana kwa miti hiyo.

"Maji yamekosa kingo za kuzuia kuingia kwenye makazi na hivyo kusababisha madhara yanayoonekana ikiwamo nyumba kubomoka.

"Katika kupambana na uharibifu huu katika eneo la bahari, tumefanikiwa kwa asilimia 50 na jitihada nyingine zinaendelea za kuhakikisha eneo la bahari linakuwa salama," anasema.

Anataja mikakati yao kukabiliana na athari hizo inajumuisha kurejesha maeneo ya bahari katika mazingira yake ya asili na moja ya eneo litakalofikiwa na mradi huo ni Kisungule.

Anasema wananchi wa Kisungule wanachimba anachokiita 'udala' (aina ya minyoo ya kulisha samaki) kama chambo ya kuvulia na kusababisha uharibifu na mmomonyoko wa udongo kwa asilimia 70 hadi 80.

Diwani huyo anataja hatua zilizokwishachukuliwa ni kufanya mikutano ya hadhara na kuwapa elimu ili kuachana na utaratibu huo kwa kuwa ni hatari kwa ustawi wa mazingira.

"Ugumu unakuja kwa sababu wanatumia kuvulia samaki ambao ni zao la biashara lakini bado tunaendelea kuhakikisha tunamaliza tatizo hilo kwa kushirikiana na viongozi wengine," anasema.



Msham Abdallah, ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Kisungule A, eneo la Mikindani mkoani Mtwara, akionyesha namna maji ya bahari yanavyoathiri jengo la Msikiti wa Rehman, kutokana na kukatwa kwa miti ya mikoko iliyokuwa ikiyazuia, ambapo waumini wa msikiti huo, wanalazimika kuchangishana fedha kwa ajili ya kukarabati uzio mara kwa mara. **PICHA: MARY GEOFREY**

# RC akemea vitendo vya ushirikina

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, amekemea vitendo vya kishirikina katika kata ya Kala wilayani Nkasi na kuwataka wananchi kuacha kuamini mambo hayo pamoja na kuwaalika waganga wa kienyeji, maarufu kama Lambalamba kufika katika kata hiyo ili kuwabaini wachawi.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji cha King'ombe, Sendiga alisema kata hiyo inaongoza mkoani hapa kwa kuwaita waganga ili wawaondoe wachawi huku akiweka wazi kwamba waganga wamekuwa wakiishia kuwatapeli wananchi na kuwachonganisha.

Sendiga alisema, imefikia hatua baadhi ya wananchi waliohamia mkoani Rukwa wameanza kukimbia kwa madai kuwa wanawaogopa lambalamba kwa kuwa wana tabia ya kusingizia kuwa mtu ni mchawi na hasa wakimwona ana uchumi mzuri ili wampige faini.

"Mnaharibu sifa nzuri ya mkoa wetu. Watu wanakimbia nyumba zao kwa kuogopa lambalamba kufika kusaka wachawi. Watu hao ni matapeli na wachonganishi. Nawataka muache kuwaalika na mnaofanya hivyo. Serikali haitawaacha salama ni lazima itawachukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliiagiza Jeshi la Polisi kuendesha msako na kuchukua hatua kwa kuwafikisha mahakamani watu wanaoendeleza vitendo vya kusaka wachawi kwenye makazi ya watu. Alisema watu hao wamekuwa chanzo cha kuvuruga amani na kuwasababishia wananchi umaskini.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, alimwahidi mkuu wa mkoa kuwa ataongoza operesheni maalum ya kuwasaka watu wanaofanya utapeli kwa kigezo cha kusaka wachawi kwenye makazi ya watu na kukusanya fedha na mifugo kwa wananchi.

Hivi karibuni katika wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, walimu watatu akiwamo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Zyangoma, walikimbia kituo cha kazi baada ya kutishiwa usalama kwa madai kuwa wamekataa lambalamba kuingia kwenye nyumba zao kwa lengo la kuzisafisha ili kuondoa uchawi.



Mbunge wa Chemba, Mohamed Moni, akichangia hoja Bungeni kwenye kikao cha nne cha mkutano wa tisa wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ashauri mikataba minene kupelekwa bungeni

**Na Richard Makore,** DODOMA

MBUNGE wa Masasi, Geoffrey Mwambe, ameshauri serikali kupeleka bungeni mikataba yote ya miradi mbalimbali inayoingia ambayo inazidi Sh. bilioni tano ili ijadiliwe kwa kuwa taifa linapata hasara inapovunjika kutokana na kulipwa fedha nyingi.

Mwambe alisema hayo juzi bungeni jijini hapo alipokuwa akichangia hoja kwenye ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilizowasilishwa juzi bungeni na Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa ( LAAC), Serikali (PAC) na Mitaji na Uwekezaji (PIC).

Alisema serikali inashindwa kesi nyingi katika mikataba iliyowahi kuingia katika miradi mbalimbali isipokuwa ilishinda mmoja pekee miaka ya nyuma wa City Water.

"Hii mikataba waheshimiwa wabunge inaliangamiza taifa letu. Umefika wakati sasa iwe inaletwa bungeni na kujadiliwa ili wabunge nao watoe mawazo yao kwa niaba ya wananchi," alisema Mwambe.

Alipendekeza mikataba mipya yote kupelekwa bungeni ikiwamo na ile ya zamani ili kuangaliwa kama imezingatia maslahi ya taifa.

Mwambe pia alisema suala la mikataba linalisumbua taifa huku akitolea mfano ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, mkataba wake umesogezwa kinyemela kwa miaka miwili.

Alisema kusogezwa kwa mkataba huo ni hasara kwa taifa maana yake, uzalishaji wa umeme ungeanza mapema serikali na wananchi wake wangefaidika.

Kwa mujibu wa Mwambe, mkataba wa ujenzi huo unatamka kwamba mwaka 2021, mkandarasi alitakiwa kuanza kuingiza maji kwenye bwawa hilo, lakini mpaka sasa suala hilo halifajafanyika.

Aidha, mbunge huyo alipendekeza mfumo wa ukusanyaji wa kodi ufumuliwe ili kupanua wigo wa kuongeza mapato ya serikali.

Sambamba na hilo, alipendekeza kuwa waongezwe wataalamu waliobobea katika kukadiria kodi ili kuondoa migogoro ya kikodi inayosababisha serikali kushtakiwa.

Pia aliomba serikali kuwalipa wafanyabiashara fedha wanazowakusanyia kupitia VAT na kwamba kama itachelewesha fedha hizo basi ijitoze yenyewe faini.

Kuhusu mikataba kwenye sekta ya madini, Mwambe alisema huko ndiyo kichaka na kwamba mingi ni mibovu na inatakiwa kuangaliwa.

Akichangia katika ripoti hiyo, Mwambe alisema kuna haja sasa kulifumua Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kuruhusu kampuni binafsi kuzalisha na kuuza umeme kwa wateja watakaowataka wao.

Alisema umefika wakati kupunguziwa majukumu ili iweze kufanyakazi zake kwa ufanisi tofauti na ilivyo kwa sasa.

Kuhusu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) alisema kwa kuwa imeshindwa kuleta tija kuna haja ya kuibadilisha na kuunda mfuko wa elimu.

Alisema mfuko wa elimu utakuwa na jukumu la kusomesha watoto wote wa kitanzania bila ubaguzi na wala kujali kipato cha familia anayotoka.

Waziri wa Ujenzi wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alitoa taarifa ya serikali kuwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), unamilikiwa na serikali kwa asilimia 100.

Profesa Mbarawa awali uwanja huo ulikuwa unamilikiwa kwa ubia katika ya serikali na kampuni binafsi nne. Alisema serikali ilinunua hisa zote za kampuni hizo na hivyo kwa sasa serikali inaumiliki kwa asilimia 100 na hivyo wananchi waondoe hofu.

Awali, baadhi ya wabunge walihoji ni nani anayemiliki uwanja huo, kwa kuwa CAG amefanya ukaguzi na kutoa maoni yake.

# SUMA JKT yatoa msaada wanafunzi viatu jozi 500

**Na Romana Mallya**

KIWANDA cha Viatu na Bidhaa za Ngozi kinachomilikiwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), kimekabidhi viatu jozi 500 kwa Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao, kwa ajili ya kuwagawia bure wanafunzi wa shule za msingi mikoa ya kusini.

Taasisi hiyo inatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya 'Samia Nivishe Viatu' ambapo mpaka sasa wanafunzi wa Kibiti, mkoani Pwani pamoja na wa Mkoa wa Tabora wameshavishwa viatu. Makabidhiano hayo yalifanyika jana mkoani Dar es Salaam yakihusisha Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kiwanda hicho, Meja Mathias John, aliyeyabidhi jozi 500 kwa Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Steven Mengele, maarufu kama Steve Nyerere.

Alisema taasisi hiyo inakwenda kuwavisha viatu wanafunzi wa shule za msingi wa mikoa ya Lindi na Mtwara.

Meja John alisema wameona jitihada za taasisi hiyo wanazozifanya za kuwavisha viatu wanafunzi waliopo vijijini na SUMA JKT imeamua iwape tabasamu watoto kwa kutoa viatu wanavyozalisha vyenye ubora.

"SUMA JKT tumeona ni vyema tushirikiane na wadau tupeleke viatu kwa watoto wetu waliopo vijijini, tunaunga mkono kampeni ya 'Samia Nivishe Viatu',viatu vyetu vinatengenezwa na malighafi inayopatikana Tanzania, wale watoto ambao hawajawahi kuvaa viatu, watavalishwa kupitia kampeni hii," alisema.

Nyerere alisema SUMA JKT ni moja kati ya familia za Watanzania ndiyo maana bidhaa zao zinakidhi mahitaji ya kitanzania.

"Wakati tunatembea vijijini unakuta mtoto wa darasa la kwanza mpaka la saba hajavaa kiatu, ana sare lakini kiatu hana mpaka miguu imeachia, ukija mjini mtoto akienda shule akirudi likizo anarudi na kiatu kipya, na alichokiacha nyumbani siyo kwamba ataendelea kukitumia, kitabaki mpaka kinaoza," alisema.

Alisema wamejipanga kila mkoa kupeleka viatu kwenye vijiji sita lengo ni kupata wasomi wa baadae.

"Mazingira yamekuwa magumu kupata matajiri wapya, wasomi wapya, mtoto anatoka nyumbani hana viatu anatembea kilometa sita, wanachomwa na miiba, akifika darasani anakuwa na msongo wa mawazo ya maumivu ya kuchomwa, anawaza atarudije nyumbani.

"Tunaishukuru SUMA JKT na Rais Samia Suluhu Hassan tunaahidi kiatu cha mama Samia kitafika kila kona ya nchi huko kijijini na tutawavalisha wenyewe viatu, kama kuna wengine wanataka kubeba, SUMAJKT imefungua milango," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga bado ina nafasi kutinga makundi CAF

**KAMA** ambavyo Rais wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Saidi, alivyosema kuwa pamoja na timu yao kukosa ushindi dhidi ya Club African katika mchezo wa kwanza kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF, lakini bado hawajakata tamaa.

Hersi amesema, wachezaji pamoja na benchi la ufundi walitumia kila mbinu ndani ya uwanja, lakini ilishindikana na kwamba bado wana matumaini ya kufanya vizuri katika mechi ya marudiano.

Amesema, ameona maoni mengi ya mashabiki wao wakitupia lawama kwa benchi la ufundi, wachezaji na hata viongozi, na kudai hiyo ni kuwavunja nguvu wachezaji.

Wachezaji na benchi la ufundi walipambana na anaamini haikuwa bahati kwao, lakini wana nafasi ya kurekebisha makosa yao ndani ya dakika 90 nyingine za kujiuliza watakapokuwa ugenini.

Amesema kinachofanyika hivi sasa ni kuiandaa timu kwa ajili ya mchezo wa marudiano ili kutimiza lengo la kucheza hatua ya makundi ingawa amekiri kuwa mchezo utakuwa mgumu.

Kauli hiyo ya Hersi Nipashe tunaiunga mkono kwa asilimia 100 kwa sababu, tunaamini Yanga ikicheza kwa mbinu, kujituma na bidii ina nafasi kubwa ya kuiondoa Club Africain nyumbani kwao kwenye mchezo wa marudiano nchini Tunisia Novemba 9 mwaka huu. Tunasema hivyo kwa sababu soka ni mchezo wa makosa na unapofanya kosa moja unaadhibiwa, hivyo Yanga wanaweza kutumia nafasi ya kucheza ugenini kuweza kupata ushindi wanaouhitaji. Baada ya kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo inamaanisha kwamba, sare yoyote ya mabao itaishuhudia Yanga ikifuzu kwenye hatua ya makundi.

Mchezo wa hapa nyumbani haukuwa na mabao yoyote yaliyofungwa, hivyo kama watatoka tena suluhu kule Tunisia, maana yake mshindi ataamuliwa kwa mikwaju ya penalti kama hatapatikana mshindi ndani ya dakika za kawaida na zile za nyongeza.

Hivyo, Yanga kwa namna moja au nyingine matokeo yoyote ya sare ya mabao itawafanya wao watinge moja kwa moja hatua hiyo ya makundi. Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba, ukiangalia namna mchezo ulivyochezwa hapa nyumbani, ni wazi kabisa klabu ya Club Africain inafungika, kwani Yanga ilitawala mchezo kwa asilimia 63 dhidi ya wapinzani wao hao.

Kama Yanga itacheza kwa kufunguka na klabu Club Africain ikafunguka, kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana mabao mengi kwenye mchezo huo wa marudiano.

Katika mchezo wa kwanza, Club Africain ilicheza kwa kujihami sana na kulinda lango lao, huku wachezaji zaidi ya 9 wakiwa nyuma kuhakikisha hakuna madhara yanayotokea kwenye goli lao.

Kwa sababu watakuwa wakicheza nyumbani kwenye mchezo huo wa marudiano, kwa namna yoyote lazima Club Africain itataka kufunguka ili kwenda mbele kutafuta mabao

Na hapo ndipo Yanga watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kulishambulia lango la wapinzani wao na kutengeneza nafasi ya kufunga mabao.

Imani yetu ni kubwa kwamba, Yanga inaweza kuvuka katika hatua hiyo, kwani ubora wa wachezaji wake ni mkubwa na walionesha kwenye mchezo wa kwanza kwamba nia na malengo wanayo.

Hivyo wakitumia mbinu za benchi la ufundi pamoja na namna walivyousoma mchezo wa kwanza, tunaamini kabisa wanaweza kufanya lolote ili kupata ushindi ugenini na hatimaye kusonga mbele kwenye hatua ya makundi.

Nipashe tukiwa wadau wakubwa wa soka na pia kwa sababu Yanga inawakilisha taifa kwenye mashindano hayo, tunaitakia kila la heri kwenye mchezo huo wa marudiano na tuna imani wataweza kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Viongozi Yanga wasijibu kila wanalosema mashabiki

**BAADA** ya Yanga kushindwa kuifunga Club Africain ya Tunisia Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya mchujo wa Kombe la Shirikisho barani Afrika, baadhi ya wanachama na mashabiki wa klabu hiyo waliongea maneno makali sana.

Maneno hayo yalielekezwa kwa baadhi ya wachezaji wao, kocha pamoja na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo.

Baada ya suluhu hiyo ya nyumbani ni kama vile wanachama na mashabiki wa Yanga wamekata tamaa ya kwenda kushinda ugenini, hasa wakikumbuka kwenye mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Al Hilal ilikuwa kama hivyo, wakitoka sare ya bao 1-1 nchini na kwenda kuchapwa bao 1-0 nchini Sudan. Ikasemwa na baadhi ya viongozi kuwa wamejifunza kutokana na makosa, lakini hali ikajirudia vile vile licha ya kuaminishwa kuwa kila kitu kiko sawa.

Nadhani hili ndilo lililowafanya baadhi ya wanachama na mashabiki wapandwe na hasira ya kuongea maneno mengi makali dhidi viongozi wao. Hali hii imemfanya Rais wa Klabu hiyo Injinia Hersi Said kuibuka na kutengeneza kipindi cha kuongea na Wanayanga, akichukua fursa hiyo kujibu baadhi ya yale ambayo wanachama na Yanga walikuwa wakiyapigia kelele. Kwa kifupi yeye na viongozi wenzake wa chini, walisikika wakisema wameyasikia yote ambayo wanachama na mashabiki wameyasema, hivyo watayafanyia kazi.

Kwangu mimi binafsi naona kuwa hakikuwa na ulazima wowote wa Yanga kujitokeza na kujibu maneno ya hasira za mashabiki kwa sababu hakukuwa na jambo lolote baya ambalo limefanyika kwenye mechi ile. Yanga haikufungwa, ingawa haikupata matokeo kwenye mechi hiyo. Hili ni jambo la kawaida sana kwenye soka.

Hebu fikiria tayari viongozi wa Yanga wamejitokeza na kujibu maneno ya mashabiki, kama ikitokea bahati mbaya itatolewa itakuwaje? Ina maana mashabiki wakichachamaa watakuja tena na kuwaambia tena mashabiki wamesikia malalamiko yao na watayafanyia kazi?

Moja ya malalamiko ya mashabiki wa Yanga ni kutaka kocha Nasreddine Nabi atimuliwe, je hayo ndiyo moja ya mambo ambayo viongozi watayafanyia kazi?

Mimi nadhani Wanayanga waliongea siku ile kwa sababu ya hasira tu ya kushindwa kupata ushindi kwa hiyo sidhani kama waliongea kitu chochote cha kujenga, zaidi ya jazba tu.

Ni sawa tu na wanandoa ambao wanapogombana maneno ya hasira zao ni kuchana na kupeana talaka, lakini siku ya pili ukimuuliza yoyote kuhusu hilo hawezi kukujibu. Kila mmoja hataki kitu kama hicho kitokee.

Viongozi wa Yanga ambao wengi wao ni vijana wajue kuwa wanaongoza taasisi kubwa yenye watu wengi na wenye tabia mbalimbali kwa hiyo wanatakiwa kuwa na 'ngozi ngumu' kama za wanasiasa hivi na si kila kinachosemwa basi viongozi wanajitokeza haraka kukijibu. Mengine yanasema tu kwa ajili ya mihemko na baada ya siku mbili mawimbi yanatulia, maisha yanaendelea.

Hivi ndivyo walivyokuwa wanaishi viongozi wa klabu kubwa za Simba na Yanga wa zamani ambao wengi wao walikuwa wanachaguliwa wakiwa na umri mkubwa. Sababu yake ni kuweza kuhimili presha kama hizi.

Hili lililotokea kwa Yanga, viongozi wajue ni dogo sana na watakutana na makubwa zaidi ya haya kwa sababu timu haitoweza kushinda kila siku, lakini pia kuna mengine yanaweza kujitokeza hata walikotoka hakujulikani.

Kuna viongozi waliiongoza Yanga ikiwa na migogoro mkubwa, lakini bado waliweza kuhimili presha za wao wenyewe ndani kwa ndani, na hata nje kwa wapinzani wao. Hebu tuangalie mfano wa wenzao Simba, kabla ya ligi kulikuwa na presha kubwa kutoka kwa mashabiki juu ya kikosi chao kuwa ni kibovu, lakini walikaa kimya. Baadaye likaja suala ya Selemani Matola. Baada ya mechi dhidi ya KMC sare ya bao 2-2 mashabiki wakitaka Matola atimuliwe, hatukusikia kiongozi yoyote wa Simba aliyejibu chochote, badala yake timu ilikwenda nchini Malawi itashinda. Kila mashabiki wakisema Matola aondoke, husikii ufafanuzi wala kiongozi anayepata na kuongea kwenye vyombo vya habari. Hii inaonyesha kuwa wanaoongoza klabu hiyo tayari wana uzoefu kwenye soka na wanawafahamu vilivyo.

Rai yangu kwa viongozi wa Yanga mambo mengine wayaache yapite kama maji kwenye mkodo wake. Wakisema kila kitu ambacho mashabiki watalipuka nacho basi wajibu, watakuwa na kazi ngumu sana kwenye uongozi wao. Wajikite zaidi kwenye kuongoza klabu na si kuongozwa na maneno ya watu.

# Wanachama 15 wa Klabu za Biashara NMB wapaa Uturuki

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA wa Klabu za Biashara za Benki ya NMB (NMB Business Club) waliotembelea Maonesho ya Biashara Uturuki, wamerejea nchini, wakibainisha ziara hiyo imebadili mbinu, mifumo na falsafa zao kiutendaji na kuwapandisha kutoka daraja la uchuuzi na uuzaji, hivyo kuwa wazalishaji wa bidhaa.

Oktoba 17 mwaka huu, wafanyabiashara 15 wa klabu hizo waliondoka nchini kwenda Uturuki kwa ziara ya siku tisa kutembelea maonesho hayo ya Trade Fairs 2022, NMB ikigharamia ziara yao hiyo.

Wakizungumza baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) juzi, wafanyabiashara hao waliishukuru NMB kwa kuratibu ziara hiyo na kusema imewaongezea hamasa, mbinu na uhusiano wa kibiashara utakaoharakisha kukua kwao kibiashara na wamejifunza namna ya kuwa wazalishaji badala ya waagizaji bidhaa.

Msemaji Mkuu wa Wanachama hao, Salvatory Chobaliko ambaye ni Mkurugenzi wa Kigoma Pharmacy Ltd, alisema kupitia ziara hiyo, katika maonesho hayo makubwa na ile ya kwenye viwanda mbalimbali vya uzalishaji wa bidhaa wanazofungamana nazo, wamejua mbinu za kuharakisha ukuaji kibiashara na kiuchumi.

"Tunaishukuru sana NMB sio tu kwa kufanikisha ziara hii, sambamba na ziara za ndani kwenye viwanda vya nguo, vipodozi, vifaa vya ujenzi, viatu, dawa, usindikaji vyakula na matunda, bali pia kutuunganisha na wafanyabiashara wakubwa na kutubadili kutoka kuwa wachuuzi na waagizaji hadi kuwa wazalishaji," alisifu.

Chobaliko alitoa wito kwa wafanyabiashara wenzake kuwa mabalozi wema wa yote waliyojifunza katika ziara yao, huku akiwataka kuitumia kubadilika zaidi na kukuza mitaji na mapato yao na kuchangia uharaka wa ukuaji wa uchumi wa taifa, huku akiiomba NMB kuendelea kuunga mkono wafanyabiashara nchini.

Bahati Senga, mmoja wa waliotembelea maonyesho hayo akiwa Mkurugenzi wa Bahati Fashion Shop, alikiri kufurahishwa na ziara hiyo katika miji ya Istanbul, Sakarya na Bursa walikoshiriki mikutano na Wanachama wa Umoja wa Wafanyabiashara (Chamber of Commerce) za miji hiyo.

"Ilikuwa ni ziara iliyotuwezesha kujifunza mambo mengi, kupitia maonyesho, ziara kwenye viwanda na mikutano yetu na wafanyabiasahara wakubwa na wenye viwanda. Tumejifunza utengenezaji na uzalishaji wa bidhaa na tunakuja kuvitumia kubadili bishara zetu na kufungua fursa za ajira kwa Watanzania," alisema Senga. Meneja Mwandamizi wa Idara ya Biashara NMB, Theresia Mayanie ambaye alikuwa mmoja wa viongozi wa benki hiyo waliofuatana na wafanyabiashara hao, alibainisha malengo ya ziara yao yamefanikiwa na wanaamini italeta mabadiliko makubwa kwenye biashara za wateja wao hao na kueleza utayari wa benki kuwasaidia.

"Madhumuni ya ziara hii yalikuwa kutembelea maonyesho hayo, lakini pia ziara za ndani viwandani na kwenye masoko makubwa. Imekuwa ya mafanikio kwa sababu imewawezesha kushiriki mikutano mikubwa na Chemba za Wafanyabiashara, mikutano ya Biashara kwa Biashara (B2B) na kupanua mtandao wa biashara zao. "Kundi hili la wafanyabiashara lilipata nafasi ya kutembelea viwanda vyao na kujifunza namna ya kuzalisha, kuuza na kupata ujuzi ambao utawasaidia kuongeza tija katika biashara zao sasa, kwani waliingia makubaliano mbalimbali ya ubia, mambo ambayo tunaamini yanaenda kunyanyua mitaji na pato lao kwa ujumla," alisema Mayanie.

Hii ni mara ya pili kwa NMB kuratibu ziara ya aina hiyo, mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2019 ambako wafanyabiasahara 10 walitembelea na Maonyesho ya 125 ya Canton Fair 2019 yaliyofanyika mjini Guangzhou, China kabla ya janga la corona kukwamisha safari hizo miaka miwili ya 2020 na 2021.




Mshauri wa Sera na Uraghabishi wa shirika la WaterAid Tanzania, Christina Mhando akikabidhi vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa Ebola vyenye thamani ya shilingi milioni tano kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, jana. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# Tanzania yapigwa jeki mapambano ebola

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA la WaterAid Tanzania limetoa vifaa vya Sh milioni tano kwa ajili ya kusaidia mkoa wa Dar es Salaam kupambana na ugonjwa wa Ebola ambao umetajwa uko nchi jirani ya Uganda.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Mashauri wa Sera na Uraghabishi wa shirika hilo, Christina Mhando, alisema msaada huo utaenda kusaidia katika mapambano ya ugonjwa huo ambao kila mmoja anatakiwa kuchukua hatua.

Mhando alisema, waliwasiliana na Wizara ya Afya ili kuona ni namna gani wanaweza kuunga mkono juhudi za serikali ili kukabiliana na ebola, ugonjwa ambao uko nchi jirani.

"Wizara ya Afya walitupatia orodha ya vifaa kinga na kutuelekeza tuvilete ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao ni moja ya mikoa mitano iliyo hatarini na ugonjwa huu wa Ebola kutokana na mwingiliano wa watu," alisema.

Aidha, alisema Oktoba 31, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa rai kwa wadau kushirikiana na serikali kutoa vifaa kinga kwa wataalamu ili kujikinga na ugonjwa wa Ebola ambao unazidi kusambaza nchini Uganda.

Mhando alisema, ndege zinazotoka kampala kuja Dar es Salaam na mabasi inaiweka Tanzania katika hatari ya kupata mlipuko huu kutokana na mwingilio mkubwa wa kiuchumi na kijamii na Uganda.

Alisema Shirika la WaterAid lina lengo la kuhakikisha kuwa kila Mtanzania , maji safi na salama silaha binafsi na usafi wa mazingira anapata huduma hizo ifikapo mwaka 2030 na linakuwa ni jambo la kawaida kwa kila Mtanzania.

"Tunaamini haya yote yanawezekana kwa ushirikiano, kutekeleza kwa kuonyesha mfano na kutumia yale mazuri tuliyojifunza kujengea uwezo watendaji na kutumika katika kufanya maamuzi katika ngazi zote," alisema

Mganga Mkuu wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alishukuru kwa msaada waliopatiwa si mara ya kwanza wamekuwa wakipanga pamoja na kutekeleza afya za upatikanaji maji safi na salama na usafi wa mazingira.

Alisema, licha ya Tanzania kutokuwa na ugonjwa wa Ebola kuna umuhimu wa kuchukua mikakati madhubuti ya kuhakikisha hapatikani mgonjwa.

Dk Mfaume alisema jitihada zinazofanywa na wadau wa maendeleo kwa kuunga mkono jitihada za serikali na Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha Watanzania wanabaki salama.

Pia, alisema vifaa walivyopatiwa vitawasaidia sio tu kwenye vituo vya afya watapekeka maeneo mengine ikiwemo viwanja vya ndege wanapokea wageni wengi kutoka nchini Uganda na kituo cha stendi ya Magufuli.

"Hivi vifaa sio to kwa Ebola vifaa hivi vitasaidia kupambana na magonjwa mengine kama Uviko-19 na hata kipindupindu. Naomba niwasihi wananchi wa Dar es Salaam kuchemsha maji ya kunywa na kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka ili kujikinga na magonjwa haya ya hatari,"alisema.

## KABWELA

**Fadhili Mohamed**



# Waomba serikali kumaliza mgogoro barabara

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI wa kijiji cha Mikenge, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wameiomba serikali kumaliza mgogoro wa barabara uliopo kati yao na mwekezaji kampuni ya ASM (T) LTD.

Mgogoro huo wa muda mrefu umewazuia wananchi na wawekezaji wengine katika eneo la pwani ya bahari kushindwa kuitumia kufika kwenye shughuli zao. Mwenyekiti wa kijiji hicho, Lameck Mayala, alisema juzi kuwa mgogoro huo tayari umefikia hatua ya ASM kutakiwa kulipwa fidia ili kufungua barabara ambayo ameifunga kwa kujenga ukuta.

"Walikuja hapa watu wa kufanya tathimini, waliuangalia huu ukuta na kusema wanaenda kuandaa ripoti kuifikisha kwa Waziri tayari kwa uamuzi, lakini mpaka sasa kumekuwa kimya. Wananchi na wafanyabiashara wengine wanaendelea kuteseka kwa kukosa barabara ya kuwafikisha kwenye maeneo yao kazi," alisema Mayala.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Mwinyipingu Mbwana, alisema mgogoro huo umekuwa wa muda mrefu licha ya viongozi wa wilaya ya Kigamboni kuufahamu bado suluhisho lake limekuwa kitandawili.

"Kwa sasa sisi tunaiomba serikali itusaidie. Vijana wengi wamepoteza kazi baada ya wawekezaji wengine kufunga hoteli zao kutokana na kufungwa kwa barabara hii," alisema Mwinyipingu.

Aidha, mmoja wa wawekezaji waliokuwa wakiitumia barabara hiyo kufika katika maeneo yao, Arif Sheikh, alisema waliwekeza maeneo hayo kwa kujenga hoteli kubwa kwa kuchukua mikopo benki lakini kwa sasa wamelazimika kufunga kutokana na kukosekana kwa barabara ya kuwafikisha kwenye maeneo yao.

"Kama mwekezaji niliifuatilia kwa kina na kufika kwa Waziri wa Ardhi Angeline Mabula ambaye alikiri kuwa suala hilo lipo mikononi mwake.

"Mheshimiwa Waziri alinihakikishia kuja kulitolea ufumbuzi suala hili na aliniambia suala hilo liko mikononi mwake lakini mpaka sasa kimya kimetawala na huyu mwenzetu ASM ameamua kuifunga kabisa kwa kujenga ukuta huu mnaouona. Tunaomba serikali itusaidie kulimaliza suala hili ili na sisi tuendelee na biashara zetu, tulilazimika kuwaondoa kazini vijana wengi kwa sababu ya biashara kukwama," alisema Sheikh.

Akiuzungumzia mgogoro huo, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, Idrisa Kayela, alisema mgogoro huo ulishatatuliwa kwa kuitaka Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kumlipa fidia ASM ili kupisha barabara hiyo inayoelekea kwenye maeneo ya wawekezaji wengine na ufukwe wa Kasa.

"Tulikaa vikao zaidi ya sita kutafuta suluhu ya mgogoro huu, sheria ya utwaaji wa ardhi namba 47 inataka mwananchi kulipwa fidia pale ardhi yake inapochukuliwa kwa ajili ya kupisha mradi wowote. Tulikubaliana na agizo lilipelekwa kwa Halmashauri ya Kigamboni kumlipa fidia ASM ili barabara hiyo ifunguliwe na wawekezaji na wananchi wengine waendelee na shughuli zao," alisema Kayela.

Pia alisema baada ya kutuma wataalamu wa kufanya tathimini, ilipitishwa mwekezaji huyo kulipwa Sh. milioni 129 na kwa sasa halmashauri ya Kigamboni inalifanyia kazi ili kumlipa.

Mkurugenzi wa ASM ambaye analalamikiwa, Abdallah Mohamed, alipotafutwa kwa njia ya simu, alikataa kuelezea lolote juu ya mgogoro huo.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Erasto Kiwale, alisema hana taarifa ya uamuzi wa kulipwa fidia kwa mwekezaji huyo.

Waziri Mabula alipopigiwa simu kuhusu suala hilo, alisema hana jibu la moja kwa moja na kwamba atakuwa kwenye nafasi nzuri ya kulizungumzia akipata maoni ya kamishna wa ardhi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kigamboni. Hata hivyo, alikiri kulifahamu jambo hilo lakini majibu yake ni mpaka anatakapowasiliana.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto) akimkabidhi zawadi, Meya wa Jiji la Busan, Korea Kusini, Park Heong-Joon wakati wa ziara yake nchini humo juzi. **PICHA: WANMM**

## Waziri Mabula, Meya Korea Kusini wateta

**Mwandishi Wetu**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekutana na kufanya mazungumzo na Meya wa Jiji la Busan Metropolitan nchini Korea Kusini, Park Heong-Joon.

Katika mazungumzo yao yaliyofanyika juzi, Meya wa Jiji hilo ambalo ni la pili kwa ukubwa Korea Kusini baada ya Seoul, alionyesha nia ya kuendeleza uhusiano baina ya nchi yake na Tanzania yaliyodumu kwa takriban miaka 30 sasa.

Aidha, Park Heong- Joon alionyesha nia ya jiji lake kuwa na program za kubadilishana uzoefu kwenye nyanja za elimu sambamba na kuwa tayari kusaidia masuala ya miundombinu. Pia, alionyesha nia ya kuja Tanzania kutembelea mbuga za wanyama katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara, mapema mwakani.

Waziri Mabula, yuko katika ziara nchini Korea Kusini ambako mbali na mambo mengine anashiriki mijadala kwenye maonyesho ya maendeleo ya teknolojia ya taarifa za kijiografia - Smart Geospatial Expo 2022.

Mwanzoni mwa ziara yake, Waziri Mabula na mwenzake wa Ardhi, Miundombinu na Usafirishaji wa Korea Kusini, Won Hee-ryong, walitia saini makubaliano ya ushirikiano wa kuimarisha sekta ya ardhi kupitia hati ya makubaliano (MOU) ya ushirikiano kwenye sekta ya ardhi na menejimenti ya taarifa za kijiografia.

# CBE yaandaa kongamano uchumi, biashara

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeandaa kongamano la maendeleo ya biashara na uchumi ambalo linatarajiwa kufunguliwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi mkoani Dodoma.

Hayo yalisemwa jana chuoni hapo jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, wakati akizungumzia kongamano hilo litakalofanyika Novem,ba 15 na 16, mwaka huu kwenye ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma.

Alisema, kongamano hilo lina kaulimbiu ya 'Biashara Uwekezaji na Ubunifu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi; na kwamba kutokana na umuhimu wake, viongozi mbalimbali wa Tanzania Bara na Visiwani watashiriki.

Prof. Mjema alitaja mada zitakazojadiliwa kwenye kongamano hilo kuwa ni pamoja na biashara ya ndani na kimataifa, uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, ubunifu na ujasiriamali, uwezeshaji wa biashara na ushirikiano na kiuchumi, uwekezaji na teknolojia, uchumi wa bluu, zuia mnyororo na fedha za kidijitali Alisema lengo la mdahalo huo wa kitaaluma ni kujenga uwezo na mitandao miongoni mwa watafiti na wadau wengine barani Afrika na kutoa fursa ya maendeleo ya kiuchumi kupitia biashara na kwamba kongamano hilo litasaidia kuleta ufahamu mpya katika tasnia mbalimbali.

Pia alisema, kutakuwa na mahafali ya 57 ya CBE ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Novemba 12, mwaka huu, katika kampasi ya Dar es Salam ambapo kutakuwa na wahitimu wa Shahada ya Uzamili, Stashahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti cha Ufundi.

Alisema wiki ya makongamano kwa Kampasi zote shughuli zitaanza Jumatatu hadi Alhamisi ambayo itakuwa siku ya kilele na kwamba katika wiki hiyo shughuli mbalimbali kama vile mawasilisho ya machapisho, maonyesho ya idara za kitaaluma ambayo yatawahusisha wahitimu wa zamani wa CBE ambao wanakaribishwa kuonyesha bidhaa na huduma wanazozifanya.

"Pia semina na warsha kuhusu mambo mbalimbali ya biashara zitawezeshwa bila gharama yoyote na katika mahafali hayo ya 57 katika Kampasi zetu zote takribani Wahitimu 2,000 watatunukiwa stahiki zao katika ngazi tofauti tofauti," alisema Profesa Mjema.

HABARI KITAIFA

# Mahakama Afrika kuanza kusikiliza mashauri wanachama kutafuta haki

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyoko jijini Arusha, inarejea tena Novemba 7, mwaka huu, kusikiliza mashauri mbalimbali yaliyowasilishwa na mataifa ya Afrika kutafuta haki.

Kabla ya kuanza kwa mashauri hayo, Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Imani Aboud, atampokea Naibu Msajili mpya wa Mahakama hiyo, Grace Wakio Kakai, raia wa Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msajili wa Mahakama hiyo, Dk. Robert Eno, Msajili Kakai, anachukua nafasi hiyo baada ya Nouhou Diallo, raia wa Burkina Faso, kustaafu rasmi akiwa katika wadhifa huo.

Alisema kabla ya uteuzi huo, Kakai alikuwa Mkuu wa Divisheni ya Sheria ya Mahakama ya Afrika.

Aidha, taarifa ya msajili huyo imeeleza zaidi kuwa mahakama hiyo itatoa hukumu za mashauri yatakayosikilizwa, Desemba Mosi, mwaka huu.

Hivi karibuni, Jaji Aboud alisema licha ya nchi nyingi za Afrika kuridhia itifaki ya kuanzishwa kwake, bado zina kigugumizi cha kutoa tamko la kuwaruhusu wananchi na taasisi za kiraia, kupeleka mashauri yake moja kwa moja kwenye mahakama hiyo.

Kati ya nchi 55 za Umoja wa Afrika ni nchi 33 zilizoridhia itifaki ya kuanzishwa kwa mahakama hiyo. Kati ya nchi hizo ni nane pekee zilizotoa tamko la kuwaruhusu wananchi wake na taasisi za kiraia kupeleka mashauri yao moja kwa moja katika mahakama hiyo.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Jumuiya ya CCM, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Anna Shinini (katikati), akipita juu ya kanga zilizotandikwa na wanachama wa umoja huo, alipowasili katika kikao cha Baraza la UWT la wilaya hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC awatwisha zigo DED, DC ujenzi shule

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongela, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Zainabu Makwinya, kuandaa mpango mahususi wa uboreshaji madarasa ya zamani ambayo ni chakavu na yanatishia usalama wa wanafunzi na walimu.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kukakugua miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashauri hiyo, ikiwamo vyumba vya madarasa, miradi ya afya na maji. "Pamoja na ujenzi wa madarasa unaoendelea na madarasa ya UVIKO-19, ni vyema mkaja sasa na maboresho katika madarasa ya zamani ili kuwa na muonekano mzuri.

"Ajenda kubwa ya Mheshimiwa Rais Samia Hassan Suluhu, ni kuondoa kero kwa wananchi pamoja na kuboresha maisha ya Watanzania," alisema.

Mnakumbuka mwaka 2021 Rais alitoa madarasa ya UVIKO-19 ambapo Mkoa wa Arusha tulipata takribani Sh. bilioni 10 na mwaka huu wa 2022, tumepata Sh. bilioni 5.7. "Katika wilaya zote za Mkoa wa Arusha, wilaya sita na halmashauri saba, Rais Samia analenga watoto wote wapate elimu bora kwa sababu hakuna urithi unaweza kumpa mtoto sasa hivi zaidi ya elimu, ndio maana kaongeza agenda ya elimu bila malipo ilikuwa inaishia kidato cha nne, sasa inakwenda mpaka kidato cha sita," alisisitiza.

Katika suala la elimu, alisema wajibu wa wazazi ni wajibu wa serikali ambapo serikali inatimiza wajibu wake kwa kutoa fedha na kuwaonyesha njia na kuwataka watendaji wa kata na vijiji kuwashirikisha wananchi katika ujenzi wa madarasa, pia baada ya kukamilika kwa madarasa hayo waendelee kukarabati madarasa ya zamani.

"Rais ametuonyesha njia na sisi lazima tujitahidi kwa kiwango chetu ili tuweze kusukuma maendeleo kwa kuweka mkakati wa kufanya kazi hizi pia, tuendelee kumuunga mkono Rais wetu na kumuomba kwasababu anatupenda na ndiyo maana halali anahangaika kwaajili ya wananchi wake," alisema.

Naye, Msanifu wa Majengo wa Halmashauri ya Meru, Innocent Kibena, alisema ujenzi wa miradi yote wamewapa utaratibu wa jinsi michoro inavyoonyesha pamoja na maelekezo yanayotakiwa kwa mujibu wa viwango stahiki vya serikali.

Mkuu wa Shule ya Msingi Ulong'a, Ester Mneney, akizungumzia ujenzi huo, alisema kuwa Septemba 29, mwaka huu, walipokea fedha Sh. milioni 60 kutoka serikalini mradi wa shule kongwe kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu kazi inayoendelea mpaka hivi sasa. Alisema ujenzi huo ulianza Oktoba 10 na unatarajia kukamilika Desemba Mosi. "Kukamilika kwa mradi huu utawanufaisha walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla ila changamoto tuliyo nayo ni kukosekana kwa nguvu kazi ya wananchi na kusababisha fundi kutumia nguvu kazi ndogo aliyonayo katika ujenzi wa msingi ambayo ni kinyume na matarajio yetu," alisema.

# Ubunifu kikwazo bidhaa Tanzania

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limesema tatizo kubwa linalofanya bidhaa zinazotengenezwa na wajasiriamali wadogo wa Tanzania kushindwa kufanya vizuri katika soko la nje na ndani ni kukosekana kwa ubunifu katika uzalishaji.

Hayo yamo katika taarifa ya Meneja wa SIDO, Mkoa wa Arusha, Japhary Donge, aliyoitoa jana alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kwa wamiliki na wakurugenzi wa viwanda vidogo.


"Msifanye biashara kwa uzoefu hakikisheni mnakuwa wabunifu, zalisheni bidhaa bora zenye viwango vya hali ya juu, kwani kwa sasa kumekuwa na ushindani mkubwa pindi bidhaa zifikapo sokoni," alisisitiza Donge.

Alisema, mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wamiliki na wakurugenzi hao, juu ya utoaji wa huduma za maendeleo ya biashara (BDS), ambayo yalifadhiliwa na UNICO-JICA kwa kushirikiana na SIDO Arusha.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Edward Rwegoshora kutoka Shirika la Kubadilisha na Kuboresha Maisha ya Watanzania (STAWI), aliwataka washiriki wa mafunzo hayo, kuhakikisha wanazingatia yale yote waliyofundishwa na waende wakayafanyie kazi kwa vitendo.

Aliwataka kuhakikisha wanafanya utafiti ili kupata uzoefu na kupima utayari wa upokeaji wa huduma za maendeleo ya biashara, lengo likiwa ni kuendeleza biashara zao na kuvutia wateja wengi zaidi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Diana Mamuya, kutoka kiwanda cha kutengeneza mvinyo cha Anna, alipongeza SIDO kwa kuandaa mafunzo hayo na kueleza kuwa yamekuja kwa wakati muafaka na kushauri muda uongezwe katika kupatiwa mafunzo kama hayo.





## Waonja neema bomba mafuta

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAKAZI wa Misima na Mabanda katika Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, wameanza kuonja 'neema' ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), baada ya kuchimbiwa visima virefu viwili kwa ajili ya kuwasaidia kukabiliana na adha ya maji inayowakabili.

Hadi kukamilika kwa mradi huo, zaidi ya Watanzania 26,563, wanaopitiwa karibu na mradi huo, watanufaika na huduma ya majisafi na salama.

Meneja wa mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya Ujenzi ya Kimataifa ya JV SPEK, Arnold Siliro, alisema kazi ya ujenzi wa kambi ya Mabanda, hadi sasa umegharimu Sh. bilioni 8.9.

Kwa mujibu wa Siliro, mradi huo ulioanza Agosti 12, mwaka huu, umefikia asilimia 46 na unatarajiwa kukamilika Disemba 24.

"Tulifanya taratibu zote za matakwa ya kisheria na kupata vibali mapema ili tusipate matatizo baadae na tufanye kazi kwa muda. Mpaka sasa JV SPEK tuko kwenye asilimia 46.8 ya utekelezaji wetu,"alisema

Aidha, meneja huyo alisema walipofika eneo hilo, walikuta hapakuwa na maji ya kutosha, hivyo waliamua kuchimba visima viwili vinavyowatosheleza wananchi wa kata mbili na mengine kuwasaidia wananchi wa kata jirani.

Pia, alisema katika utekelezaji wao wamefanikiwa kufuata matakwa ya mkataba walioingia na serikali, kwa kuanza kulipa fidia wananchi wote ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi huo.

"Tutakapokuwa tumemaliza utekelezaji wa mradi wetu na kuondoka, basi visima hivi tutawaachia wananchi wa Mabanda na watu wa Handeni, kwa sababu haya maji yaliyopo hapa, yanaweza kutosheleza watu wengi," alisema.

Akizungumzia mradi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, Mwajuma Ukwaju, alisema mradi huo umekuwa chachu kwa Wilaya hiyo, kwa kuwa mji umekua kibiashara na kuchangia kuongeza mapato.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema mradi huo sio tu, utafungua fursa za Wilaya ya Handeni, bali pia Mkoa kwa ujumla wake.

Hata hivyo, Mgumba, alidokeza kuwa mradi huo pia utazinufaisha Wilaya za Handeni, Kilindi, Muheza, Korogwe, Tanga, na Mkinga.

Aliishukuru kampuni hiyo, kwa kuelezwa mkataba wao wa kutumia watu na vitu ndani ya wilaya husika kwa kutoa ajira kwa vijana huku akiwasisitiza kuendelea kuzingatia mkataba huo kwa kufanya kazi nzuri itakayo wawezeaha kuonekana na kupewa kazi nyingine inapotokea uhitaji.

# Mwenyekiti kitongoji akutwa amekufa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KIFO chenye utata, kimewagawa wakazi wa Kijiji cha Sawe kilichoko Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Somanga, Geofrey Massawe, mwili wake kudaiwa kukutwa ukining'inia juu ya mti. Inaelezwa kuwa mwili wa Mwenyekiti huyo, ulikutwa juu ya mti wa mparachichi ukiwa na kamba ya kufungia ng'ombe.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alithibitisha kuwa mwili wa Massawe ulikutwa kwenye mti huo Novemba 2, mwaka huu, majira ya asubuhi.

"Ni kweli mwili wake ulikutwa juu ya miti wa mparachichi lakini tunasubiri taarifa ya 'postmortem' (taarifa ya uchunguzi wa kitabibu) ya nini kimemuua.

"Katika uchunguzi wetu wa awali, marehemu hakuacha ujumbe wowote kuhusu alichokifanya. Kwa hiyo hivi sasa makachero wetu wanaendelea na uchunguzi dhidi ya kifo hicho," alisema.

Mmoja wa wakazi wa Somanga, Sospeter Uronu, alisema alimwona Massawe kabla ya kifo chake akiwa na kamba na alipomwuliza anakwenda wapi, alimjibu anakwenda kukata majani ya mbuzi.

"Hapa kwangu si mbali na nyumbani kwake. Jana (juzi) asubuhi nilimwona akiwa na kamba akaniambia anatafuta majani ya mifugo yake, lakini muda mfupi baadaye tulipata taarifa kwamba kuna mtu amejinyonga na tulipofika tulikuta ni ndugu yetu, inauma sana,"alisema.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sawe, Penda Kimaro, alisema alipigiwa simu na wananchi na kutaarifiwa kwamba wamemkuta mtu akiwa ananing'inia juu ya miti, huku kamba ikiwa shingoni.

"Baada ya kupata tu hiyo taarifa, niliita Polisi wa Kituo cha Polisi Bomang'ombe na walipokuja walimchukua na kumpeleka Zahanati ya Masama kwa ajili ya kumhifadhi,"alieleza



Ofisa Tarafa ya Muheza, mkoani Tanga, Japhet Hayule (kushoto), akishiriki kwenye ujenzi wa madarasa mawili na ofisi moja ya walimu katika shule ya sekondari ya kata ya Magila, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wavamia na kuharibu shamba la utafiti

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WATU wasiojulikana wamevamia na kuharibu vibaya mimea asili iliyoko kwenye shamba la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), lililoko wilayani hapa na kuanza kufanya shughuli za kiuchumi, ikiwamo kukata miti na kuchoma mkaa.

Shamba hilo lililoko eneo la West Kilimanjaro, hivi sasa limekutwa likiwa na matanuri 100 ya mkaa unaotokana na uvunaji haramu wa miti ya asili.

Alipoulizwa kuhusu uharibifu huo wa miti na mazao yake, Mkurungenzi wa Shamba hilo, Dk. Leornad Marwa, alisema kinachoendelea katika mashamba yake ni uamuzi wa taasisi wa kupunguza miti ili kupanda majani kwa ajili ya mifugo.

"Huu ni utaratibu wa kawaida, kwa sababu shamba hili ni la malisho ya mifugo. Kwa hiyo kinachoonekana kinafanyika huko ni usafi unaolenga kupanda nyasi za mifugo,"alisema Marwa

Kabla ya Marwa kutoa ufafanuzi huo, wakazi wa West Kilimanjaro, walitoa taarifa za kueleza kusikitishwa kwao na uharibifu wa mimea ya asili na miti ya asili katika shamba hilo.

John Zakaria, mkazi wa Kijiji cha Miti mirefu alisema: "Katika shamba hili kwa miaka mingi, kulikuwa na miti mingi lakini kadri muda unavyozidi kwenda, miti inazidi kupungua kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo uchomaji mkaa.

"Sawa hatukatai ni shamba la serikali, lakini kwa sisi wadau wa mazingira, tunaona kwamba tunaruhusu ongezeko zaidi la mabadiliko ya tabianchi.

"Kwa nini viongozi wa TALIRI waruhusu watu kukata miti na wengine kuchoma mkaa. Hii ni ajabu, kwa sababu serikali inahimiza watu kupanda miti, wao wanawaruhusu kukata miti," alisema.

"Sisi kama wadau wa mazingira, kwa hali ya sasa ilivyo ya ukosefu wa mvua, kila mtu anaona wanyama wana kufa, mgao wa maji unaitikisa nchi, kwa kweli hatujafurahishwa," aliongeza.

Grace Mwanri, mkazi wa Wiri, akizungumzia uharibifu huo wa mazao ya miti ya asili, alisema kwa miaka zaidi ya 30, katika shamba hilo kulikuwa na miti ya kutosha lakini kwa sasa inayoonekana ni ardhi na hakuna tena ikolojia ya misitu ya asili iliyopo.

Naye, Anna Mosses, mkazi wa Ngarenairobi, alisema viongozi wa shamba hilo wanapaswa kuwa makini na ukataji miti huo na uchomaji mkaa, kama nia ni kufanya usafi wasingeruhusu mimea hiyo iteketezwe.

"Miti inayokatwa katika eneo hilo, ni miti ya asili ambayo ni migunga ambayo wanyama kama Twiga, Tembo na wanyama wengine wanapenda kuitumia kama chakula," alisisitiza.



# Chuo chapewa somo udahili wa wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Benjamini Mkapa kimetakiwa kudahili wanafunzi kulingana na uwiano wa rasilimali zilizopo ikiwa ni pamoja na sehemu za kujifunza kwa vitendo ili kupata wataalam wenye umahiri na weledi wa kutosha .

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Paschal Rugajo, alisema hayo juzi katika Hospitali ya Benjamini Mkapa wakati wa uzinduzi wa chuo hicho ambacho kimeanzishwa kwa ajili kuzalisha wataalam wa mionzi.

"Ili kuhakikisha ubora wa wataalam wanaozalishwa kwenye chuo hiki ,naelekeza mhakikishe kuwa udahili wa wanafunzi unakuwa kwa uwiano wa rasilimali zilizopo ikiwa ni pamoja na sehemu za kujifunzia kwa vitendo ,epukeni kudahili wanafunzi wengi kwa lengo la kupata fedha bila kujali ubora wa mafunzo utakaopelekea upatikanaji wa wataalam wenye umahiri na weledi wa kutosha," alisema.

Aidha, Prof. Rugajo aliipongeza Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa hatua hiyo ya kuanzisha chuo cha kuzalisha wataalam wa mionzi huku akiutaka uongozi kuwasilisha andiko la ujenzi wa jengo la chuo .

"Mnapaswa mliweke hili kwenye bajeti yenu ili tuone namna tutakavyoweza kushirikiana nanyi katika ujenzi wa jengo hilo." Alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, alisema chimbuko la kuanzisha mafunzo hayo lilitokana na changamoto ya upatikanaji wa wataalam wa kada hizi ngazi ya cheti na diploma wakati wa kujaza nafasi za ajira katika hospitali hiyo.

"Mfano tulibaini uhaba mkubwa wa radiographer (wataalamu wa mionzi) na Anaethetists (wataalam wa dawa za usingizi na ganzi) kwenye soko suala ambalo lilitulazimu kuomba vibali vya kuhamishia wataalam wa kada hizi kutoka vituo vingine ambavyo navyo vilikuwa na uhaba wa wataalam hawa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mafunzo ya Radiolojia yameanza kutolewa tangu Oktoba 3, mwaka huu, na kwamba mafunzo mengine yanayotarajiwa kutolewa ni utabibu wa meno, mazoezi kwa ajili ya tiba na uchunguzi wa macho.

Kwa mujibu wa Dk. Chandika. hospitali hiyo imedhamiria kuanzisha mafunzo hayo kutokana na uwepo wa vifaa tiba vinavyowezesha wanafunzi hao kujifunza kwa vitendo.

"Kwa ujumla wake mafunzo haya yatasaidia Wizara ya Afya kutimiza azma yake ya kuboresha huduma za afya kwa kutoa wataalam wenye weledi mkubwa hususan katika awamu hii ya sita ya serikali ambapo kuna uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba na miundombinu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya," alisisitiza Dk.Chandika

# Kumekucha uhakiki mali viongozi wa umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imetangaza kuanza uhakiki wa rasilimali, maslahi na madeni kwa viongozi wa umma 658 wakiwamo mawaziri, naibu mawaziri, majaji na makatibu wakuu.

Watakaobainika kuwa na kasoro katika uhakiki wa mali na rasilimali hizo, watafikishwa kwenye Baraza la Maadili.

Aidha, kwa mwaka jana, viongozi 36 kati ya 425 waliohakikiwa walibainika kuwa na dosari mbalimbali na kufikishwa kwenye baraza hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamishna wa Maadili, Jaji wa Rufani Sivangilwa Mwangesi, alisema kazi ya uhakiki itaanza Novemba 7 hadi 18, mwaka huu.

"Viongozi watakaohakikiwa ni baadhi ya mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu na wengine wa kada mbalimbali. Uhakiki utafanyika kwenye mikoa 10 ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Lindi, Njombe, Dodoma, Tanga, Geita, Mwanza, Tabora na Iringa," alisema.

Aliwataka viongozi wanaofanyiwa uhakiki kufanya maandalizi kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa huku wito ukitolewa kwa wananchi wenye taarifa muhimu kuhusu rasilimali na madeni ya viongozi kutoa ushirikiano.

Aliwaomba wakuu wa mikoa, makamanda wa polisi na mamlaka zingine kutoa ushirikiano kwa maofisa watakaofika kwenye maeneo hayo ili kufanikisha uhakiki huo.

Alisema kwa viongozi wanaokutwa na dosari hufikishwa kwenye mahakama yao ambayo ni baraza la maadili.


"Nitoe tahadhari kwa viongozi wahusika wajihusishe na watu watakaokuja na vitambulisho vya kuonesha hao ndio wahusika wa sekretarieti ili wasiangukie kwenye mikono ya matapeli ambao huingilia mchakato huo," alisema.

Kadhalika, aliwakumbusha viongozi wote ambao wanapaswa kutoa matamko yao ya rasilimali, maslahi na madeni ya mwaka 2022 kutimiza takwa hilo la kisheria.

"Matamko ya viongozi yameanza kupokelewa kuanzia mwezi Oktoba na tarehe ya mwisho ni Desemba 31, mwaka huu,"alisema.

Katibu wa Idara ya Usimamizi wa Maadili, John Kaole, alisema kwa mwaka 2021 ulifanyika uhakiki wa viongozi 425 na kati yao, 36 walibainika kuwa na kasoro kwenye masuala ya mali na mgongano wa maslahi.

"Hatua zilizochukuliwa kuna ambao wamepelekwa kwenye uchunguzi na hatimaye kwenye baraza la maadili lakini kuna wengine kasoro zao zilikuwa zinarekebishika walipewa ushauri wa kurekebisha, na wengine hawakujaza vizuri matamko suala hilo lilipelekwa idara ya elimu ya umma ili kutoa elimu ya ujazaji," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. Bilioni 1.3 kwa vikundi vya wajasiriamali wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, jijini Dodoma mapema wiki hii, iliyotolewa na Halmashauri ya Jiji hilo, kupitia mikopo ya asilimia 10. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanaoitukana serikali mtandaoni waonywa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa, amesema kwa uwekezaji ambao serikali imeufanya katika sekta ya mawasiliano nchini hakuna mtu ambaye anaweza kufanya uhalifu mtandaoni akabaki salama.

Aidha, amewataka Watanzania badala ya kutumia mitandao ya kijamii kuitukana serikali na viongozi wake, watumie fursa zilizopo kwenye mpango wa Tanzania ya Kidijiti kujikwamua kiuchumi.

Msigwa alisema hayo jana mara baada ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Bakari Jabir, kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kuanzia Julai, 2021 hadi Septemba, mwaka huu.

Alisema kutokana na uwekezaji ambao serikali imefanya hivi sasa katika sekta hiyo ya mawasiliano nchini ni vigumu kwa mtu yeyote kufanya uharifu wa kimtandao na akabaki salama bila kukamatwa.

"Kwa namna ambavyo serikali hii ya awamu ya sita ilivyo wekeza katika sekta hii na vyombo vya dola vilivyo hakuna mtu anaweza kufanya uhalifu akabaki salama watu wengi wanakamatwa sema ni huruma yetu lakini wakitaka iko siku tutawataja. Unakuta wengine vijana wadogo tu wanatumika kuitukana serikali na viongozi wake," alisema Msigwa

Pia aliwataka Watanzania kutumia fursa zilizoko kwenye sekta ya mawasiliano kuanzisha vitu ambavyo vitawasaidia kujikwamua kiuchumi badala ya kuendelea kutumika kuitukana serikali.

Awali, Dk. Bakari akiwasilisha taarifa yake alizitaja baadhi ya kero katika sekta hiyo nchini kuwa ni pamoja na uharibifu wa miundombinu ya mawasiliano.

"TCRA imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwenye kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulinda miundombinu ya mawasiliano" alisisitiza.

Alisema kero nyingine ni utoaji wa huduma za mawasilino kwa wote kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa bado.

Hata hivyo, alibainisha namna ambavyo wamekuwa wakikabiliana na kero hizo kupitia kituo cha kitaifa cha usalama mtandaoni (TZ-CERT) ambacho kimeendelea kukabiliana na uhalifu mtandaoni ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau.

"TCRA imeendelea kusimamia ubora wa huduma za mawasilinao kwa kutumia mitandao ya kisasa ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na watoa huduma zinakidhi viwango bora," alisema



**HABARI ZANZIBAR**

## Mkakati wawekwa kuitangaza Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WIZARA ya Utalii na Mambo ya kale imejipanga kutangaza utalii katika kisiwa cha Pemba yakiwamo magofu yaliyobeba historia ya kale hadi kufikia watalii 100,000 ifikapo mwaka 2025.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Fatma Mbarouk Khamis, alisema hayo jana alipozungumza na watendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kisiwani Pemba na kutembelea baadhi ya majengo ya kale ambayo ni sehemu ya vivutio vya utalii.

Alisema, serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya utalii Pemba ikiwamo ujenzi wa uwanja wa ndege pamoja na bandari tatu na barabara muhimu zinazounganisha mikoa miwili ya kisiwa hicho.

Fatma alisema barabara ya Chake Chake hadi Wete, Pemba yenye urefu wa kilomita 22.2 inatarajiwa kujengwa na maandalizi yake yako katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza na kukamilika kwake kutarahisisha mawasiliano.

Pia, alisema tayari wamekamilisha ujenzi wa magofu ya kale yaliyobeba historia ikiwemo Mkamandume Pemba ambayo yatasaidia kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Pemba.

Alisema uwekezaji katika baadhi ya visiwa vidogo vilivyoko Pemba kikiwamo Misali kwa kiasi kikubwa utasaidia kuitangaza Pemba katika rasilimali za viumbe vya baharini katika utalii wa kuzamia.

Naye Afisa Mdhamini wa Wizara hiyo, Zuhura Mgeni Othman, alisema idadi ya watalii wanaotembelea Pemba imeanza kuongezeka kwa watalii 732 katika mwezi wa April hadi June mwaka huu na mwezi Septemba idadi imeongezeka na kufikiya 2,000.

''Matarajio yetu hadi ifikapo mwaka 2025 sekta ya utalii Pemba itaimarika na kupokea watalii 80,000 baada ya kukamilika kwa miradi muhimu ya miundombinu ya barabara na bandari na uwekezaji wa ujenzi wa hoteli za kitalii katika visiwa vidogo," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Makumbusho ya kale Pemba, Maryam Mansab, alisema wamefanikiwa kwa asilimia 80 kuyawekea maelezo ya majengo ya kale na makumbusho yaliopo Pemba ikiwemo historia yake kwa wageni.

"Majengo mengi yaliyotambuliwa na makumbusho ya utalii yaliyopo Pemba yamewekewa maelezo yake hatua ambayo imerahisisha watalii wanaokuja kufahamu huku wengine wakifanya kazi za kitafiti," alisema.

# Timu yaundwa kuchunguza kupanda maji ya bahari katika makazi ya watu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imepeleka timu ya wataalamu kufanya uchunguzi wa tukio la kupanda kwa maji ya bahari katika makazi ya wananchi wa kijiji cha Nungwi ili kunusuru athari iliyojitokeza.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo lilotokea hivi karibuni.

Alisema kupanda kwa maji ya bahari kunatokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Shajak alisema tukio kama hilo lilishawahi kujitokeza katika miaka ya nyuma katika kijiji hicho na fukwe zimeshaathiriwa na mmong'onyoko wa ardhi kutokana na kupanda kwa maji ya bahari.

Alisema kupanda kwa maji ya bahari kunatoa tahadhari kwa Zanzibar kuwa ina hali ngumu inayoweza kusababisha athari kwa jamii, hivyo ni vyema kuongeza nguvu za kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Moja ya kazi kubwa inayofanywa na serikali, alisema ni tathmini ya athari za kimazingira ambazo imejitokeza katika maeneo mbalimbali na kuchukua hatua za kukabiliana na athari hizo. "Tukishapata majibu ya athari za kimazingira tutajua nini cha kufanya katika kuchukua hatua maana watu wanafikiri kuwa kila sehemu tunaweza kujenga ukuta wa kuzuia maji ya bahari. Lakini njia nyingine ya kuzuia maji ni kupanda mikoko," alisema.

Kwa mujibu wa Shajak, athari za mabadiliko ya tabianchi zipo, hivyo wananchi wanapaswa kutoendeleza mambo yanayoweza kusababisha madhara ikiwamo kukata mikoko na kuchimba mchanga katika fukwe kwa ajili ya ujenzi.

Alisema, kijiji hicho si mara ya kwanza kupata athari ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa mwaka 2012 serikali ilizindua mradi wa maji safi na salama kijijini hapo baada ya maji waliyokuwa wakitumia kuvamiwa na maji ya bahari.

"Eneo lote la Nungwi limekumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na hawana uwezo wa kupata maji safi na badala yake wanapata maji ya chumvi, hivyo serikali ililazimika kuchimba visima katika kijiji jirani cha Potoa kwa ajili ya wananchi wa nungwi kupata maji safi" alisema Dk. Shajak.

Aidha, alitaka jamii kushiriki kwa pamoja kuendeleza mapambano ya mabadiliko ya tabianchi ili Zanzibar kuwa salama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Dk. Shajak alisema Zanzibar ni kisiwa hivyo imeathirika na mabadiliko ya tabianchi hasa kutokana na hali inavyojitokeza duniani na matokeo yake maji kupanda katika nchi kavu.

Alisema, Zanzibar ina maeneo 143 ambayo yameathirika na yanahitaji uharaka wa kufanyiwa kazi ili kudhibiti maji ya bahari kuvamia makazi ya wananchi na tayari serikali imeshatenga Bilioni nne kwa ajili ya kukabiliana na athari hizo.

Awali, wananchi wa kijiji cha Nungwi wakizungumza na Nipashe walisema wako hatarini kupoteza nyumba zao kutokana na maji ya bahari yanayojaa na kufika katika makazi yao.

Hali hiyo iliyojitokeza wiki moja iliyopita ilizua taharuki kubwa baada ya maji hayo kuvamia soko la samaki ambalo liko karibu na makazi ya wananchi huku wananchi wa kijiji hicho wakisema kama hatua za haraka hazitachukuliwa nyumba zao zitaathirika.




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti ya REPOA, Donald Mmari (kulia) akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano na shirika la PASGR la nchini Kenya, kuhusu kuijengea uwezo wa kitafiti na sera. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# REPOA, PASGR zaungana kuboresha utafiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Utafiti na Sera (REPOA) na Shirika binafsi la PASGR lenye makao yake makuu nchini Kenya, zimetiliana saini hati ya makubaliano kujengea uwezo wa utafiti na sera.

Hafla ya utiaji saini huo ilifanyika jana katika hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar ambapo PASGR itakuwa na kazi ya kujenga uwezo kwenye sera za umma na utawala bora ndani ya Afrika.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema lengo la makubaliano hayo ni kupanua wigo na kuwajengea uwezo watafiti na watunga sera ndani ya Afrika, katika kuangalia namna ya kuwawezesha wananchi kuimarisha na kuongeza tija katika uzalishaji katika sekta mbalimbali.

Dk. Mmari alisema kuna shida ya kupata masoko na mitaji na changamoto nyingi za mabadiliko ya tabianchi na kwa sasa yanafanyiwa utafiti na kuongeza uwezo na kujifunza kutokana na wengine ambao wamefanikiwa katika nchi za Afrika.

Alisema, namna ya kufanikiwa ni pamoja na kubadilisha uzoefu na kufanya utafiti wa pamoja ndani na nje ya Tanzania.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa PASGR, Antony Mveyange, alisema wakati umefika Watanzania kujifunza kutoka nchi zingine katika masuala ya utafiti wa sera za umma ili kuleta matokeo chanya katika sekta hiyo.

Alisema, hatua ya makubaliano na REPOA itawajengea uwezo watafiti kuona namna ya kuimarisha utafiti wa kisera unaojiekeleza kutatua changamoto zinazoleta vikwazo hasa kwa vijana kuwa washiriki katika uzalishaji, kuajiriwa nakutambua fursa za kujiajiri.

"Nafasi hii ni muhimu itatoa wigo kwa Watanzania kupata mafunzo na kufanya utafiti mbalimbali ndani ya nchi, Afrika na nje ya Afrika ambao utawasaidia watunga sera," alisema.

Alisema taasisi hiyo ina uzoefu kufanya utafiti masuala ya sera za umma na utawala bora katika takriban nchi 26 za Afrika.




**AMBER**

UKURASA 15

Nipashe BT

JUMAMOSI NOVEMBA 5, 2022



# DAVIDO


## AENDELEA KULIWAZWA

UKURASA WA 20

YUKO WAPI ?

# SALUM ABDALLAH-4

## Mwanamuziki mkongwe tajiri, Mtunzi wa kibao 'Mkono wa Idd'



**Na Adam Fungamwango**

KWA wiki zote tatu za historia ya mwanamuziki Salum Abdallah Yazidu (SAY), tuliangalia historia yake, alivyozaliwa na kuanza muziki kwa shida, hadi alipotoka nchini Cuba na kuishia Mombasa nchini Kenya, na kisa cha kurejeshwa nchini kiasi cha baba yake sasa kumuachia afanye atakavyo.

Tumeona baada kuachwa akawa mwanamuziki haswa, staa na kuwashangaza wengi hata waliokuwa wakimfanyia zengwe kwa baba yake.

Akatunga na kurekodi nyimbo nyingi zilizompatia umaarufu hadi leo hii ambazo ni "Ngoma Iko Huku', 'Shemeji Shemeji','Mkono wa Idd', 'Wanawake Tanzania', 'Sipati Majibu,' 'Naumia', 'Cuba Chacha' na 'Ewe Mola Wangu. na 'Ewe Mola Wangu' wimbo wa mwisho wa mwanamuziki huyo kabla ya kufariki, na mashairi ya wimbo huo yalitafsiriwa na mashabiki kuwa alikuwa anatabiri kifo chake.

Leo tuaangalia ajali aliyoipata mwanamuziki hiyo na jinsi kilivyotokea.

Bendi mbili kubwa maarufu za pale Morogoro mjini zote zilitegemea kupiga siku hiyo, na pia zilipangiwa kutembelewa na viongozi hao.

Kutokana na ushindani mkubwa wa bendi hizo wanamuziki na washabiki wa bendi hizo walikuwa roho juu kusubiri mpambano wa usiku huo.

Kwenye muda wa saa kumi na mbili jioni baada ya shamrashamra za kupokea viongozi kwisha bwana Ramadhan Mdidi aliyekuwa msaidizi wa mmoja wa madereva wa Salum, alikuja kumueleza mkuu wao huyo kuwa moja ya gari lake limenasa kwenye mchanga katika mkondo wa mto walikokuwa wakichimba mchanga, kwa hiyo ilikuwa busara kuliondoa gari usiku uleule au la mvua ingenyesha gari lingeweza kuchukuliwa na maji.

Salum Abdallah akaagiza gari likavutwe.

Salum ndiye aliyekuwa kiongozi muimbaji wa bendi ya Cuban Marimba, pia alikuwa ana malori kadhaa aliyokuwa akiyatumia katika mradi wa kujenga nyumba za National Housing pale Morogoro, kama nilivyoeleza huko awali kuwa alikuwa pia anaendesha mali na biashara za familia yao na za kwake pia.

Alhamisi tarehe 18 Novemba, 1965 ilikuwa siku yenye hekaheka kubwa mjini Morogoro, ugeni mkubwa ulikuwa unasubiriwa katika mji huo. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, viongozi wakuu wa nchi wakati huo, walikuwa wakisubiriwa



na wananchi wa hapa katika sherehe ya kufungua Chuo cha Kilimo ambacho kwa sasa kinajulikana kama SUA (Sokoine University of Agriculture). Pamoja na wageni hao pia alitegemewa kuwepo aliyekuwa Mbunge wa Morogoro mjini wakati huo Mheshimiwa Oscar Kambona.

Salum akamtuma mwanamuziki wake Waziri Nyange atangulie kwenye ukumbi ambako wangepiga muziki ili kujaribu vyombo tayari kwa onyesho la usiku ili yeye aende na lori jingine kwenda kuvuta gari lililonasa kwenye mchanga.

Siku hiyo Cuban Marimba walikuwa wapige muziki Community Center wakati wenzao HYPERLINK "https://sw.wikipedia.org/w/index.php?title=Morogoro_Jazz_Band&action=edit&redlink=1" \o "Morogoro Jazz Band (bado haujaandikwa)" \t "_blank" Morogoro Jazz Band walikuwa wapige Kichangani.

Kiasi cha saa moja hivi mmoja wa waliokuwemo kwenye lori lililoondoka na Salum Abdallah, alirudi mbio nyumbani na kuwataarifu kuwa kumetokea ajali na Salum ameumia. Ajali hii ilikuwa ya ajabu na imekuwa daima ikileta maneno kwa walioikumbuka.

Kwa maelezo ya waliokuwepo, giza lilikuwa limekwisha ingia na wakati lori likikaribia Msamvu, taa zilizimika ghafla na gari ikayumba lakini taa zikawaka tena, kiasi cha waliokuwemo kuanza kucheka, lakini kicheko chao kilikatika ghafla baada ya kugundua kuwa mlango wa upande aliokuwa amekaa Salum ulikuwa wazi naye amedondoka.

Walirudi nyuma na kumkuta akiwa kalala barabarani akiugulia maumivu.

Mzungu mmoja alipita wakati uleule na gari dogo akawapa lifti watu wawili toka kwenye lile lori, mmoja akaenda nyumbani kwa Salum kutoa habari na mwingine akaenda kuchukua taxi iliyomchukua majeruhi mpaka hospitali. Wote waliopata habari wakakimbilia hospitali wakamkuta mwenzao anaugulia maumivu, madaktari walimuomba anyooshe mikono na kisha miguu alipoweza, wakaamini hajavunjika bali ni maumivu ya juu juu ambayo yangeisha, kiasi cha kumruhusu arudi kwake na awahi matibabu kesho yake asubuhi.

Salum mwenyewe akawaambia wenzie wafungue vyombo wasipige dansi siku ile, wengi wakakesha nae.

Usiku kucha ulikuwa wa maumivu makubwa, asubuhi mgonjwa alipelekwa hospitali akafanyiwa upasuaji ikagundulika alivunjika kiuno na mifupa kupasua kibofu cha mkojo, jambo ambalo kutokana na kuchelewa kugundulika lilikuwa ni baya sana.

Kama saa saba mchana alitolewa chumba cha upasuaji na wenzie waliokuwa wakisubiri wakaambiwa waende makwao wakale vizuri ili waje baadaye kutoa damu kwa ajili ya mgonjwa.



# AMBER LULU HUYOOO!
## Kuvaa shela la harusi

NANI kasema haolewi? Basi kama ulikuwa unawaza kwamba mpambaji wa video za muziki, Amber Lulu, hawezi kuwekwa ndani tena kama mke, basi jua imekula kwako.

Katika taarifa za ndani, Amber Lulu yupo katika maandalizi ya kuolewa kwa mara ya pili, tena safari hii kwa kijana mbichi ambaye mwenyewe anajinasibu kwamba amefika mwisho kimahaba.

Katika jumbe zake anazochapisha za hivi karibuni katika mitandao ya kijamii, Umber Lulu, kila wakati amekuwa akimsifia mpenzi wake huyo wa sasa, huku akimshukuru Mungu kumwonyesha mtu sahihi.

Katika Insta Stori, Amber Lulu amewaambia mashabiki wake kwamba hivi karibuni atafunga ndoa.

"Naolewa. Asante Mungu, sijatarajia hili," Lulu ameandika.

Awali, msanii huyo amekuwa akipakia picha za kimahaba akiwa na msanii wa Bongo Fleva The Dream, hivyo kuongeza minong'ono kwamba msanii huyo ambaye ni mdogo kwake ndiye mume wake mtarajiwa.

Jana pia alitupia video fupi katika akaunti yake ya Instagram, akionekana akirembwa huku akiambatanisha na ujumbe unaosomeka 'Bi Harusi mtarajiwa'

Awali msanii huyo aliwaambia mashabiki zake kwamba alikuwa amepata mpenzi anayempenda mwanawe

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag

**@burudanitele**





**@shamsaford**
Wanaume mnawachanganya sana hawa michepuko. Mnasema hamna furaha na ndoa zenu lakini wake zenu wajawazito kila siku.

**@lizabethmichaelofficial**
Saluni sio sehemu ya umbea tu sikuhizi wote tumeelimika. Huku sisi tunapeana elimu na kushauriana ni jinsi gani tutawapa kilicho bora.





**@roma_zimbabwe**
Tunapoingiza tumbo ndani basi muwe mnatupiga picha fasta, sio mnachelewa, tunapumua kwa shida wenzenu.

**@kajalafrida**
Ukomavu ni wakati furaha yako haitegemei watu wengine





**@masanjamkandamizaj**
MUNGU ATUSAIDIE SANA!!Uwongo ni Dhambi!NAWAKUMBUSHA TUU RAFIKI ZANGU

## BASI SAWA

### Sammy William azidi kupasua anga



MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi nchini, Sammy William, amewashukuru mashabiki kwa mapokezi makubwa ya wimbo wake, 'Ni Wewe' aliomshirikisha Neema Ntigonza na sasa anajiandaa kuachia ngoma nyingine.

Akizungumza na BT, Sammy alisema miongoni mwa nyimbo zilizomtambulisha vyema na sasa anamshukuru Mungu kwa kuzidi kupasua anga kwenye tasnia hii.

"Namshukuru Mungu yeye ndio amezidi kunipaisha, wimbo Ni Wewe umenipa nafasi kubwa kwenye tasnia na nimeona nikipata sapoti kutoka kila pande na wadau mbalimbali, mashabiki wakae mkao wa kula," amesema Sammy.

### Vanillah awaomba mashabiki wambebe



MWANAMUZIKI mpya kutoka Lebo ya King music, Vanilla Music, amesema ndoto yake haitakamilika kama mashabiki hawatampokea na kukubali ngoma zake.

Msanii huyo ambaye anasifika kwa kutunga mashairi, kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema atafanya kila awezavyo kuhakikisha ladha ya muziki inazidi kuwa tamu kutoka kwake.

Vanillah Music ni mmoja ya wasanii waliohusika katika uandishi wa ngoma ya UTU ya mkongwe Ali Kiba ambayo inafanya vizuri.



## VANESSA MDEE KUMBE CHA WIVU

IMEELEZWA kuwa kwa sasa msanii wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee, hataki utani kwa mume wake Rotimi, kiasi kwamba ameamua kumzalia watoto mfululizo ili kumdhibiti na macho ya nje.

Vanessa hivi karibuni ametangaza kutarajia kupata mtoto wa pili na mume wake huyo kutoka Nigeria, baada ya mtoto wao wa kwanza Seven kufikisha umri wa miaka miwili.

Kulingana na chanzo cha karibu cha msanii huyo, kimesema mwanamuziki huyo amekuwa na wivu uliopitiliza kwa Rotimi na kumpatia watoto ni sawa na kumdhibiti kuepukana na vishawishi kutoka kwa warembo wengine wanaomtolea macho.



## Tundaman amuonya Ali Kiba

MWANAMUZIKI kongwe wa Bongo Fleva, Tundaman amemuonya Ali Kiba kwamba anaweza kuweka katuni kwenye video kana hatakubali kwenda kushuti video ya wimbo wao.

"Namwambia Ali Kiba, mwezi huu kama Ali Kiba na Darassa hatawajitokeza kushuti video naweza kuweka katuni, naomba wajitokeze tufanye kazi,"Amesema.

Amesema, ngoma hizo zipo katika EP yake ya nyimbo saba ambayo imewashirikisha wasanii wengi wa zamani.

## NGOMA ZILIZOZAA MISEMO ILIYOTRENDI

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA inaenda kasi sana. Leo unaweza kukuta watu wanafanya hivi, lakini kesho wakabadilika na kufanye vile. Ndiyo maana kwa sasa usikariri maisha.

Kila kukicha kila kitu kinabadilika. Hata misemo nayo inabadilika. Hapo nyuma kidogo wala si siku nyingi kulikuwa na misemo kama 'mabaharia' na mingine mingi.

Hivi sasa kuna misemo mingine kabisa. Ingawa ukiisikiliza si mipya, lakini sababu kubwa ya 'kutrendi' ni kusemwa au kutolewa na watu maarufu kama vile wanamuziki, wasanii, wanamichezo, waigizaji na watu wengine ambao wanaushawishi kwenye jamii.

Leo tunawaletea misemo kadhaa ambayo 'ilitrendi' huko nyuma pamoja na watu maarufu walioitambulisha, au kuitunga misemo hiyo.

**Habari ndiyo hiyo-Mwana FA**

Naweza kusema kuwa hapa Tanzania hakuna msanii ambaye ametengeneza misemo mingi 'iliyotrendi' kama Mwana FA. Kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Muheza na jina lake kamili ni Hamisi Mwinjuma. Huyu unaweza kumwita ni baba wa misemo ya Kibongo.

Alitoa ngoma iitwayo 'Habari Ndiyo Hiyo'. Jina la ngoma hii nalo likawa msemo 'uliotrendi' sana Bongo. Mtu alimwambia mtu kitu akashangaa, au akimpasha ukweli atamwambia 'habari ndiyo hiyo.'

**Unanitega?- Mwana FA**

Ilikuwa ni katikati ya miaka ya 2000, Mwana FA kama kawaida yake akatoa ngoma nyingine akaiita 'Unanitega?' 'Mbona miguu iko wazi unanitega? (aa-aaa), kifua kiko wazi unanipenda? (hebu huko).

Msemo huu nao ulitawala sana hasa kwa vijana kwenda kwa wasichana ambao walionekana kuvaa nguo zisizo na stara wanapopita mbele yao.

**Unan'taka Kwio-Meja Kunta**

Msanii wa Singeli Meja Kunta, yeye alikuja na msemo ambao ulitrendi sana hasa kwa akinadada wa 'unamtaka kwio, unahela kwio, kwio hiyo kwio'. Hii ilitokana na ngoma yake ya 'Wanga'.

**Usinifokee-Baba Levo**

Msanii Baba Levo, naye alikuja na msema wake msemo wake uliotamba sana mitaani na kwenye mitandao wa kijamii usemao 'Usinifokee'.

**Ni Yeye-TID**

Ni msanii mkongwe ambaye ni mwanzilishi wa msemo wa 'Ni Yeye'. Msemo huo ukawa maarufu na kuanza kutumiwa na watu wengi wakiwamo hata wanasiasa Ilifika wakati alianza kulalamika kuwa amechukuliwa msemo wake na watu wanautumia bila yeye kupata chochote.



## FILAMU

# Malkia Anita: Ubaya hauna posho

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote ubaya hulipwa kwa ubaya tu. Ukimfanyia mtu ubaya, hata kama yeye hatokulipa, lakini Mungu humlipia kile ambacho ulichomfanyia mwenzako.

Kwa hiki nilichokiandika hapa, leo tutaitazama filamu iitwayo 'Malkia Anita'. Ni moja ya filamu kali sana na cha kufurahisha kidogo imetungwa na kuchezwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ikichezwa na wasanii kutoka nchini humo, lakini wakiigiza kwa lugha ya Kiswahili.

Waliocheza filamu huu ni Celine Mirimo, Shaaban Groile, Georges Bulere Ushindi, Laetitia Munihire, Janvier Bulenda, Fatuma Kikongo, Clarisse Mirimo, na wengineo.

Inaanza kuonyesha kwenye moja kati ya vijiji vya Congo DR, binti mmoja akiishi kwa manyanyaso makubwa kutoka kwa mama yake mdogo.

Binti huyo anaitwa Anita ambaye baba na mama yake walifariki akiwa bado mdogo kwenye vita na akalelewa na mama yake mdogo aitwaye Fatuma.

Sarah binti wa Fatuma wanashirikiana kumtesa Anita, wakiwa hawafanyi kazi yoyote zaidi ya kumgeuza binti huyo kijakazi.

Kwenye himaya hiyo kuna mfalme alitwaye Bauba. Ana watoto wawili wa kike na wa kiume ambao wanasoma kwenye mji mkuu wa Kinshasa.

Wakati wa likizo walirejea nyumbani. Mfalme akafanya pati kubwa sana kwa watoto wake kurejea likizo.

Bayeni ni mtoto wa kiume na Sakina wa kike. Katika pitapita yake kuangalia himaya ya baba yake anasikia sauti safi kama ya kinanda. Lakini wimbo ni wa masikitiko mno. Anamkuta msichana mmoja



ambaye angeonekana mrembo kama si mavazi makukuu aliyovaa na kukosa matunzo.

Alikuwa amejikunyata shambani. Mtoto wa mfalme Bayeni alimkuta na kumuuliza kama ana shida. Akakataa. Mtoto Hakuna aliyejua ni nani. Kila mtoto wa kike alijipamba, akapambika, akidhani ndiye atachukuliwa.

Anita aliachwa nyumbani kwa ajili ya kufanya kazi, pia hakuwa na mavazi mazuri. Alipoondoka, mtumishi wa mfalme akamletea mavazi mazuri ya gharama. Alipotokea kwenye sherehe kila mmoja alishangaa. Bayeni akamtambulisha kuwa ndiye mchumba wake.

Sarah na mama yake hawakukubali, walimfanyia ulozi na binti huyo akageuka mwendawazimu. Ugonjwa huo wa akili ulichukuliwa sababu ya Sarah kujipendekeza kwa mtoto wa mfalme ili aolewe yeye. Haikuwezekana. Mganga wa kijiji alifanikiwa kumponya Anita. Akabainisha kuwa alifanyiwa ulozi na Sarah kwa kushirikiana na mama yake. Kwa aibu Saraha alipatwa na mshtuko wa moyo akafa. Mfalme akatoa idhini Fatuma apewe adhabu kali kesho yake. Kabla ya adhabu yeye mwenyewe akajinyonga. Bayeni akapewa ufalme na baba yake Bauba, Anita rasmi akawa binti mfalme.

BONGO FLEVA

# KIKWETE NDANI YA 'DEDICATION'

# Ommy Dimpoz aahidi burudani ya kipekee



**Na Beatrice Shayo**

BAADA ya kimya kirefu, msanii wa Bongo Fleva, Ommy Dimpoz, leo anazindua kibabe albamu yake mpya yenye ngoma 15 kali.

Uzinduzi huo wa albam inayoitwa 'Dedication' mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

Burudani ya uzinduzi huo itafanyika katika hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam. Akizungumza jana, Dimpoz amesema mbali na Rais Kikwete pia amewaalika baadhi ya mabalozi , Mawaziri, wanasiasa na wasanii.

"Baada ya pati tutaenda pale Elements tutajumuika na watu wote kwa maana huu ukumbi wa Rotana hautatosha wote lakini baada ya kesho nawakaribisha watu wote kule kidimbwi," amesema.

Dimpoz amesema, sababu ya kumchagua Kikwete kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, kuwa ni kiongozi anayependa wasanii na amekuwa mmoja wa watu waliokuwa wakimjulia hali kila wakati alipokuwa anaumwa.

"Kikwete amekuwa zaidi ya kiongozi kwangu, wakati nilipokuwa naumwa amekuwa akijulia hali kila mara lakini ni mtu anayependa wasanii wengi pia hapa nchini, nilitamani pia hata Rais Samia Suluhu Hassan lakini yupo katika ziara China," ameongeza

Hata hivyo ameeleza viongozi mbalimbali wanatarajia pia kuudhuria katika uzinduzi huo ambao umejaa na matukio ya kuburudisha mashabiki zake.

Dimpozi amesema albamu ameipa jina la Dedication kutokana na mengi aliyopitia wakati anatafuta maisha hivyo ni kama amewapa zawadi mashabiki wake.

"Nimepitia mambo mengi maisha yangu ni Dedication nikaona sio vibaya albamu yangu kulipa hilo jina ingawa katika hizo nyimbo 15 hakuna nyimbo inayoitwa Dedication," alisema Dimpoz.

Nyota huyo ameeleza kwamba albamu hiyo tayari iko katika mitandao yote.

Baadhi ya wasanii aliowashirikisha ni Marioo, Nandy, Fally Ipupa, Dj Kerozen, Blaq Diamond, Julio Masid na wengine.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**

Kama kawaida yao, leo Jumamosi wapo ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, kesho Jumapili watakuwa katika ukumbi wa Platnum Kijichi.

**Msondo Ngoma**

Kama kawaida kila Ijumaa wapo Gwambina Lounge, leo Jumamosi watakuwa ndani ya ukumbi wa Makutano Park Vikindu Pwani na kesho watamalizia wikienda ndani ya ukumbi wa Dar Safari Buza.

**Town Classic Band**

Bendi hii mpya iliofanya onyesho la 'listening part' Jumamosi iliopita, inatarajiwa kuanza kufanya maonyesho jijini Dar es Salaam wiki ijayo.

**Twanga Pepeta**

Tangu jana bendi hii yenye wanamuziki nyota kibao akiwamo Ally Choki, ipo jijini Mwanza ikitoa burudani katika ukumbi wa The Prince Complex.

**Tukuyu Sound Band**

Bendi hii inayoundwa na vijana, kama kawaida yao kila Jumapili humalizia wikiendi katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park Ubungo.

**Kimokimo Band**

Kundi hili ambalo linaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa linatoa burudani ya nguvu katika ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal.

**Waluguru Original**

Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, kila Jumamosi hufanya vitu vyake katika ukumbi wa Terminal Pub Msamvu na Jumapili itakuwa ndani ya ukumbi wa ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya iliogawainyika kutoka Sikinde, lleo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Becah, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Mjengoni Classic Band**


Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi ifanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**The Kilimanjaro Band**

Baada ya kukaa kwa muda mrefu, bendi hii kongwe, kwa sasa inaendelea kujifua huku ikitafuta kumbi ili kuanza kutoa maonyesho kila mwisho wiki.

**Maina Band**

Bendi hii inayomilikiwa na mwimbaji wa siku nyingi Liston Maina, jana ilitoa burudani katika ukumbi wa Hekima Garden Mikocbeni B, leo Jumamosi itakuwa ndani ya ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.



# KAPOROMOKA KWA KASI

## MASHABIKI WATEMBEZA KIKAPU KUMCHANGIA

NI kama mzaha vile, lakini ni jambo la kweli limetokea tena kwa msanii nyota wa Marekani Kanye West, baada ya kupoteza utajiri wake siku moja mashabiki watembeza kikapu kwa ajili ya kumsaidia.

Tukio hilo lilijitokeza kwenye mitandao ya kijamii baada ya mashabiki wa mwanamuziki huyo anayesifika kwa kutoa kauli zenye utata, walipoanzisha zoezi la kumchagia pesa kwa ajili ya kumrudisha kwenye orodha ya  mabilionea.

Hayo yalianzia kwenye ukurasa mmoja uliopewa jina ''Make Kanye West Billionare Again'' baada ya rapa huyu kupoteza dola bilioni mbili.

Hili lilitokea baada ya utajiri wake kushuka kuanzia mabilioni ya dola hadi dola milioni  400.

Mitandaoni watu walionekana wakihimizwa kutoa machango wao kwenye ukurasa huo wa GoFundMe.

Staa huyu mwenye umri wa mika 45 alipoteza kiasi hicho cha pesa baada ya kupoteza ushirikiano na kampuni ya Adidas.

Kampuni hiyo ilijiengua baada ya kukasirishwa na matamshi yenye chuki ya Kanye West.

Baadaye kampuni zingine kama vile Gap, Footlocker, TJ Maxx, na Balenciaga walifuata nyayo hizo  na kukata uhusiano na rapa huyo huku wakisisitiza  hawana nia ya kufanya kazi na West tena.

Hata hivyo,ukurasa huo uliondolewa kwa kile kilichodaiwa ukiukaji wa sheria na mikakati ya tovuti ingawaje hawakuwa wamechangisha pesa nyingi kabla ya akaunti hiyo kufungwa.

Juhudi za kumfadhili Kanye West hazikuzaa matunda ila zilipata uungwaji mkono mitandaoni kwani wengi walisambaza habari hiyo.



# Davido aendelea kuliwazwa

WASANII mbalimbali duniani wanaendelea kuonyesha hisia zao za majonzi baada ya kifo cha mtoto wa mwanamuziki nyota Afrika, Davido.

Mwanamuziki, Wizkid amefuta matangazo yote

Yanayohusu albamu yake mpya, kama ishara ya kuomboleza.

Albamu hiyo inayoitwa "More Love, Less Ego" ilipaswa kutolewa Novemba 4, 2022, lakini Wizkid aliifuta na kueleza atatangaza baadae siku iyakayozinduliwa.



## Hakuna kuacha kitu Desiigner

WAPENZI wa muziki wa Hiphop nchini Marekani, wamemuomba msanii nyota, Desiner kuacha kufikiria kuutupa muziki huo, badala yake afanye kazi kwa bidii kama kumuenzi rafiki yake Takeoff.

Rappers wengi wanaamini Takeoff anamchango mkubwa katika mabadiliko ya muziki huo, kifo chake kilichotakana na kupigwa risasi kimeacha pengo kubwa.

Mastaa wengi akina Ja Rule, amesikitishwa na namna tukio la Takeoff kupigwa risasi hasa kutokana mchezo wa kete GAME OF DICE.

Kwa ufupi mchezo wa kete ni aina ya kamari na mastaa wengi nchini Marekani wanajihusisha sana. Mara nyingi michezo ya kete huendeshwa na makundi ya wahuni.

## Pere kama wanakushtukia

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria, Pere amewapa wakati mgumu mashabiki zake baada ya kuwaomba kusali sana, huku akiwatahadharisha dunia ni sehemu mbaya.

Pere alisisitiza kuwa maombi yanaweza kubadilisha ratiba ya matukio mengi kwani maisha ya kiroho yanaweza kumfikia yule anayeshinda matamanio ya mwili.

Kauli ya nyota huyo imechochea hisia tofauti kwa mashabiki zake, baadhi wakimpongeza na wengine wakimpinga na kueleza hayo yanatokana na kuporomoka kwa umaarufu.





## Burna Boy, Fireboy ndani Wakanda Forever

TASNIA ya muziki nchini Nigeria inazidi kuvuka mipaka, baada ya wasanii wanne kuingizwa katika albamu mpya ya wakanda Forever.

Majina ya wasanii waliotajwa kuingizwa katika mradi huo ni Burna Boy, Tems, Fireboy na Ckay ambao nyimbo zao zitakuwa katika albam hiyo ambayo itatoka sambamba na filamu yake ya Black Panther.


Kuchaguliwa kwa wanamuziki hao kunaonyesha jinsi muziki wa Afrobeat unazidi kukua kwa kasi.

## Mke wa Chadwick atoboa ya moyoni

NYOTA wa Black Panther ambaye alifariki Agosti 2020, Chadwick Boseman, imebainika alikuwa katika vita ya kupigania maisha yake kwa miaka minne kutokana na ugonjwa wa saratani ya utumbo.

Akifichua jambo hilo, mke wake Simone Ledward Boseman, ameeleza jinsi vita hiyo ilivyokuwa ngumu na kukatisha tamaa.

Akizungumza na Whoopi Goldberg, katika kipindi cha Good Morning America, amesema tangu mume wake afariki amekuwa akihifadhi urithi wa mumewe na akafichua jinsi anavyoona miaka michache iliyopita kuwa ngumu kwake.



MAKALA

# Mtaalam gwiji na mbinu kukabili changamoto za kilimo cha zabibu

Na Mwandishi Wetu

KILIMO cha zabibu kina mchango mkubwa kwa pato la taifa licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Hivi karibuni Mwandishi Wetu alifanya mahojiano na Archard Kato, mmiliki wa kampuni ya Alko Vintages ya kutengeneza mvinyo jijini Dodoma.

Kato, amekuwa kwenye sekta ndogo ya zabibu kwa miaka zaidi ya 30, kama mtafiti kwenye Kituo cha Utafiti wa Zabibu (TARI Makutupora); mhandisi michakato na mtaalamu msindika mvinyo. Pamoja na mambo mengine, anazungumzia jinsi ya kuvuka changamoto zinazokabili zabibu na mnyororo wake wa thamani kama ifuatavyo.

**SWALI**: Inawezekana hakuna aliyedumu kwenye kilimo na sekta ndogo ya zabibu kama wewe. Unakitathmini vipi kilimo cha zabibu na mnyororo wake wote wa thamani?

**JIBU:** Nikiangalia kilimo cha zabibu naona kinakwenda vizuri. Kina changamoto nyingi, kina vikwazo kama ilivyo mazao mengine. Changamoto hizo zitapungua kwa kadri tutakavyokuwa tunafanya kwa pamoja na serikali. Muhimu zaidi ni tuelewe vikwazo ni nini, lakini wakati mwingine watu wajielemishe waijue zabibu vizuri. Siku hizi tuna simu janja. Huko kuna maarifa mengi. Watu waende huko kuongeza uelewa juu ya zabibu.

**SWALI:** Watengenezaji wengi wa wine wanaoibukia wanatumia mapipa, maarufu kama sim tank. Mapipa haya hayapunguzi ubora wa kinywaji?

**JIBU**: Kuna wanaoamini kwamba labda kutengenezea wine kwenye sim tank kunaiathiri. Hapana. Inategemea soko na soko.

Unapokuwa unataka kwenda soko la nje ambalo lina tahadhari kubwa, lazima utazame mahitaji yake. Vinginevyo, kutengenezea kwenye sim tank haina maana kwamba wine hiyo ni mbaya, kwamba haifai. Kuna watu wana dhana kwamba mvinyo wa kwenye sim tank haufai. La hasha.

Kwamba kama hili jambo linafanyika mahali fulani wanafikiri kwamba halifai. Hapana. Ni suala kwamba kila mtu ana namna na mahali pa kuanzia.

Hata sisi tulianzia kwenye sim tank, leo tunatengenezea kwenye matanki yasiyoshika kutu na kwenye makasiki ya mbao, lakini tulianzia kwenye sim tank.

Kwa hiyo, nafikiri hizi sim tank ziendelee kutusaidia mpaka watu watakapoboresha kufikia hatua iliyo bora zaidi. Itategemea watu wanataka kufikia masoko ya mbali kiasi gani na kuuza kiwango kikubwa zaidi.

**SWALI:** Wakulima wanataja sana changamoto ya masoko. Wameitika mwito, wameboresha mashamba yao na mavuno yamekuwa makubwa, soko limefurika, hakuna pa kuuza zabibu zao. Watatokaje katika mkwamo huo siku zijazo?



**JIBU:** Kwa uzoefu wangu wa miaka zaidi ya 30 katika Sekta ya Zabibu naweza nikasema kwamba mazuri yanakuja. Kuna matarajio mazuri mbele hata kama kuna changamoto nyingi zinazotukabili sasa.

Bahati nzuri kwetu, sasa Wizara ya Kilimo ina mawaziri, Hussein Bashe na naibu wake Anthony Mavunde wanaojitahidi sana. Wamejitahidi sana katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata masoko.

Nimesikia pia kutoka serikalini kwamba karibuni kuna kiwanda kitaanzishwa cha kuchakata zabibu. Hii ni hatua nzuri sana.

Lakini pia watu waelewe kwamba zaidi ya asilimia 50, hasa asilimia 60 ya wine inayouzwa duniani huwa ni mchuzi. Wengi hawaelewi kweli hii. Na sisi badala ya kuuza wine ya kwenye chupa, tunaweza kuuza mchuzi kwa nchi za jirani.



Archard Kato

Hiyo itatusaidia kupanua soko kwa manufaa ya wakulima wetu na itakuwa na manufaa kwa watengeneza mvinyo pia na vijana wetu watapata ajira.

Kenya, kwa mfano, hawana wine ya kutosha. Kupitia kwa Shirika lao la Kenya Wines Agency wananunua wine kutoka Afrika Kusini wanafunga kwenye chupa. Uganda na Rwanda hawana fursa hiyo, na DR Congo nao hawana zabibu.

Hapa cha msingi tunahitaji uwezeshaji wa serikali, na hasa, Shirika la Viwango (TBS) liweke viwango vya mchuzi. Kwa sasa TBS lina viwango vya wine ya chupa, wakati umefika waweke viwango vya mchuzi wa zabibu ili tuanze kuuza kwenye masoko ya Afrika Mashariki, tuushindanishe mchuzi wetu na mchuzi unaotoka kwingine kwenye masoko ya nchi za jirani zetu.

Tukifanya hivyo tutakiwa pia tunatumia turufu ya pekee tuliyonayo ya kuwa ni sisi pekee kwa Afrika Mashariki tunaolima zabibu. Tuwezeshe majirani zetu wanunue mchuzi wetu watengeneze wine kwao kama jinsi ambavyo, kwa mfano, Uholanzi na Canada wanavyofungasha wine kwenye chupa kutokana na mchuzi wanaonunua kwa mamilioni ya lita kutoka nchi za Amerika ya Kusini kama Chile, na Afrika Kusini, hata kama wao hawalimi zabibu.

Kwa hiyo na sisi nchi za jirani hizi tunaweza tukafanya hivyo, cha msingi ni kwamba tushirikiane na taasisi za serikali katika hilo jambo kuweza kufikiwa.

**SWALI:** Wakulima na hata watengenezaji wa mvinyo wadogowadogo wanataja pia changamoto ya mitaji, na hasa mikopo kuwa kikwazo kikubwa. Kwamba benki hazitoi uwezeshaji au msukumo wa kutosha?

**JIBU:** Nieleze kidogo. Taasisi zetu za fedha bado ni changa kwa maana ya aina ya bidhaa wanazotoa. Kwamba benki zetu zilizo nyingi ni za biashara, si za uwekezaji. Tulikuwa na TIB na sasa tuna Benki ya Kilimo, lakini hatuzioni kama zinafanya vizuri sana.

Matokeo yake ni kwamba hawa wakulima na wazalishaji wadogo wanapata shida ya mitaji.

Mara nyingi unakuta wanalalamika gharama ya vifaa. Na hasa kutaka kuwa na ubora kwa maana ya teknolojia. Kwamba hawezi kufikia ubora fulani kwa sababu teknolojia wanayoitumia si muafaka hata kama wanauza wine yao.

Tunao wakulima na watengeneza mvinyo ambao wameweza kukopa fedha benki, lakini benki iliwauliza mnamuuzia nani! Mnapeleka wapi!

Kwa hiyo kama wangekuwa wamejiambatanisha na wanunuzi wa mchuzi, kwa mfano, sisi kwa kipindi fulani tuliwaunga mkono baadhi yao. Tulikubaliana kununua mchuzi wao, wakienda benki kuomba mkopo tuseme wa milioni 200 au milioni 300, wakiulizwa wanatutaja, hapo inakuwa rahisi kwa sababu sisi tunawawekea dhamana kwa kuwa tuna makubaliano nao ya kununua mchuzi au zabibu zao.

Cha kufanya wakulima na watengenezaji wadogo wa wine wajiambatanishe na wanunuzi wa mchuzi. Itasaidia kuwadhamini mikopo benki waboreshe uzalishaji wao.

Kingine ni kwamba benki wanahitaji kuona dhamana, kwa hiyo kama kile kidogo wanachokipata na mahesabu yao yanakwenda vizuri, mwaka wa kwanza, na wa pili, waweke vitu vinavyoweza kuthaminishwa kama dhamana ya mkopo.

Nawafahamu baadhi ya wakulima ambao mapato yao ya zabibu yamewawezesha kujenga nyumba za kupangisha. Baada ya muda zile nyumba zinaweza kutumika kama dhamana za mikopo kwa sababu benki wanataka dhamana iwe kitu kisichohamishika. Kwa kufanya hivi baada ya mwaka wa tatu au wa nne, tatizo linaweza kupungua.

# RFB ilivyoleta mageuzi matumizi ya barabara

Na Mwandishi Wetu



MWonekano wa daraja jipya la Kiyegeya linalounganisha mikoa ya Morogoro na Dodoma lililojengwa na serikali kwa kutumia fedha za matengenezo ya dharura kutoka Mfuko wa Barabara baada ya daraja la zamani kusombwa na mafuriko. **PICHA: RFB.**

Mfuko wa Barabara na Bodi yake (Roads Fund Board), vilianza kufanya kazi mwaka 2000 na vilianzishwa kupitia Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta Sura 220. Mfuko na bodi ulianzishwa kama sehemu ya mabadiliko yaliyofanywa na serikali kwenye sekta ya barabara.

Mfuko wa Barabara ulianzishwa ili kuhakikisha uwapo endelevu wa fedha za kugharamia matengenezo ya barabara za kitaifa, yaani barabara kuu na barabara za mikoa na barabara za wilaya kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007. Sheria hii inazihusu barabara za Tanzania Bara.

Azimio la kwanza la uanzishwaji wa mfuko liliitwa "AZIMIO LA KUANZISHA

MFUKO MAALUMU WA FEDHA ZA BARABARA" au "MFUKO WA BARABARA" lilifanyika Agosti 1991 na azimio la pili liliitwa "AZIMIO LA KUANZISHA MFUKO WA BARABARA WA SERIKALI ZA MITAA" ambalo lilifanyika Agosti 1992.

Kuanzishwa kwa tozo katika mafuta ya dizeli na petroli katika Ibara ya 17 ya Sheria ya Hazina na Ukaguzi (Sura ya 439) ambayo inaipa mamlaka Serikali kuanzisha mfuko maalum na kutokana na taratibu za utawala Azimio halikuwa na nguvu ya kisheria hivyo hakukuwa na uwajibikaji katika Azimio, ili kuupa mfuko nguvu ya kisheria na kupata nguvu katika kufadhili matengenezo ya barabara na usimamizi wa mfuko.

Bunge lilifanya marekebisho ya sheria za Barabara (Namba 2) ya mwaka 1998 ambayo ilianzisha Mfuko wa Barabara na Bodi ya Mfuko wa Barabara. Sheria ilifanyiwa marekebisho mwaka 2006 na inatumika kama sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta Sura 220 (iliyofanyiwa marekebisho 2006).

Bodi ilianza kufanya kazi mwaka 2000 katika jengo la TETEX Barabara ya Pamba Dar es salaam. Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Mfuko wa Barabara alikuwa Rose Mang'enya, Philipo A.Magani aliyefuatiwa na Dkt. James Wanyancha. Mwenyekiti wa sasa wa Bodi ya Mfuko wa Barabara ni Joseph O. Haule.

**MAJUKUMU YA BODI**

Kutokana na kifungu cha 5(4) cha Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, majukumu makuu ya Bodi ya Mfuko wa Barabara ni pamoja na; kumshauri Waziri mwenye dhamana ya barabara juu ya vyanzo vipya vya mapato ya mfuko, marekebisho ya viwango vya vyanzo vilivyopo na kanuni za ukusanyaji wa mapato ya mfuko kwa dhumuni la kuhakikisha uwepo wa mapato ya kutosha na endelevu kwa ajili ya shughuli za barabara.

Mkukumu mengine ni kutumia fedha za Mfuko kwa makusudi yaliyoidhinishwa na Bunge, kuweka na kutoa utaratibu utakaotumiwa na wakala wa ukusanyaji mapato ya mfuko, kuhakikisha kuwa mapato yote ya Mfuko yamekusanywa na kupelekwa kwenye akaunti ya Mfuko, kutengeneza au kurekebisha utaratibu wa ugawaji wa fedha za Mfuko na kumshauri waziri mwenye dhamana ya barabara kuhusu utaratibu huo.

Mengine kumshauri waziri mwenye dhamana ya barabara juu ya ugawaji wenye ufanisi wa fedha za mfuko, kugawa fedha za mfuko kwa Wakala wa Barabara, kuhakikisha kuwa shughuli za kiufundi na kifedha za Wakala wa Barabara na mfuko wenyewe zinafanyika kwa ufanisi mkubwa, kufuatilia matumizi ya fedha zilizopelekwa kwa wakala ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na mfuko na kutoa mapendekezo mengine yoyote kwa waziri yatakayoonekana ni muhimu ili kuiwezesha bodi kutimiza malengo yake.

**VYANZO VYA MFUKO**

Tozo ya mafuta ni chanzo kikuu cha mapato ya mfuko kwa kuwa huchangia wastani wa asilimia 97 ya mapato yote ya mfuko. Tozo hiyo ya mafuta ni Sh. 263 kwa kila lita ya petroli na dizeli ambayo mapato yake hukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kuongezeka kwa mapato kutoka chanzo hiki, kunategemea zaidi kukua kwa sekta za kiuchumi ambazo hutegemea zaidi matumizi ya nishati za dizeli na petroli.

Ushuru kwa magari ya kigeni yanayoingia nchini, kwa wastani unachangia asilimia moja ya mapato ya mfuko. Ushuru huu pia hukusanywa na TRA kwenye ofisi za mipakani kwa kufuata sheria ya "The Foreign Vehicles Transit Charges Act CAP 84 (R.E 2006)". Kwa magari yenye ekseli hadi tatu hutozwa dola sita kila kilomita 100 na dola 10 kwa magari yenye ekseli zaidi ya tatu. Mapato kutoka kwenye chanzo hiki yanategemea zaidi hali ya usalama nchini, ufanisi wa bandari na ubora wa barabara.

Chanzo kingine ni fedha zipatikanazo kupitia magari yanayozidisha uzito barabarani, kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya mwaka 2016. Mfuko haukichikulii kama chanzo endelevu kwa kuwa kimewekwa ili kudhibiti uzidishaji wa mizigo kwa magari yanapokuwa barabarani na hivyo mapato yake yanatarajiwa kushuka kadri wasafirishaji watakavyozidi kufuata sheria hiyo. Lengo la chanzo hiki ni kufidia uharibifu halisi wa miundombinu ya barabara uliosababishwa na chombo husika cha usafiri au usafirishaji.

**UFANISI WA MFUKO**

Ili kuongeza ufanisi kwenye ufuatiliaji wa matengenezo na hali ya barabara, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Bodi ya Mfuko wa Barabara imeunda Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji Hali ya Barabara. Mfumo huo ulizinduliwa rasmi Julai, mwaka huu, wakati wa warsha ya kujadili namna ya kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwenye miundombinu ya barabara iliyofanyika jijini Mwanza.

Wakati wa uzinduzi huo uliofanywa na naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Geoffrey Kasekenya, Bodi ya Mfuko wa Barabara iliagizwa kufuatilia na kuhakikisha taarifa na malalamiko yanayotolewa na watumiaji wa barabara yanafanyiwa kazi kwa wakati na Wakala wa Barabara wanaohusika na utengenezaji wa barabara hizo ambao ni TANROADS na TARURA.

"Upatikanaji wa taarifa za hali ya barabara kwa wakati ni moja ya njia muhimu za kutunza miundombinu ya barabara. Naipongeza Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kubuni mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na wananchi na watumia barabara katika kufuatilia na kutoa taarifa kwa vyombo husika juu ya hali ya barabara katika maeneo yao," alipongeza Kasekenya.

Akisoma taarifa yake, Meneja wa Mfuko wa Barabara, Eliud Nyauhenga, alisema kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, Tanzania imeshuhudia uharibifu mkubwa wa mara kwa mara wa miundombinu ya barabara kutokana na mafuriko yanayosababishwa na mvua kubwa zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Aliutaja uharibifu huo kuwa ni pamoja na kusombwa kwa madaraja na makalavati kunakoleta usumbufu na hasara kubwa kwa wasafiri na wasafirishaji na kuisababishia Serikali gharama kubwa za matengenezo.

"Mfano wa karibuni ni kuzolewa kwa daraja la Kiyegeya mwaka 2020 ambako kulisimamisha kwa muda shughuli za usafiri na usafirishaji kupitia barabara ya Morogoro – Dodoma ambayo inatumiwa na mikoa ya kati, Kanda ya Ziwa na nchi jirani kama Rwanda, DRC Congo na Burundi, kutokana na kusombwa kwa daraja hilo, Serikali ililazimika kutumia takribani bilioni 10.89 kujenga daraja jipya na barabara unganishi," alisema.

Meneja Msaidizi Ufundi wa Mfuko wa Barabara, Mhandisi Rashid Kalimbaga, anasema lengo la mfumo mpya wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa hali ya barabara ni kuwashirikisha wananchi na hasa watumiaji wa barabara katika kusimamia na kutunza miundombinu ya barabara ili kuepusha uharibifu wa miundombinu ya barabara unaoweza kusababisha madhara makubwa kwa jamii. Kupitia mfumo huo, taarifa za hali ya barabara kutoka kwa watumiaji wa barabara zitapelekwa kwa mameneja wa TANROADS, TARURA na Bodi ya Mfuko ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa na hatimaye kupeleka mrejesho kwa watoa taarifa.

**MATUMIZI YA MFUMO KIELEKTRONIKI**

Takwimu zinaonyesha kuwa tangu Julai hadi Octoba, 2022 baada ya kuanza kwa matumizi ya mfumo mpya wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa hali ya barabara, malalamiko 7,308 yamepokewa. Kati yua hayo, 1,526 ni kuhusu kuharibika kwa barabara, 953 ni kuhusu mashimo barabarani, 678 ni kukosekana kwa alama za barabarani, 649 ni uchafu kwenye mifereji, 408 ni kuvunjika kwa kalavati pamoja na malalamiko ya aina nyingine.

Hivi sasa wananchi wanaweza kutumia simu-janja kwa kupakua mfumo mpya wa barabara na kutoa taarifa za hali ya barabara au simu za kitochi kutoa taarifa ya hali ya barabara kwa kubofya *152*00# na kufuata maelekezo.

Gharama za kutuma taarifa kwa wanaotumia simu za kitochi au kishikwambi ni bure na wanaotumia simu-janja wenye mitandao ya Airtel na Vodacom kupitia mfumo wa Barabara, wanaweza kutumia mfumo huo bila ya kuwa na kifurushi cha mtandao. Aidha, Mazungumzo yanaendelea ili matumizi ya mfumo wa barabara bila gharama kwa simu- janja yawezeshwe kwa watumiaji wa mitandao mingine.

Joshua Mkelemi, mkazi wa Dodoma ameipongeza serikali kwa kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya

barabara kwa kuwa mfumo huo unawaweka watoa huduma za barabara na wananchi karibu, na hivyo inakuwa rahisi kwa wananchi kutoa malalamiko yao kwa watoa huduma moja kwa moja, ambapo nao wanatakiwa kuyafanyia kazi malalamiko hayo kwa wakati ili kuboresha zaidi huduma hii ya barabara nchini.

**MATUMIZI WATAALAMU**

Sambamba na matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya barabara Mfuko wa Barabara hutumia pia wataalamu wake wa ndani pamoja na wataalamu washauri katika kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa kwa Wakala wa Barabara (TANROADS na TARURA) kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinatumika ipasavyo. Wataalam hao huzungukia miradi iliyopokea fedha za matengenezo ya barabara ili kujiridhisha kuwa thamani ya fedha iliyotolewa inaendana na matengenezo ya barabara yaliyofanyika.

# Ruwasa inapopania 'kuwatua mama ndoo' za maji vijijini

## • Miradi mipya 1,258 yaanzishwa 604 yakamilika

Na Joseph Mwendapole

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), imefanikiwa kuwaondolea adha ya upatikanaji wa maji wananchi wa vijijini ikiwa ni miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019.

Hivi karibuni Mkurugenzi wa usambazaji RUWASA, Bwire Mkama, amezungumzia changamoto, mafanikio na nini mpango mkakati wa kuhakikisha wanafikisha asilimia 100 kwa wananchi waishio maeneo hayo.

Ametoa maelezo hayo wakati wa kikao kazi baina ya wakala na wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Mkurugenzi huyo anaanza kwa kusema kwamba majukumu ya RUWASA ni kupanga, kusanifu, kujenga na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa maji chini ya ardhi, ikiwa ni pamoja na kusafisha visima, kufanya upimaji wa wingi wa maji na ukarabati wa visima.




Baadhi ya visima vya maji vinavyochimbwa kuwakomboa wananchi wa maeneo ya vijijini kutoka kwenye shida ya maji

Anataja majukumu mengine kuwa ni kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa ya aina tofauti, ikiwa ni pamoja na kupima aina ya miamba na udongo kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa na kazi zingine za kihandisi ikiwemo kufuatilia na kutathimini utendaji wa vyombo vya utoaji huduma ngazi ya jamii.

Mhandisi huyo anaeleza wakati wakala inaanzishwa mwaka 2019 asilimia 64, ya wananchi wa maeneo ya vijijini ndiyo ilikuwa ikipata maji safi na salama lakini kufikia Desemba mwaka 2020 idadi hiyo iliongezeka hadi kufikia asilimia 70.

Anasema hadi Juni mwaka huu idadi ya wananchi wa vijijini waliokuwa wakipata maji iliongezeka na kufikia asilimia 74 na kwamba lengo ni kufikia kiwango kilichoainishwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), inayotaka asilimia 85 ya wananchi wa vijijini wawe wamefikiwa na huduma hiyo ifikapo mwaka 2025.

Mhandisi Bwire anasema wakala inatekeleza miradi mingi ambayo mingine inagharamiwa kwa fedha za ndani na mingine mashirika mbalimbali ya kigeni kama mradi wa uboreshaji wa miongozo na mifumo unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Anasema ujenzi wa miundombinu ya maji unafanywa kwa fedha za ruzuku na fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) wakati ujenzi wa miundombinu ya maji, kuimarisha mifumo, kujenga uwezo wa utoaji wa huduma vijijini unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Pia mradi wa ujenzi wa miundombinu ya maji na kujenga uwezo wa utoaji wa huduma vijijini unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Uingereza (UK AID) ambalo kwa sasa linafahamika kama (FCDO).

Mhandisi Bwire anaeleza pamoja na mafanikio yote hayo RUWASA inakabiliwa na upungufu wa watumishi 822 wa kada mbalimbali wakiwemo waendesha mitambo na madereva.

Anasema hadi Oktoba mwaka huu Ruwasa ina jumla ya watumishi 1,660 sawa na asilimia 66.7 ya mahitaji halisi ya watumishi



Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo

2,482, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 822.

Anasisitiza kwamba upungufu wa watumishi hao uko kwenye kada za kimkakati kama vile za ununuzi, uhasibu, ofisa maendeleo ya jamii, waendesha mitambo na madereva.

Anasema pamoja na changamoto hiyo, RUWASA bado inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mipya na iliyorithi kutoka katika halmashauri mbalimbali za Wilaya.

Mhandisi Mkama anasema tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019, RUWASA imerithi miradi 632 kutoka halmashauri hizo ikiwa haijakamlika lakini hadi mwaka huu miradi 607 imeshakamilika ambayo ni sawa na asilimia 96.

Anasema vijiji vinavyonufaika na miradi hiyo ni 1,027 na jumla ya wananchi ambao wanaendelea kunufaika na kukamilika kwa miradi hiyo ni 1,901,854 wakati gharama halisi iliyotumika kutekeleza miradi hiyo imefikia Sh bilioni 154.1.

Mhandisi Bwire anasema RUWASA ilirithi miradi ya maji 177 iliyokamilika lakini ilikuwa haitoi maji, mpaka sasa wamefanikiwa kukamilisha miradi 147 inayotoa maji ambayo ni sawa na asilimia 83.

Anaongeza kwamba vijiji vinavyonufaika na miradi hiyo kwa sasa ni 203 na wananchi 657,264. Gharama iliyotumika kurekebisha miradi hiyo ya maji ni Sh. bilioni 6.2.

Anasema katika kipindi cha miaka mitatu RUWASA imekuwa ikifanya utafiti wa kutafuta maji ardhini, na ilipanga kuchimba visima 1,358 lakini imefanikiwa mpaka sasa kuchimba visima 627, visima vinavyoendelea kusambaza maji ni 435.

Gharama iliyotumika kuchimba visima vyote hivyo ni Sh bilioni 18.8 na kuongezaa kuwa tangu kuanzishwa kwake RUWASA imeshaibua miradi mipya 1,258 ambayo 604 imeshakamilika.

Anasema vijiji vilivyonufaika na visima hivyo ni 1,673 na wananchi ambao wananufaika na maji hayo ni 2,820,180 wakati gharama iliyotumika kuchimba ni Sh bilioni 240.4.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala, Mhandisi Clement Kivegalo anasema ili kuondoa malalamiko ya ucheweshaji wa malipo ya wakandarasi wakala imekuja na teknolojia mpya itakayomwezesha mkandarasi kufuatilia malipo yake kidijitali.

Anasema wanaandaa mfumo huo kwa kushirikiana na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maji na kwamba lengi ni kuondoa ukiritimba na ucheleweshaji wa malipo ya makandarasi.

Aidha, anasema wakala imeamua kuja na mfumo huo baada ya malalamiko ya makandarasi kucheleweshewa malipo yao hali ambayo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji na kusababisha malalamiko ya watu.

Anasema kupitia mfumo huo ambao uko kwenye majaribio, mkandarasi anaweza kuingia kwenye mfumo kupitia simu yake ya mkononi na kuangalia malipo yake yamefikia sehemu gani bila ya kufunga safari kwenda RUWASA au kupiga simu mara kwa mara.

"Tunataka mkandarasi akishakabidhi hati zake za madai RUWASA asilazimike kurudi tena au kupiga simu mara kwa mara. Kupitia mfumo huu ambao tunaufanyia majaribio kwenye mikoa mitano mkandarasi atakuwa na uwezo wa kuchungulia kupitia simu yake malipo yake yako sehemu gani," anasema

Anasema wamemua kufanya hivyo ili kuweka uwajibikaji kwa watumishi wa wakala wanaohusika na malipo kubaini atakayezembea kufanya malipo hayo kwa wakati uliopangwa aweze kuwajibishwa na kutoa maelezo kwanini ameshindwa kutimiza wajibu wake.

"Huu utaratibu wa mtu kuamua amlipe nani na wakati gani ni ukiritimba ambao unasababisha hisia za rushwa na umeleta malalamiko mengi, lakini sasa mwarobaini wa haya yote ni mfumo huu mpya kwa sababu mhusika hatalazimika amwone mtu ana kwa ana ndipo amlipe," anasisitiza.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Sikukuu bila nguo mpya hapatoshi enzi hizo

**Na Adam Fungamwango**

## • Watoto wanaulizana, waliowahi kununuliwa ni kama siku haziendi



"DOLI Doli, nimenunuliwa nguo ya sikukuu na viatu." Ni wimbo ambao utakuwa unaimbwa kwa mbwembwe na mmoja kati ya watoto ambaye wazazi wake wamemnunulia nguo ya sikukuu.

Anaweza kuangaliwa jicho baya au kununiwa na watoto wenzake ambao wao mpaka muda huo kwao 'bila bila' yaani hata wazo la kununuliwa bado.

Angalau kwa mbali anaweza kusapotiwa na wale ambao wazazi wake wamewaambia wasubiri mwisho wa mwezi huu.

"Na sisi baba kasema atatununulia. Tena kasema na viatu vizuri kushinda hata vya kwako." Mmoja atampa jibu hilo.

Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya zamani watoto kinapokuja kipindi kama hiki kuelekea kwenye sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Ni kipindi ambacho wazazi wa zamani walikuwa kwenye pilikapilika ya aina yake kutafuta pesa kwa ajili ya kuwanunulia watoto nguo za sikukuu, pamoja na kula chakula kizuri siku hiyo.

Kuna wakati mzazi hata kama hana pesa, lakini atalazimika kujitutumua kwa ajili tu ya kutowafanya watoto wake wajisikie vibaya siku hiyo.

Tatizo kwa watoto ni kwamba watanunuliwa lini, ndilo lililokuwa linawasumbua. Wakiona wenzao wamenunuliwa wao bado basi roho juu.

Kwa wakati huo mama ndiyo atasumbuliwa zaidi na watoto, akiulizwa maswali ya kwa nini mpaka siku hiyo bado tu hawajanunuliwa.

Nasema wakati huo kinamama walikuwa wakisumbuliwa zaidi kwa sababu, kwenye miaka ya 1990 kurudi nyuma kulikuwa aina tofauti ya akinababa na wa sasa. Wa siku hizo ni wanademokrasia.

Miaka hiyo hakuna mtoto yoyote hata akili yake tu imtume asimame mbele ya baba yake amuulize ni kwa nini mpaka wakati huo hawajanunuliwa nguo za sikukuu. Kitakachompata kwenyewe atasimulia.

Sasa ukute kipindi kama hiki mtoto amekuwa wa 30 shuleni au wa pili kutoka mwisho, baba anagoma kabisa kununua nguo. Anasema hawezi kumnunulia nguo mtoto ambaye 'hana akili' darasani.

Kwa bahati mbaya sana, nimesema kina baba wa zamani walikuwa wakisema wamesema. Ni kweli hatomnunulia mtoto ambaye hakufanya vema darasani. Atanunua tu kwa yule ambaye amefanya vizuri.

Hapo sasa jukumu la kununua nguo kwa waliobaki linabaki kwa mama. Ni kinamama tu ndiyo waliokuwa hawakubali kuona mtoto au baadhi ya watoto wake hawajapata nguo za sikukuu kwa sababu tu hawajafanya vema shuleni.



Atabania pesa ya kula anayoachiwa, atakopa au kuazima, ili mradi tu arekebishe hilo tatizo. Halafu akishanunua ndiyo mtoto atakoromewa kuwa asiwe mvivu wa shule, awaige wenzake, na atatishiwa kuwa mwakani au sikukuu ijayo hatununuliwa tena kama akiendelea kuwa 'kichwa maji'.

Twende kwa wale ambao watanunuliwa mapema nguo za sikukuu. Hao ni wale wanaonunuliwa kama mwezi huu wa Novemba yaani nguo tayari zipo sandukuni.

Pamoja na kwamba wana uhakika, lakini hawa nao utawaonea huruma. Yaani safari za kwenda sandukuni haziishi. Atafungua ataiangalia mara tatu tatu, atafunga. Atarudi tena ataviangalia viatu. Wakati mwingine atavijaribu. Na nguo atavaa na kujiangalia alivyopendeza. Anatamani sikukuu iwe hata kesho, siku wanaona haziendi. Anataka siku hiyo ifike upesi ili avae apendeze akawakosoe wenzake.

Hali hii wakati mwingine inasababisha ugomvi na mama. Yeye anakuwa ameshazipiga pasi na kuzikunja vizuri, ameshaweka na kidonge cha dawa ya mende, halafu tena kuna mtu anakwenda kufunguafungua.

Ingawa hili lipo kwa miaka ya sasa, lakini siyo kama ilivyokuwa enzi zile. Ni kwa sababu miaka ya leo, mtoto anaweza kuvaa nguo za zamani na mwingine akavaa nguo mpya wala mtu asijue zipi mpya na zipi za zamani.

Sababu kubwa ya kipindi kile watoto kuhitaji zaidi nguo za sikukuu kwa sababu kulikuwa na uhaba wa nguo. Pia hawakuruhusiwa kuvaa nguo zinazoonyesha kuwa ni bora. Hizo ziliwekwa kwa ajili ya safari, kanisani, au sherehe za kijamii. Kuna nguo fulani hivi ambazo kinamama walikuwa wamezirasimisha kama ni za watoto wao za kushindia nyumbani tu. Hata hizo za sikukuu ikishamalizika, hazikuruhusiwa tena kuvaliwa mpaka siku maalum kama hizo nilizozitaja mwanzo.

Wazazi au kinamama wa sasa wanawapiga watoto zao 'pamba' za nguvu hata wakiwa tu nyumbani. Halafu watoto wa kisasa si watundu sana kama wa zamani. Zamani unaweza baadaye kumkuta yupo kifua wazi na shati keshapoteza huko alikokwenda kucheza mpira wa wenzake.

Kuwepo kwa nguo nyingi zenye ubora unaofanana umefanya kusiwepo sana mahitaji ya lazima ya watoto kununuliwa nguo za sikukuu. Mtoto anaweza kuwa alinunuliwa tu nguo mwezi uliopita na hiyo hiyo akaitumia kwenye sikukuu ikawa haitofautiani na ya wenzake walionunuliwa kwa ajili hiyo.

Nitaweka meseji chache za wadau waliochangia hili kwenye mtandao wa kijamii.

"Nakumbuka nilinunuliwa suruali nisiyoipenda nililia toka nyumbani hadi kanisani, tuliporudi ikabidi wazazi waende tena dukani kunichukulia suruali ya mchele mchele ndiyo nikanyamaza," alikumbuka mdau mmoja kilichomtokea miaka mingi nyuma akiwa mtoto.

"Hili suala limenikumbusha enzi za utotoni. Kweli ilikuwa raha sana. Mkiwa mnacheza mnaulizana vipi nyie mmeshanunuliwa nguo za sikukuu? Watoto ambao wazazi wao wanachelewa kununua huwa wanakosa raha kabisa. Siku hizi sipendi kabisa kuzoesha watoto wangu hiyo tabia," aliandika mwingine.

"Mkuu kwa kweli nakumbuka wakati tukiwa wadogo kwetu kijiji kuna nguo ilikuwa huwezi kuvaa mpaka usafiri. Sisi tulikuwa na nguo za kuvaa tukienda Dar es Salaam tu. Kwa sasa kila nikikumbuka natabasamu tu." Mdau mwingine akachangia.

**Tuma meseji 0716 350534.**

# Rais Tshisekedi ahimiza umma kuingia vitani

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amewataka raia kujiunga katika mapambano dhidi ya nchi ya Rwanda.

Katika hotuba yake kwa taifa Alhamisi jioni, Felix Tshisekedi alitoa wito wa uhamasishaji wa umma kwa raia katika kukabiliana na vita dhidi ya waasi wa M23, wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda.

"Hii ni fursa ya kuwaonya wasaliti wote, raia, wanajeshi wengine wenye nia mbaya wanaotumikia masilahi ya adui. Watakutana na ukali wa sheria, na adhabu ya haki ambayo aina hii ya tabia haistahili". Alisema Tshisekedi.

Aliongeza kuwa vitendo vya Rwanda havikubaliki.

"Vita vilivyowekwa juu yetu na majirani zetu vinadai majibu kutoka kwa kila mmoja wetu, sasa ni wakati wa kunyamazisha tofauti zetu za kisiasa."Felix Tshisekedi alisema.

Katika hotuba hiyo Tshisekedi aliwataka vijana pia kuunga mkono juhudi za jeshi.

"Kujipanga katika kikundi cha umakini ili kusaidia, kuandamana na kuunga mkono" alisisitiza.

Rwanda imekua ikikanusha kuhusika na mzozo huo.

Rais Tshisekedi aliongeza kuwa juhudi za kidiplomasia za kupunguza mvutano kati yake na Rwanda hazikufaulu. Mara kwa mara aliishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23, ambao wamehusika katika mfululizo wa mapigano na jeshi la Congo tangu mwezi Mei.

Mshauri wa usalama wa Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alisema kuwa nchi yake haiwezi kuingia kwenye vita na DRC.

"Rwanda haiwezi kwenda vitani kwa sababu Wakongo wanarusha mawe mpakani au kuchoma bendera. Tunapigana vita vya kimkakati, sio vita vya uchochezi". Alisema Jenerali James Kabarebe. **BBC**



Papa Francis (kushoto) akizungumza na Mfalme wa Bahrain Hamad bin Isa al-Khalifa (kulia) wakati wa mkutano wao , kusini mwa mji mkuu wa Bahrain jana. **PICHA: AFP**

# Watu milioni 4.5 wakosa umeme Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ameishutumu Russia kwa kufanya kile alichokiita ugaidi wa nishati katika mashambulizi yanayofanyika kila siku.

Hata hivyo, wanajeshi wa Russia inaelezwa wanaendelea kupata mafanikio machache kwenye uwanja wa vita.

Zelensky alisema watu milioni 4.5 hawakuwa na umeme kufuatia mashambulizi kwenye mtandao wake wa nishati.

Katika wiki za hivi karibuni, Russia imefanya mashambulizi makubwa ya makombora na ndege zisizo na rubani kwenye vituo vya nishati ya Ukraine.

Mashambulizi hayo yanakuja huku maofisa wakisema kuwa wanajeshi wa Russia huenda wakaondoka katika mji muhimu wa kusini wa Kherson.

Baada ya kupata kushindwa kwa mfululizo katika uwanja wa vita, Russia imeongeza mashambulizi katika wiki za hivi karibuni kwenye miundombinu ya umeme katika miji iliyo mbali na mstari wa mbele.

Katika mwezi uliopita tu, theluthi moja ya vituo vya umeme nchini humo vimeripotiwa kuharibiwa, kulingana na Rais Zelensky.

Serikali ya Ukraine imelazimika kuwasihi wakazi kujaribu kutumia nishati kidogo kutokana na tatizo hilo.

"Usiku wa leo, watumiaji wapatao milioni 4.5 wamekatwa kwa muda katika matumizi ya nishati," alisema Rais Zelensky.

Wakati huo huo, mkuu wa jimbo la Dnepropetrovsk, Valentin Reznichenko alisema kwamba siku ya Ijumaa, mifumo ya kulinda anga ya Ukraine iliangusha ndege nane zisizo na rubani za shaheed, katika jimbo la Dnepropetrovsk .

Kulingana na Reznichenko, ndege zote ziliangushwa katika eneo la Nikopol.

Hakujakuwa na ripoti za mashambulizi ya ndege zisizo na rubani katika maeneo mengine ya Ukraine kuanzia jana jioni.

**BBC**

## Marubani Kenya waanza mgomo

**NAIROBI,** KENYA

MARUBANI katika shirika la ndege la Kenya, KQ wamepanga kuingia katika mgomo leo na kusababisha baadhi ya safari kukatishwa.

Maofisa wa muungano wa wafanyakazi walitangaza mgomo huo, siku moja baada ya notisi ya kutekelezwa kutolewa na muungano wa marubani ambao wanalitaka shirika hilo kurejesha michango kwa hazina yao ya kustaafu.

Katika taarifa hiyo, Chama cha Marubani wa Mashirika ya Ndege ya Kenya (KALPA) kilisema wanachama wao hawataripoti kazini katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi kuanzia leo saa kumi na mbili asubuhi saa za Kenya.

Huu ni uwanja wa ndege mkubwa zaidi nchini humo, na ni uwanja wa ndege wa nne kwa shughuli nyingi zaidi barani Afrika.

"Hatua za Usimamizi wa Kenya Airways zimetuacha bila chaguo lingine," ilisema taarifa hiyo iliyotiwa saini na katibu mkuu Murithi Nyagah.

Notisi ya mgomo wa siku 14 ya chama hicho ilimalizika Jumatano, lakini shughuli katika shirika la ndege zilibaki bila kukatizwa hadi Alhamisi.

Maofisa wa shirika la ndege la Kenya Airways bado hawajajibu wito wa mgomo huo.

Mapema wiki hii, kampuni hiyo ilisema haiwezi kurejesha michango ya hazina ya ruzuku ya marubani hadi 2023. **BBC**

## Imran Khan apata nafuu, baada ya kupigwa risasi

**ISLAMABAD,** PAKISTAN

Waziri mkuu wa zamani wa Pakistan Imran Khan, anaendelea kupata matibabu hospitalini baada ya kupigwa risasi mguuni juzi.

Mtu mmoja aliuawa na wengine 10 walijeruhiwa katika shambulizi hilo lililoulenga msafara uliokuwa ukitembea taratibu katika mji wa Wazirabad ulio umbali wa kilomita zipatazo 170 mashariki mwa mji mkuu, wa Pakistan, Islamabad.

Wafuasi wa kiongozi huyo aliyetimuliwa madarakani mwezi Aprili, waliapa kuendelea na msafara huo unaoshinikiza kuitishwa wa uchaguzi wa mapema. Daktari wa Imran Khan, Faisal Sultan, alisema mwanasiasa huyo yuko katika hali njema na anaweza kuruhusiwa kuondoka hospitalini wakati wowote.

Maofisa wa chama cha Khan cha Pakistan Tahreek-e-Insaf, PTI, wameitisha maandamano makubwa ya wafuasi wa chama hicho nchini kote.

Kufuatia taarifa za kushambuliwa kwa Khan hapo juzi, waandamanaji waliwasha moto na kuziba barabara katika miji kadhaa ya Pakistan. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAM N. SANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0819-0026** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIBAO SECONDARY SCHOOL mwaka 2008 . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIG/RB/430799/2022**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**GRACE FOCUS SHAYO** anatangaza kupotelewa na passport yenye **No. 240517** iliyotolewa 21 September, 2007 na kuisha 20 September, 2017. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DSM/PHQ/RB/378524/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**RAJABU SAMSON SAMA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2007-0094** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIKUBIJI SECONDARY SCHOOL mwaka 2019 Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa : **DAR/MBA/RB/427228/2022** na RESULT SLIP ya kidato cha sita chenye index namba **S0554-0593** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia NGUDU HIGH SCHOOL mwaka 2022, kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .Polisi taarifa: **DAR/MBA/RB/427238/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIOUF PETER MARTINE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5042/0086** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MUNGU BARIKI SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **KAG/KAY/RB/415526/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MESHACK NATHANAEL MESHACK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3490-0111** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST BAKANJA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018 . Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**KIG/KIB/RB/421811/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha BUGURUNI Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 11/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE C/O GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa BEAKA INTERNATIONAL TRANSPORT LTD**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa BEAKA INTERNATIONAL TRANSPORT LTD**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 11 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha BUGURUNI Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 43/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE t/a GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa SAMWEL SWAI NA GEMINII SAM ENTER**

**KUITWA SHAURINI MDAIW**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa SAMWEL SWAI NA GEMINI SAM ENTER**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3mwezi 11 2022

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 873 OF 2022**

**In the matter of the Estate of the late**
**KATABANIA LUTAMIGWA**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**MARY KALABO KANALUANDA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **8 day of NOVEMBER 2022**

**DATED AT DAR ES SALAAM this 23rd day of September 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**FADHILI MSAFIRI SWILA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 625 BXB.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI

**MBE/MBE/RB/352443/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWINGA MANGWANGI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 778 AHB.** Chassis namba **VW2ZZZZ25ZKG006287.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/430031/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha ILALA Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 12/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE C/O GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa 1.MOHABAN TRADING 2 FARMING LTD**

**2.PHILEMON O MOLLEL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa 1. MOHABAN TRADING 2 FARMING LTD**
**2. PHILEMON O MOLLEL**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 11 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha BUGURUNI Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 47/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE C/O GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa NISTRY KALOMGOTI NA RUBBER MASTERS GENERAL SUPPLIES**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa NISTRY KALOMGOTI NA RUBBER MASTERS GENERAL SUPPLIES**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 11 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha BUGURUNI Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 09/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE C/O GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa 1.PLASTIC SUPER MARKET**
**2.MOIZ G NAMABHAI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa 1. PLASTIC SUPER MARKET**
**2. MOIZ G NAMABHAI**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 11 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ILALA**

**Kituo cha BUGURUNI Mkoa D'SALAAM**

**Shauri la madai 10/2022**

**Jina mdai NAS TYRE SERVICE C/O GILBERT MUSHI**

**Jina la mdaiwa SECURE MOBILE SOLUTION**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa SECURE MOBILE SOLUTION**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazmia kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea .

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hi imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 11 2022

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-4

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Wakati huo ulisikika muungurumo wa bodaboda ambayo ilikata kona ghafla. Kwa bahati mbaya, Adel na Mary aliposimama ilikuwa ni karibu na kona hiyo.

Mwendeshaji alikata kona kwa kasi na akili yake haikumtuma wala kudhani kama anaweza kukutana na watu au watoto kwenye kona.

Ilipokata tu ilielekea kwa Mary. Alikuwa ameshika kikapu. Adel tayari alihisi hatari. Tayari dereva wa bodaboda alianza kuhamanika baada ya kuona kuna watu na kwa spidi aliyonayo hawezi kusimama.

Kitendo hicho bila kuchelewa, Adel ambaye alisimama kando kidogo na Mary, alisogea hatua moja kubwa, akamshika mkono Mary kwa nguvu na kumvuta kule alipo.

Ni kati kati huyo, bodaboda aipita pale aliposimama Mary, lakini dereva alikuwa ameshaanza kuyumba baada ya kukuta kuna watu kwenye kona. Dereva na bodaboda yake alianguka kwenye kichaka karibu na mti wa mkorosho.

Nguvu ya mkono wa Adel ilimvuta Mary hadi alikosa balansi na kutokana na tishio la kugongwa alipatwa na mshtuko, kiasi cha kuzuiwa kifuani.

Adel alipomvuta na kuhakikisha bodaboda imepita bila kumgonga alitumia mguu wake wa kushoto kutitia chini ili kuupa mwili nguvu ya kumzuia Mary asianguke. Badala yake alitegesha kifua chake, mwili wa msichana huyo akatua kifuani mwake.

"Mungu wangu." Ilikuwa ni sauti ya binti huyo.

"Usiogope,umeshapona."Akajibiwa.

Kikapu kilikuwa kimeanguka hatua kadhaa kutoka walipo.

Wote wawili walikuwa wakihema kwa nguvu kutokana na tukio la ghafla lililotokea. Kwa sababu walikuwa wameegemeana na kila mmoja mikono kumkumbatia mwenzake kwa ajili ya kujibalansi walianguke, kila mmoja alisikia mapigo ya moyo ya mwenzake vizuri zaidi.

Wakaangaliana machoni kwa sekunde kadhaa, halafu kila mmoja akayatoa kwa aibu.

"Kikapu chako kile kule." Adel alikuwa wa kwanza kuzungumza.

"Kikapu si muhimu, muhimu ni afya na uhai wetu. Tushukuru Mungu tumepona."

Ni wakati huo huo waliongozana hatua kadhaa, Adel aliokota kikapu,




**"Nenda nyumbani, jioni nitakuja nikuone unaendeleaje."**

Mary akawa anaokota vitu vilivyokuwa ndani yake ambavyo vilikuwa vimemwagika na kusambaa. Zilikuwa ni mboga za majani pamoja na viungo vya chakula ambavyo alikuwa ametoka kununua sokoni.

"Nashukuru sana mgeni kwa kuniokoa, muda huu kama nisingekuwa marehemu, basi ningekuwa mlemavu."

"Siyo kwamba nilaumiwe mimi kwa kukusimamisha pale kwenye kona hadi kuhatarisha usalama wako?"

"Mmmh, usiseme hivyo, ajali ni popote na haina kinga, inawezekana tungekuwa tumepishana pale, halafu huko huko mbele angenikuta na kunigonga. Wakati huo wewe haupo."

Adel alitabasamu. Mbali na urembo msichana alijaliwa pia hekima mbali na umri wake mdogo.

"Inawezekana, pole sana, basi kwa sasa nenda nyumbani, jioni nitakuja nikuone unaendeleaje."

Mary alitabasamu tena na kuangua kicheko laini.

"Hapana usije."

"Kwa nini, unamuogopa shemeji?"

"Nitakuja mwenyewe."

"Unapajua nilipofikia?"

"Wewe si mgeni wa kwa kina bibi Anna Msafiri?"

"Ndiyo."

"Basi nitakuja, ila wewe usije kabisa nyumbani."

*************************************

Hakupata japo lepe la usingizi. Alikuwa akimuaza Mary. lile tukio lililotokea mchana ni kama lilikuwa linajirudia tena kichwani mwake. Halafu akajishangaa na kujiuliza ni kweli alikuwa yeye nyakati za mchana alikutana na msichana huyo na kuwa naye na dakika zaidi ya 30? Alionekana ni zaidi ya msichana.

Kitu kilichomkwaza na kuonekana kuwaza sana ni kutofika nyumbani jioni hiyo kama alivyoahidi.

"Nenda nyumbani, jioni nitakuja nikuone unaendeleaje."

"Hapana usije. Nitakuja mwenyewe. Wewe si mgeni wa kwa kina bibi Anna Msafiri? Basi nitakuja, ila wewe usije kabisa nyumbani." Ni maneno yaliyojirudia kichwani mwa Adel yaliyozungumzwa na Mary. Jioni imepita lakini hakutokea.

Jambo la kwanza lililomjia ni kuachwa kwenye mataa. Kumpenda au kutompenda lilikuwa ni jambo la mbele sana, lakini kwanza alichotaka ni kuwa karibu na msichana yule. Kutofika kwake kulionekana kama kumemkwaza. Angeweza kwenda, lakini kwa kuwa ameshaambiwa asiende, kitendo cha kufanya hivyo kingeonyesha kuwa si mkweli, si mwaminifu na ingeweza kuwa sababu ya kuanza kumtilia shaka wakati huu kwake ndiyo muda wa kuanza kubembeleza.

Kama mwanaume hata hivyo aliendelea kuwaza. "Au amekosa nafasi? Kwa nini amenisisitizia kuwa nisiende kwao? Kuna nini? Hataki wazazi kuwatia aibu wazazi wake kuonekana ameanza tabia ya kuwaletea wanaume wasiotambulika nyumbani? Au ana mwanaume mwingine kwa hiyo hataki ionekane kachukua tena mwingine na kuleta ugomvi? Inawezekana kimoja kati ya hiki ndiyo jibu kamili. Lakini ni lipi?" Aliendelea kujihoji mwenyewe.

Picha ya Mary ilimjia vizuri kichwani. "Aisee ni kasichana karembo kweli." Akajisemea.

Adel hakuwa mbali na ukweli. Mary ndiyo alikuwa kama malkia wa kijiji. Kila mwanaume alimhitaji. Lakini Mosha Usonzo alionekana kumhitaji zaidi. Na yeye ndiye aliyesababisha wanaume wote kijiji wamuogope kumsogelea.

Usonzo naye alikuwa amechelewa, kwani tayari alikuwa ni mpenzi na mchumba wa Enock, kijana mmoja kijijini hapo.

Alikuwa msichana mrembo kweli ambaye kila mwanaume anayepishana naye ni lazima ageuke kumungalia na kukiri kuwa katika maisha yake hakuwahi kukutana na msichana mrembo kama huyo.

Sura yake ilikuwa ya mviringo, mashavu yake yalikuwa na vishimo ambavyo hujulikana sana kama 'dimpozi' hasa anapocheka.

Mdomo, macho yake ya duara, pua ni baadhi ya vitu vingine vilivyowafanya wanaume wengi kuchanganyikiwa.

Alikuwa ni mwembamba, lakini hipsi zake zilitengeneza daraja katikati kiasi cha kuonekana kama mcheza sinema maarufu duniani.

Anapotembea mwendo wake unakuwa kama mwanamitindo hivi. Ngozi yake maji ya kunde na ya kuvutia na kung'aa, lakini pia anapocheka meno yake yalionekana kujipanga vema kama punje za mahindi zilizojaa kwenye bunzi lake.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# WIZARA YAIPA SIKU 14 BMT MATUMIZI DAWA MICHEZONI

**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni Sanaa na michezo imetoa siku 14 kwa Baraza la Michezo la Taifa BMT na Kamati ya kupambana na matumizi ya dawa za kusisimua mwili kuwasilisha nyaraka za kukamilisha rasimu ya kupambana na mbinu haramu michezoni.

Akizungumza wakati wa kufunga semina ya siku nne iliyokuwa imegawanyika katika makundi mawili yenye washiriki 150 kutoka vyama vya michezo wadau, wachezaji, viongozi kutoka Baraza la Michezo la Taifa, Katibu Mkuu, Hassan Abbas, alisema kipindi hiki ambacho Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akiwekeza mabilioni kwenye michezo sio ya kukosea.

Abbas alisema anaipa siku tatu kamati ya kupambana na mbinu haramu michezoni kuhakikisha wanawasilisha nyaraka za madeni ya Regional Antidoping Organization (RADO) na World Ant doping Agency (WADA) ambazo ni madeni ya nyuma. Katika hatua nyingine kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohamed Makame, amekuja jijini kwenye ziara ya siku tatu kwa ajili ya kukutana na viongozi wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) pamoja na viongozi wa idara ili kujifunza jinsi ya kuendesha mchezo ngumi visiwani humo.

Alisema lengo la kuja hapa nchini ni kwa ajili ya kupata uzoefu kubadilishana mawazo na wenzetu wa huku hususani katika mchezo wa ngumi.

"Ikumbukwe Zanzibar imekuwa ikikatazwa kwa muda mrefu kujihusisha na mchezo wa ngumi hasa masumbwi lakini mwaka huu Baraza la wawakilishi limeruhusu sasa mchezo huu uanze kuchezwa rasmi hivi sasa tuko kwenye mchakato wa kuanza usajili wa vilabu na mashirikisho yake,"

"Tumeona ni vyema tuje huku kubadilishana mawazo na kupata uzoefu zaidi siku hizi mbili tatu tuweze kukutana nao wote ili tuone nini watatumbia kuhusu michezo hii " alisema Makame.

Alisema pia wamekuja kuangalia changamoto wanazo kumbana nazo ili wajue jinsi ya kuzikabili lakini pia wanataka tuone miundombinu ya michezo hii.

"Tunataka tukutane na vyama vya waamuzi , mashirikisho , mapromota na kamisheni za ngumi za wazi zinazosimamiwa na OBFT na zile za kulipwa zinazosimamiwa na TPBRC ili kujifunza zaidi kutoka kwao," alisema Makame.




Mwanamuziki nyota wa kizazi kipya, Omary Ally Mwanga, maarufu kama Marioo, (katikati) akizungumza wakati wa hafla ya kumtangaza rasmi kama Balozi wa kampuni ya michezo ya kubashiri ya Parimatch jijini Dar es Salaam juzi. Wengine kuanzia kushoto waliokaa ni Afisa Habari wa Parimatch, Ismael Mohamed, Mtayarishaji wa Muziki, Abbah, Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Bahati Nasibu, Emmanuel Ndaki, na Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania Erick Gerald. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Tamasha la Muziki kukutanisha wadau wa kimataifa*

**Na Faustine Feliciane**

TAMASHA kubwa la Muziki linalotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili kuanzia Novemba 24-26 mwaka huu linatarajiwa kuwakutanisha wasanii wa hapa nchini na wadau wa Muziki wa kimataifa.

Tamasha hilo linalosimamiwa na taasisi ya kimataifa ya 'Music in Afrika,' linatarajiwa kukutanisha wasanii 60 kutoka hapa nchini na nje ya nchi huku pia makampuni makubwa ya kurekodi Muziki yakishiriki kwenye tamasha hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Hassan Abassi, alisema tamasha hilo kufanyika hapa nchini ni fursa kubwa kwa wasanii wa ndani ambao watajitangaza na kupata nafasi ya kubadilishana uwezo na wadau wengine.

Aidha, alisema kufanyika kwa tamasha hilo la 'Acces' ni matokeo chanya ya filamu ya Royal Tour inayoitangaza Tanzania kimataifa.

"Serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa tamasha hili pamoja na shughuli zake ikiwa ni pamoja na makongamano na mikutano itakayotangulia kufanyika kabla ya tamasha lenyewe, wasanii wa hapa nchini hii ni fursa kubwa kujitangaza, kuna makampuni makubwa ya kurekodi Muziki yatakuwepo hapa, lakini pia watu wenye uwelewa mkubwa wa Muziki watakuwepo hapa nchini, wasanii wachangamkie hii fursa kwa kujiandikisha kushiriki," alisema Dk Abassi.

Aidha, alisema kuwa Tanzania imekuwa nchi ya tano Afrika kuwa mwenyeji wa tamasha hilo ambalo limeshafanyika pia kwenye nchi za Senegal, Ghana, Kenya na Afrika Kusini. Alisema Tanzania kuna wasanii maarufu lakini hawanufaiki na umaarufu wao kwa sababu ya kushindwa kujisimamia na kujiendesha kibiashara.

"Wasanii maarufu tunao wengi lakini hawana hela, yaani umaarufu wao hauwasaidii kujiingizia kipato kwa sababu ya kushindwa kujiendesha kibiashara, tamasha hili sasa linawaleta watu nguli kwenye Muziki, kama wasanii watajitokeza kwa wingi na kuungana nao naamini wakitoka hapo hawatakuwa kama walivyo sasa," alisema Dk Abassi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa taasisi ya Music in Afrika, kutoka Afrika Kusini, Eddy Hatiye alisema kabla ya kufanyika tamasha hilo, wasanii watapata fursa ya kupata uwelewa wa biashara ya muziki kutoka kwa wadau wakubwa wa muziki.

"Tunatarajia kuwa na watu kutoka katika makampuni makubwa ya kurekodi Muziki ya Universal, Sony na watu wa Boomplay ambao watatoa mada mbalimbali.

"Tunaishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Utamaduni kwa ushirikiano wao, tunatarajia kuwa na wasanii 30 kutoka hapa Tanzania na wengine 30 kutoka Mataifa mengine ambao wote watatoa burudani kwenye tamasha," alisema Eddy.

Aidha, msanii Faridi Kubanda 'Fid Q' ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Shirikisho la wasanii Tanzania, aliwataka wasanii wenzake kuchangamkia fursa hiyo kuweza kujiimarisha kwenye Muziki na kujitangaza.

## Julio: Yanga SC iwekeze kimataifa

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya timu ya Yanga kutoka suluhu dhidi ya Club African kwenye mchezo wa kwanza wa kufuzu hatua ya makundi kwenye kombe la Shirikisho Afrika, CAF, mchezaji na kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kiwelu Julio ameitaka timu hiyo kukubali kujiwekeza kwa muda mrefu ili kufanya vizuri kimataifa.

Akizungumza na Nipashe, Julio amesema kuwa, kila kitu kinahitaji maandalizi hivyo Yanga hawawezi kufanya usajili mara moja na kutarajia matokeo mazuri, jambo linalohitaji muda kama walivyofanya wenzao Simba.

"Maamuzi yanatukosti sana, leo Yanga wanakuwa bora kwenye ligi ya ndani kwa sababu ya kubebwa na waamuzi, wanatakiwa kuwekeza kimataifa," alisema.

"Ukizungumzia Simba ipo kwenye kiwango kwa sababu imejiandaa kwa muda mrefu, Yanga wasitegemee ubingwa tu wa mwaka jana kumnunua Aziz Ki, Mayele tayari watakwenda kushindana kama Simba.

"Na si kwamba wachezaji hawa ni wabaya, bado hawajapata muunganiko na wachezaji waliokuwepo kwa kuwa ni wachezaji wapya hawajawajua sawasawa kina Fei wacheze nao vipi, ushindi wao unatokana na juhudi binafsi.

"Ki ukweli ukilinganisha Simba na Yanga katika Ligi ya ndani na mashindano ya kimataifa, Simba wapo vizuri zaidi kwa kuwa wamejiwekeza muda mrefu hata baadhi ya wachezaji wakiondoka na kuja wengine wanawahi kukopi mfumo na wanafanya vizuri.

"Yanga waache kuwapa presha wachezaji na badala yake viongozi wasajili timu kwelikweli na wakubali kukaa kwa muda mrefu kwa kujipanga ili mambo yaende," alisema Julio.

## Polisi Tanzania yahamia Karatu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Polisi Tanzania imetangaza rasmi kuhamia kwenye Uwanja wa Black Rhino Karatu, Arusha kwa ajili ya mechi zake za Ligi Kuu baada ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) kuufungia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Robert Munisi amesema jana kuwa wamehamia kwenye uwanja huo wa Karatu kwa muda, huku akithibitisha mechi yao dhidi ya Singida Big Stars inayotarajiwa kuchezwa Jumapili ijayo itapigwa kwenye uwanja huo.

"Mechi yetu dhidi ya Singida Big Stars itachezwa kwenye uwanja wa Karatu, tumeuchagua huo kwa sababu ya kufungiwa uwanja wa Sheikh Amri Abeid na Bodi kututaka tuchague uwanja mwingine," alisema Munisi.

Hata hivyo alisema wamewatumia barua Bodi kwa ajili ya kwenda kuukagua uwanja wao wa Ushirika Moshi ambao wanaamini uko tayari kwa Ligi Kuu baada ya kuufanyia marekebisho.

"Kama ukikaguliwa na kupitishwa basi tutarejea kwenye uwanja wetu wa Ushirika," alisema.

Polisi Tanzania ilikuwa inatumia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid baada ya Uwanja wa Ushirika Moshi kuanza kufungiwa kwa kutokidhi viwango. Hiyo inakuja siku mbili tu baada ya Bodi ya Ligi Kuu kuvifungia viwanja wa Sheikh Amri Abeid, Ali Hassan Mwinyi, Tabora na Gwambina Complex kwa kile walichodai kukosa vigezo vya kikanuni na sheria za mpira wa miguu.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa eneo la kuchezea 'pitch' za viwanja vyote hivyo vitatu hakuna majani ya kutosha kama ilivyoainishwa kwenye masharti ya kanuni za leseni za klabu hivyo kuufanya kutokuwa salama kwa watumiaji pamoja na kupunguza ubora wa picha za matangazo ya televisheni zinazorushwa na kupunguza hali ya ushindani ambao ndiyo chanzo cha ubora wa michezo na ligi kwa ujumla.

## ZISIKUPITE

### JOAO KUUZWA

KLABU ya Atletico Madrid wako tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa Ureno Joao Felix mwenye umri wa miaka 22 msimu ujao, ambapo pia analengwa na Manchester United. (***Cedena SER via Express***)

### MALINOVSKYI KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefikia makubaliano ya kumsaini kiungo wa kati wa Atalanta na Ukraine, Ruslan Malinovskyi mwenye umri wa miaka 29, Januari. (***Il Giorno via Express***)

### ENZO ATAKIWA LEICESTER

KLABU ya Leicester City imekuwa ikimtafuta kiungo wa kati wa Lorient, Mfaransa Enzo le Fee mwenye umri wa miaka 22, kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Youri Tielemans wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 25, ambaye alihusishwa na uhamisho wa Arsenal kipindi cha majira ya joto. (***90 min***)

### ARTETA KUIMARISHA KIKOSI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema "ataangalia kila kitu" kuhusu uimarishaji wa kikosi chake Januari huku Washikabunduki hao wakilenga kudumisha changamoto ya ushindi. (***Express***)

### ARSENAL NA VIWANGO

MIKEL Arteta anataka kuleta wachezaji wa "kiwango kingine" kwa Arsenal Januari, huku winga wa Orlando City na Uruguay, Facundo Torres mwenye umri wa miaka 22 na winga wa Shakhtar Donetsk wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, wakiongoza orodha ya wachezaji wanaolengwa. (***Mail***)

### RASHFORD MKATABA MPYA

KLABU ya Manchester United ina imani mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 25 na beki wa kulia wa Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, wataongeza mikataba yao na klabu hiyo. Ni miongoni mwa wachezaji kadhaa ambao mikataba yao inaisha msimu wa joto, akiwemo mlinda lango wa Hispania, David de Gea mwenye miaka 31, beki wa kushoto wa England, Luke Shaw mwenye miaka 27 na fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye miaka 37. (***90min***)

### TORRES ATAKIWA VILLA

ASTON Villa wamemfanya mlinzi wa Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25, kuwa mchezaji wanayemlenga zaidi baada ya kumteua Unai Emery kuwa kocha wao mpya. (***Football Insider***)

### TETE AGOMBEWA

KLABU ya West Ham United imeungana na Southampton, Leicester City na Brentford kumfuatilia winga wa Brazil, Tete mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwa mkopo Lyon kutoka Shakhtar Donetsk. (***Sun***)

### MESSI VIPAUMBELE

MKATABA mpya wa Lionel Messi wa Paris St-Germain unajumuisha kipengele kinachomruhusu fowadi huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 35, kuweka vipaumbele vya kimataifa kabla ya klabu yake kuelekea kile kinachotarajiwa kuwa Kombe lake la mwisho la Dunia. (***TN via Express***)


### FIRMINO KUONGEZEWA

KLABU ya Liverpool inajiandaa kuanzisha mazungumzo kuhusu mkataba mpya na mshambuliaji wa Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31. (***Football Insider***)

### LOPETEGUI KUTUA WOLVES

KLABU ya Wolves inatarajiwa kumteua, Julen Lopetegui kuwa kocha wao mpya mnamo Novemba 13, siku moja baada ya kucheza na Arsenal katika mechi yao ya mwisho kabla ya mapumziko ya Kombe la Dunia. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PIQUE KUSTAAFU BARCELONA LEO

### Anatundika daruga rasmi baada ya kushinda kila taji kwenye soka na...

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa Barcelona, Gerard Pique amesema leo Jumamosi anastaafu kucheza soka baada ya mechi yake ya mwisho kwenye uwanja wa Nou Camp.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye alikulia hapo Barcelona na baadae kucheza kwa misimu minne kule Manchester United, alitoa tangazo hilo kwenye video iliyowekwa kwenye mtandao wa kijamii.

**Barca itacheza na Almeria kwenye mchezo wa Ligi Kuu, LaLiga, leo na ndio itakuwa mechi yake ya mwisho Pique.**

"Siku zote nimekuwa nikisema kwamba hakutakuwa na timu nyingine baada ya Barca na hivyo ndivyo itakavyokuwa," alisema.

Pique alikuwa mchezaji wa vijana na Barca hadi mwaka 2004 aliposajiliwa na Man United.

Alikuwa mchezaji mlinzi wa pembeni wa Mashetani Wekundu waliposhinda Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2007-08, na akajiunga tena na wababe hao wa Katalunya mwaka 2008.

Katika muda wake Barcelona amecheza zaidi ya michezo 600 na kushinda mataji 30, yakiwemo mataji manane ya LaLiga, matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na saba ya Copa del Rey.

Msimu huu Barcelona imetolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa LaLiga, pointi moja nyuma ya Real Madrid.

Pique alistaafu kucheza soka la kimataifa mwaka wa 2018 baada ya kuichezea Hispania jumla ya mechi 102 na kutwaa Ubingwa wa Ulaya mwaka 2012 na Kombe la Dunia mwaka 2010.

Alisema: "Mpira umenipa kila kitu. Barca wamenipa kila kitu. Ninyi, mashabiki mmenipa kila kitu.

"Na sasa kwa kuwa ndoto zote za mtoto (mwenyewe) zimetimia, nataka kusema kwamba nimeamua sasa ni wakati wa kukamilisha safari hii."

Pia alitania angerudi kwenye uwanja maarufu wa Barca, akisema: "Mnanifahamu, muda si mrefu nitarejea. Mtaniona Camp Nou. Barca iishi muda mrefu zaidi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,046,4
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
FULHAM
1 | 1.15
X | 7.34
2 | 13.66
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WERNER KUTOCHEZA KOMBE LA DUNIA



**MUNICH, Ujerumani**

FOWADI wa Ujerumani, Timo Werner hatashiriki Kombe la Dunia baada ya kupasuka kifundo cha mguu alipokuwa akiichezea RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, siku ya Jumatano.

Werner aliumia katika kipindi cha kwanza baada ya kufanyiwa faulo na Taras Stepanenko wa Shakhtar Donetsk, na alitolewa baada ya kujaribu kuendelea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alibadilishwa na Emil Forsberg dakika ya 19 na Leipzig wakashinda mchezo huo kwa mabao 4-0, na hivyo kujihakikishia nafasi ya kuingia hatua ya 16 bora.

Leipzig siku ya Alhamisi ilitangaza Werner hatacheza tena mwaka huu, ikisema kwenye Twitter: "Timo Werner alipata jeraha la kifundo cha mguu jana (juzi) usiku katika ushindi dhidi ya Shakhtar Donetsk.

"Vipimo vinaonesha kuwa kwa bahati mbaya amepasua kifundo cha mguu wake wa kushoto na kwa hiyo atakuwa nje kwa mwaka wote 2022."

Tangu aanze kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2017, Werner amefunga mabao 24 katika mechi 55 kwa nchi yake.

Alijiunga tena na Leipzig Agosti baada ya misimu miwili na Chelsea na amefunga mabao tisa katika mechi 16 za klabu hiyo ya Bundesliga, lakini hatapanda ndege kwenda Qatar.

Habari hizi ni pigo kwa kocha mkuu wa Ujerumani, Hansi Flick anapojiandaa kwa michuano yake mikubwa ya kwanza tangu achukue mikoba ya Joachim Low, na mchezo wao wa ufunguzi utakuwa dhidi ya Japan Novemba 23 mwaka huu.

# Atletico Madrid yamuweka sokoni Joao

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid imemuweka sokoni Joao Felix na sasa wako tayari kupokea ofa yoyote, kwa mujibu wa Cadena SER.

Joao ambaye Atleti ilimsajili kwa euro milioni 126 kutoka Benfica kwa mkataba wa miaka saba mwaka 2019 kwa sasa amekuwa hana nafasi ndani ya kikosi hicho.


Fowadi huyo wa Ureno ameshindwa kupata nafasi huu, akiwa na mabao mawili pekee.

Awali Bayern Munich walidaiwa kupeleka ofa ya euro milioni 100 kumnunua Felix katika msimu wa joto, huku Manchester United ikiripotiwa kutoa ofa ya euro milioni 130 iliyokataliwa Agosti.

Mapema mwezi uliopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 aliwasilisha ombi la kutaka kuondoka klabuni hapo.

Mchezaji huyo ameonesha kabisa kwamba, hana furaha baada ya kushindwa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara chini ya kocha, Doiego Simeone.

Klabu ya Paris Saint-Germain na Barcelona hivi karibuni nazo zilihusishwa na kuwania kumchukua mchezaji huyo.



HABARI MICHEZO

433,814/-

# KMC YAITISHIA NYAU GEITA GOLD

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KMC ambayo imepiga kambi Kanda ya Ziwa kujiandaa na mechi dhidi ya Geita Gold mchezo unaotarajiwa kupigwa Novemba 11 kwenye Uwanja wa Nyamkumbu, imesema haitokubali kupoteza tena mechi hiyo.

Afisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala amesema baada ya kupoteza mechi mbili mfululizo kwa kufunga bao 1-0 dhidi ya Yanga pamoja na Kagera Sugar, wamejiandaa kikamilifu kuhakikisha hawapotezi tena mechi ya tatu watakayocheza dhidi ya timu hiyo.

"Tulipoteza mechi yetu dhidi ya Geita Gold kwa bao 1-0, ni mechi ya pili mfululizo kupoteza, lakini hii haiwezi kuonesha kwamba sisi si bora na tutauonyesha kwenye mechi hiyo tutakayochezwa Novemba 11.

Kwa sasa tupo hapa hapa mkoani Kagera, isingewezekana kurudi Dar baada ya kucheza dhidi ya Kagera, halafu turudi tena kucheza dhidi ya Geita Gold, badala yake tumepiga kambi huku huku kwa ajili ya mechi hiyo, najua mchezo utakuwa mgumu lakini tunajipanga vizuri, ila tunaomba tu wasitufanyie vurugu kama walivyotufanyia msimu uliopita kwa sababu sisi hatukulipiza walipokuja Dar," alisema.

Mpaka sasa KMC imecheza mechi 10 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 13 ikiwa kwenye nafasi ya nane, huku timu itakayocheza nayo mpaka jana ilikuwa kwenye nafasi ya tisa ikiwa na pointi 13 kwa mechi 10, lakini KMC inakaa juu kwa tofauti ya bao moja tu la kufunga, ikipachika mabao 10, Geita Gold ikiwa imefunga mabao tisa.



Baadhi ya wanafunzi wa shule ya Msingi Minazini, wakifanya igizo kuhusu ukatili wa kijinsia, katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike, yaliyoandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), na kufanyika kwenye viwanja vya Sekondari ya Makumbusho, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens vitani tena leo

INATOKA UK. 32

"Malengo yetu ni kufanya vizuri katika kila mechi tunayocheza, wachezaji wote tumejipanga kupambana zaidi, tunahitaji kuipa heshima klabu yetu ya Simba na nchi, tunajua nyumbani watu wote wanatufuatilia, hatutawaangusha," alisema mshambuliaji huyo.

Mechi nyingine za mwisho za hatua ya makundi zitachezwa kesho jijini Rabat kwa TP Mazembe Queens ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuvaana na Mamelodi Sundowns Queens ya Afrika Kusini wakati Waarabu wa Misri ambao wamefungwa mechi mbili za kwanza, Wadi Degla itachuana na Bayelsa kutoka Nigeria.

Mamelodi Sundowns Queens ndio mabingwa watetezi wa michuano hii ambayo mshindi atajinyakulia kitita cha Dola za Marekani 400,000 na mshindi wa pili ataondoka na Dola za Marekani 250,000 huku timu nyingine zilizoingia hatua ya nusu fainali zitaambulia Dola za Marekani 200,000 kila moja.

# Yanga kazi moja tu

INATOKA UK. 32

Baada ya Dubai, msafara huo utalala hapo kisha Novemba 5, kuanza safari kwenda Tunisia na kuwasili kwenye uwanja wa ndege wa Carthage.

Mara baada ya kuwasili, kikosi kitaanza safari kwenda mji wa Sousse kuweka kambi ya siku mbili na baadaye kwenda katika mji ambao watachezea mechi hiyo.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/11/22 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.83 | 3.23 | 2.48 |
| 02. 05/11/22 | 18:00 | QPR vs West Bromwich | 2.44 | 3.29 | 2.84 |
| 03. 05/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Brentford | 2.73 | 3.28 | 2.54 |
| 04. 05/11/22 | 19:00 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.73 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 05/11/22 | 20:00 | Galatasaray vs Besiktas | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 06. 05/11/22 | 20:30 | Everton vs Leicester | 2.33 | 3.27 | 3.03 |
| 07. 05/11/22 | 21:00 | PAU FC vs Amiens | 2.79 | 3.14 | 2.64 |
| 08. 05/11/22 | 21:00 | Bastia vs Paris FC | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 09. 05/11/22 | 21:00 | Dijon vs Guingamp | 2.50 | 3.16 | 2.96 |
| 10. 05/11/22 | 22:30 | Arminia Bielefeld vs Kaiserslautern | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 06/11/22 | 14:30 | Bologna vs Torino | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 12. 06/11/22 | 15:00 | Chelsea vs Arsenal | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 13. 06/11/22 | 15:30 | KAA Gent vs Brugge | 2.54 | 3.59 | 2.54 |
| 14. 06/11/22 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Greuther Furth | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 15. 06/11/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.31 | 3.52 | 2.83 |
| 16. 06/11/22 | 19:05 | Lille vs Rennes | 2.48 | 3.48 | 2.63 |
| 17. 06/11/22 | 19:30 | Tottenham vs Liverpool | 2.88 | 3.53 | 2.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 05/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1269 | Giresunspor vs Istanbulspor | 1.89 | 3.43 | 3.93 |
| 15:30 | 1838 | Sheffield Utd vs Burnley | 2.45 | 3.27 | 2.73 |
| 16:00 | 2189 | Maccabi Tel Aviv vs Sectzya Nes Ziona | 1.09 | 7.81 | 17.56 |
| 16:00 | 2604 | Getafe vs Cadiz CF | 2.16 | 3.05 | 3.60 |
| 16:00 | 2749 | Musanze vs Mukura | 2.20 | 3.00 | 3.60 |
| 16:00 | 2873 | Red Arrows vs Forest Rangers | 1.75 | 2.91 | 5.43 |
| 17:00 | 1173 | Salernitana vs Cremonese | 2.08 | 3.36 | 3.32 |
| 17:00 | 2399 | CR Belouizdad vs El Bayadh | 1.26 | 4.66 | 10.69 |
| 17:00 | 4757 | Empoli vs Sassuolo | 2.67 | 3.37 | 2.45 |
| 17:30 | 1223 | Augsburg vs Eintracht Frankfurt | 4.15 | 3.90 | 1.72 |
| 17:30 | 1336 | Borussia Dortmund vs VfL Bochum | 1.22 | 6.17 | 9.95 |
| 17:30 | 3333 | Hoffenheim vs RB Leipzig | 2.87 | 3.46 | 2.26 |
| 17:30 | 3951 | Hertha BSC vs Bayern Munchen | 8.72 | 6.34 | 1.24 |
| 17:30 | 4469 | Mainz vs VfL Wolfsburg | 1.98 | 3.52 | 3.42 |
| 18:00 | 1259 | Manchester City vs Fulham | 1.15 | 7.34 | 13.66 |
| 18:00 | 1328 | Millwall vs Hull City | 1.81 | 3.41 | 4.26 |
| 18:00 | 1609 | Blackpool vs Luton Town | 2.72 | 3.26 | 2.46 |
| 18:00 | 1699 | Sunderland vs Cardiff | 2.20 | 3.17 | 3.22 |
| 18:00 | 2176 | Leeds vs Bournemouth | 1.70 | 3.81 | 4.35 |
| 18:00 | 2477 | Middlesbrough vs Bristol City | 1.81 | 3.50 | 4.15 |
| 18:00 | 2678 | Stoke City vs Birmingham | 2.04 | 3.42 | 3.37 |
| 18:00 | 3286 | QPR vs West Bromwich | 2.47 | 3.32 | 2.67 |
| 18:00 | 3328 | Nottingham vs Brentford | 2.68 | 3.22 | 2.53 |
| 18:00 | 3579 | Wolverhampton vs Brighton | 3.27 | 3.22 | 2.15 |
| 18:00 | 3802 | Rotherham vs Norwich City | 3.66 | 3.46 | 1.93 |
| 18:00 | 4467 | Celtic vs Dundee Utd | 1.08 | 9.35 | 21.88 |
| 18:00 | 4653 | Swansea vs Wigan | 1.90 | 3.37 | 3.87 |
| 18:00 | 5903 | CRS Salmi vs Raja Casablanca | 4.38 | 2.68 | 2.01 |
| 18:00 | 5911 | Watford vs Coventry | 1.90 | 3.42 | 3.82 |
| 18:15 | 1755 | Valladolid vs Elche | 1.80 | 3.60 | 4.21 |
| 18:30 | 1861 | Hapoel Hadera vs Maccabi Netanya | 3.55 | 3.26 | 1.96 |
| 18:30 | 4801 | FC Vizela vs FC Arouca | 1.93 | 3.23 | 4.07 |
| 19:00 | 2510 | Hapoel Haifa vs Hapoel Katamon | 2.59 | 3.28 | 2.45 |
| 19:00 | 3438 | CSKA Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.31 | 4.93 | 8.68 |
| 19:00 | 4023 | AC Ajaccio vs Strasbourg | 2.74 | 3.09 | 2.59 |
| 19:00 | 4527 | Orlando Pirates vs Amazulu | 1.90 | 3.10 | 3.98 |
| 19:30 | 5926 | ASC Diambars vs Casa Sport | 3.55 | 2.70 | 2.40 |
| 20:00 | 2488 | Atalanta vs Napoli | 3.27 | 3.52 | 2.04 |
| 20:00 | 3957 | MC Oran vs Paradou AC | 2.11 | 2.78 | 3.76 |
| 20:00 | 4464 | Galatasaray vs Besiktas | 2.09 | 3.48 | 3.23 |
| 20:00 | 4871 | MAS Maghrib A Fes vs Mouloudia Oujda | 1.64 | 3.25 | 5.44 |
| 20:30 | 3308 | Werder Bremen vs Schalke 04 | 1.61 | 4.16 | 4.55 |
| 20:30 | 3318 | FC Ashdod vs Hapoel Tel Aviv | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 20:30 | 4529 | Celta Vigo vs Osasuna | 2.09 | 3.26 | 3.51 |
| 20:30 | 4644 | Everton vs Leicester | 2.35 | 3.27 | 2.87 |
| 21:00 | 4335 | Porto vs Pacos Ferreira | 1.12 | 7.97 | 18.92 |
| 22:45 | 1796 | AC Milan vs Spezia | 1.20 | 6.15 | 11.90 |
| 23:00 | 2470 | Barcelona vs Almeria | 1.14 | 7.77 | 16.05 |
| 23:00 | 2813 | Angers vs Lens | 4.57 | 3.88 | 1.67 |
| 23:30 | 2955 | Sporting Lisbon vs Vitoria Guimaraes | 1.32 | 4.99 | 8.59 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Novemba 5, 2022

Nipashe





## Pique kustaafu Barcelona leo



Timu ya Simba Queen ikiwa mazoezini **PICHA:SOMOE NG'ITU**

# YANGA KAZI MOJA TU KWA CLUB AFRICAIN

●●●Yapaa kuifuata Tunisia, Rais Hersi ataka mshikamano, kuweka kambi siku mbili kabla ya...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kimeondoka jana mchana na matumaini ya kufanya vizuri katika mchezo wake wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika, CAF, dhidi ya Club Africain.

Timu hiyo imeelekea Tunisia na itaweka kambi ya siku mbili kwenye mji wa Sousse na kurejea jijini Tunis kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya wenyeji hao, utakaochezwa Novemba 9, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema maandalizi yako vizuri na wana imani ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano.

Alisema anaimani mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kutafuta ushindi na wenyeji wao watacheza kwa kufunguka kutafuta matokeo mazuri.

"Tumeona walivyocheza hapa nyumbani, walizuia sana na kupoteza muda, mechi ya marudiano hawatacheza hivyo kwa sababu wako nyumbani na watafunguka kwa ajili ya kutafuta ushindi na tumefanyia kazi makosa yetu na matumaini yetu ni kutafuta ushindi.

"Tumeona madhaifu yetu kwenye mechi ya kwanza na yanaendelea kufanyiwa kazi na tuna imani kubwa wachezaji wakijitoa tutasonga katika hatua inayofuata kwenye michuano hii," alisema Kaze.

Katika hatua nyingine, Rais wa Yanga, Hersi Said amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuendelea kuonyesha umoja na mshikano katika kipindi hiki ambacho timu yao inaenda kupambana.

Alisema wamepokea na kufanyia kazi mapendekezo yote yanayotolewa na mashabiki na wanachama katika mapungufu ili kujenga klabu yao kuwa imara zaidi.

"Niwaombe mashabiki na wanachama, wapuuze kejeli zilizopo sasa na kuonyesha mshikamano kwa viongozi, wachezaji na benchi la ufundi katika kufikia malengo yetu.

"Timu inaenda nchini Tunisia katika mchezo wa marudiano huu ni wakati wanachama kuunga mkono wachezaji, benchi la ufundi ili kufanya vizuri katika mchezo wetu huo dhidi ya Club Africain," alisema Hersi.

Alisema wanajivunia kutofungwa mechi 45 na kutwaa taji la kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo limeletwa na wachezaji na benchi hili la ufundi la sasa.

Hersi alisema wanachama wanatakiwa kuonesha mshikamano na kuendelea kusapoti timu hiyo kwa kipindi hiki ambacho inaenda nchini Tunisia kwa ajili ya kutafuta ushindi dhidi ya Club Africain.

Kikosi cha Yanga kimesafiri jana mchana kuelekea Tunisia, msafara huo wenye wachezaji 22 na viongozi 9 uliondoka kwa ndege ya Shirika la ndege la Emirates.

INAENDELEA UK. 31

## Simba Queens vitani tena leo

**Na Somoe Ng'itu, MARRAKECH**

WAWAKILISHI wa Afrika Mashariki na Kati, Simba Queens, kutoka Tanzania, inatarajia kukutana na Green Buffalo kutoka Zambia katika mechi ya mwisho ya Kundi A itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Grand de Stade Marrakech, nchini Morocco.

Simba Queens yenye pointi tatu sawa na wapinzani wao, itashuka uwanjani ikihitaji matokeo ya ushindi tu ili iweze kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake wakati Wazambia hao wanahitaji sare.

Tayari wenyeji, ASFAR FC yenye pointi sita na leo itamaliza hatua hiyo ya makundi kwa kuwavaa Determine Girls kutoka Liberia wameshatangulia hatua ya nusu fainali sambamba na Mamelodi Sundowns Queens ya Kundi B.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, aliiambia Nipashe wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na watashuka dimbani kwa ajili ya kupambana kuhakikisha wanaondoka na ushindi.

Lukula alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye upinzani kutoka katika kila upande kwa sababu timu zote zinahitaji na zina nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hii.

Kocha huyo alisema anaawaamini wachezaji wake wakitulia wataibuka na ushindi na endapo watafanikiwa kumfunga Green Buffalo, hakuna kitakachowazuia kutwaa ubingwa wa mashindano haya kwa mwaka huu.

"Nina timu nzuri, inafanya vizuri pia mazoezini, kama wataonyesha ubora wao, ninawaamini watafunga mabao na tutasonga mbele, lakini ninajua mechi haitakuwa rahisi, pia tunaomba bahati iwe upande wetu," kocha huyo raia wa Uganda alisema.

Naye nahodha wa Simba Queens, Oppa Clement, alisema wachezaji wote wana ari na wamepania kucheza katika kiwango cha juu katika mchezo huo.

Oppa alisema malengo yao ni kurudi nyumbani na taji hilo na hakuna ambacho kitawazuia endapo watavuka 'mtihani' unaowakabili leo wa kuwaondoa Green Buffalo.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >